

# YALIYOMO

<b>1.0</b>	<b>UTANGULIZI.....</b>	<b>3</b>
<b>2.0</b>	<b>HALI YA SEKTA YA MAJI NCHINI.....</b>	<b>5</b>
2.1	<i>RASILIMALI ZA MAJI.....</i>	5
2.2	<i>HUDUMA YA MAJI VIJJINI .....</i>	8
2.3	<i>HUDUMA YA MAJI MIJINI.....</i>	8
2.4	<i>KUJENGA UWEZO WA KITAASISI.....</i>	11
<b>3.0</b>	<b>UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2014/2015 NA MALENGO KWA MWAKA 2015/2016.....</b>	<b>12</b>
3.1	<i>RASILIMALI ZA MAJI.....</i>	12
3.1.1	Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji .....	12
3.1.2	Ubora na Usafi wa Maji .....	24
3.2	<i>HUDUMA YA MAJI VIJJINI .....</i>	30
3.2.1	Mpango wa “Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa” <i>(Big Results Now – BRN) .....</i>	30
3.2.2	Utekelezaji wa BRN kwa Miradi ya Maji Vijiijini.....	31
3.2.3	Mpango wa BRN kwa mwaka 2015/2016 .....	32
3.2.4	Hali ya Utekelezaji wa Miradi ya Maji Vijiijini .....	32
3.3	<i>HUDUMA YA MAJI MIJINI.....</i>	41
3.3.1	Kuboresha Huduma za Maji Mijini.....	41
3.3.2	Kuboresha Huduma ya Maji katika Miji ya Mpanda, Njombe na Bariadi .....	51
3.3.3	Usanifu wa Miradi ya Maji katika Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo .....	53
3.3.4	Miradi ya Kutoa Maji kutoka Ziwa Victoria Kupeleka Miji Mbalimbali.....	54
3.3.5	Miradi katika Jiji la Dar es Salaam .....	55
3.3.6	Huduma ya Maji katika Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa .....	60
3.3.7	Miradi ya Maji ya Kitaifa .....	65
3.3.9	Kuzijengea Uwezo Mamlaka za Maji Mijini .....	68
3.4	<i>TAASISI ZA WIZARA YA MAJI.....</i>	70
3.4.1	Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji <i>(EWURA) .....</i>	70
3.4.2	Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji.....	72

3.4.3 Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa ( <i>DDCA</i> ).....	73
3.4.4 Bohari Kuu ya Maji.....	73
<b>3.5 MASUALA MTAMBUKA.....</b>	<b>75</b>
3.5.1 Sheria .....	75
3.5.2 Habari, Elimu na Mawasiliano.....	76
3.5.3 Teknolojia ya Habari na Mawasiliano .....	76
3.5.4 Jinsia.....	77
3.5.5 UKIMWI .....	78
3.5.6 Maendeleo ya Rasilimali Watu .....	78
3.5.7 Mapambano Dhidi ya Rushwa.....	80
3.5.8 Uratibu wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji .....	80
<b>3.6 CHANGAMOTO NA HATUA ZINAZOCHUKULIWA.....</b>	<b>83</b>
<b>4.0 SHUKRANI.....</b>	<b>88</b>
<b>5.0 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2015/2016.....</b>	<b>89</b>

**HOTUBA YA WAZIRI WA MAJI**  
**MHE. PROF. JUMANNE ABDALLAH MAGHEMBE (MB) AKIWASILISHA BUNGENI**  
**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA MAJI**  
**KWA MWAKA 2015/2016**

### **1.0 UTANGULIZI**

1. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu, baada ya kupokea taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa **Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Profesa Peter Mahamudu Msolla, Mbunge wa Kilolo**, ambayo ilichambua bajeti ya Wizara ya Maji; naomba sasa Bunge lako likubali kupokea, kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2015/2016.
2. **Mheshimiwa Spika**, nachukua fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa ushauri, maoni na ushirikiano mkubwa walioutoa wakati wa uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2014/2015 pamoja na mpango na bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2015/2016. Napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kwamba maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati yamezingatiwa katika bajeti hii.
3. **Mheshimiwa Spika**, kipekee kabisa naomba kumpongeza **Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuteuliwa na **Bw. Ban Ki Moon**, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, kuwa Mwenyekiti wa Jopo la Ngazi ya Juu kuhusu Mwitikio wa Kimataifa wa Majanga ya Afya (*High-Level Panel on Global Responses to Health Crisis*). Vilevile, nampongeza kwa kukabidhiwa Uenyekiti wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki za Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi na Tanzania. Kukabidhiwa kwake majukumu haya makubwa kunaonesha uongozi wake mahiri na madhubuti katika nyanja mbalimbali kitaifa na kimataifa.

Vilevile, napenda kukupongeza Mheshimiwa Spika, kwa kazi nzuri unayoifanya katika kuliwakilisha vizuri Bunge letu Tukufu kitaifa na kimataifa. Nichukue fursa hii kukupongeza kwa kuchaguliwa kwako mwezi Novemba, 2014 kuwa Rais wa Bunge la SADC kwa kipindi cha miaka miwili. Nakuombea kila la kheri na mafanikio katika kutekeleza majukumu hayo.

4. **Mheshimiwa Spika**, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge walioteuliwa kuwa Mawaziri na Manaibu Waziri ili kuziongoza Wizara mbalimbali. Vilevile, nawapongeza Wenyeviti wapya wa Kamati mbalimbali za Kudumu za Bunge waliochaguliwa wakiwemo **Mhe. Amina Mohamed Mwidau**, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali; **Mhe. Festus Bulugu Limbu**, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti na **Mhe. Richard Mganga Ndassa**, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini. Ni mategemeo yangu kuwa katika kipindi hiki kilichobaki tutashirikiana kwa karibu katika kufanikisha majukumu yaliyo mbele ya Bunge letu.

5. **Mheshimiwa Spika**, vilevile, nichukue fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya **Mhe. Dkt. Grace Khwaya Puja** na **Mhe. Dkt. Innocent Sebba** walioteuliwa na **Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kijiunga na Bunge lako Tukufu. Nawatakia heri na mafanikio katika kazi yao hiyo mpya.

6. **Mheshimiwa Spika**, nawashukuru na kuwapongeza **Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb)**, Waziri Mkuu na **Mhe. Mary Michael Nagu (Mb)**, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Uhusiano na Uratibu, kwa hotuba zao ambazo zimetoa mwelekeo wa bajeti na uchumi kwa mwaka 2015/2016 pamoja na utekelezaji wa kazi za Serikali kwa mwaka 2014/2015. Nawapongeza pia, Mawaziri wenzangu wote walionitangulia kuwasilisha hoja zao.

7. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu ilipokea kwa mshtuko na masikitiko makubwa, taarifa ya kifo cha kipenzi chetu, marehemu **Kapteni John Damiano Komba** aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbinga Magharibi. Nachukua nafasi hii kutoa pole kwako wewe Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu, familia ya marehemu, ndugu na wananchi wa jimbo la Mbinga Magharibi pamoja na Watanzania wote kwa msiba huo mkubwa. Marehemu pamoja na ubunge wake, alikuwa msanii mahiri ambaye Taifa litamkumbuka daima. Vilevile, natoa pole za dhati kwa wananchi waliopoteza ndugu zao na mali kutokana na matukio ya ajali za barabarani, maafa ya mafuriko na mvua kubwa katika maeneo mbalimbali nchini. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote mahali pema peponi. **Amin**.

8. **Mheshimiwa Spika**, napenda sasa kuchukua fursa hii kuwasilisha hotuba ya bajeti ya Wizara yangu ambayo inatoa taarifa ya hali ya Sekta nchini; utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2014/2015 na malengo ya mwaka 2015/2016; na maombi ya fedha kwa mwaka 2015/2016.

## **2.0 HALI YA SEKTA YA MAJI NCHINI**

**9. Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu inatekeleza mipango ya Serikali kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Malengo ya Maendeleo ya Milenia 2015; Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA II); Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010-2015; Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 - 2015/2016); Mpango wa “Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa” (*Big Results Now - BRN*) na Ahadi za Serikali. Aidha, Wizara inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maji chini ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji kwa mujibu wa Sera ya Maji ya mwaka 2002; Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Maji (2006 – 2015); pamoja na Sheria za Maji na Kanuni zake.

**10. Mheshimiwa Spika**, vilevile, Serikali inatekeleza miradi ya maji vijijini kupitia mpango wa *BRN* ambapo Sekta ya Maji ni moja ya sekta sita zilizopewa kipaumbele katika mpango huo. Awamu ya kwanza ya mpango huo wa miaka mitatu (2013/2014 – 2015/2016) ilianza kutekelezwa mwezi Julai, 2013. Katika awamu hiyo, jumla ya miradi **1,810** inatarajiwa kujengwa na itakapokamilika jumla ya vituo **56,981** vya kuchotea maji vitajengwa na wananchi wapatao **milioni 15.4** zaidi watanufaika hivyo kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji vijijini kufikia **asilimia 74**. Kutokana na mpango huo kuonesha mafanikio katika kutekeleza miradi ya maji vijijini, nimeziagiza Idara zote pamoja na Taasisi zilizo chini ya Wizara yangu kuanza kutekeleza majukumu yao kupitia mpango wa “Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa”.

**11. Mheshimiwa Spika**, Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji inatekelezwa katika vipindi vya miaka mitano kuanzia mwaka 2006/2007 hadi mwaka 2024/2025. Hadi sasa, hali halisi ya utekelezaji katika Sekta ya Maji imefikia hatua mbalimbali kama ifuatavyo:-

### **2.1 RASILIMALI ZA MAJI**

**12. Mheshimiwa Spika**, Rasilimali za maji zilizopo Tanzania kwa sasa zinakadiriwa kuwa **kilomita za ujazo 87** juu ya ardhi na **kilomita za ujazo 38** chini ya ardhi. Rasilimali hizo zinatumika kwa matumizi mbalimbali ikiwemo majumbani, kilimo cha umwagiliaji, uzalishaji wa nishati, mifugo, uvuvi, viwanda, uchimbaji wa madini, usafirishaji, utalii na ujenzi. Hata hivyo, mtawanyiko na upatikanaji wa rasilimali hizo nchini hauko sawa katika maeneo yote kutokana na tofauti za kijiografia, kijiolojia na mabadiliko ya hali ya hewa. Vilevile, rasilimali za maji zinatumika kwa ajili ya kuhifadhi bioanuai na kupokea majitaka yaliyosafishwa na kufikia viwango vinavyokubalika baada ya matumizi. Usimamizi wa vyanzo vya maji nchini unaendelea kutekelezwa na Bodi za Maji za Mabonde yote tisa kwa kufuata kanuni za usimamizi wa rasilimali za maji.

**13. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa kihaidrolojia unaoanzia mwezi Novemba 2013 hadi Oktoba 2014, maeneo mengi nchini yalipata mvua za kuridhisha na kuongeza kiasi cha maji katika mito na mabwawa. Hata hivyo, hali ya upatikanaji wa mvua katika mabonde ya maji nchini ilitofautiana kulingana na tabia za hali ya hewa. Wastani wa viwango vya mvua katika mabonde yote **tisa** nchini vilikuwa kama

ifuatavyo:- Bonde la Pangani **milimita 817** ikilinganishwa na **milimita 720** kwa mwaka wa kihaidrolojia uliopita; Bonde la Rufiji **milimita 1,271** ikilinganishwa na **milimita 1,144**; Bonde la Wami/Ruvu **milimita 2,306** ikilinganishwa na **milimita 979**; Bonde la Ziwa Nyasa **milimita 1,643** ikilinganishwa na **milimita 1,356**; Bonde la Ziwa Victoria **milimita 1,450** ikilinganishwa na **milimita 968**; Bonde la Kati **milimita 774** ikilinganishwa na **milimita 825** ya mwaka uliopita, katika Bonde la Ziwa Rukwa **milimita 900** ikilinganishwa na **milimita 844**; Bonde la Ziwa Tanganyika **milimita 1,116** ikilinganishwa na **milimita 917** na katika Bonde la Ruvuma na Pwani ya Kusini wastani wa **milimita 801** ikilinganishwa na **milimita 835** mwaka uliopita. **Jedwali Na.1** linaonesha mwenendo wa viwango vya mvua katika mabonde **tisa** nchini kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia Novemba, 2011 hadi Oktoba, 2014.

**14. Mheshimiwa Spika**, kutokana na takwimu zilizokusanywa, wastani wa viwango vya maji katika mito na mabwawa viliongezeka katika maeneo mengi ikilinganishwa na msimu wa mvua wa mwaka uliopita. Viwango vya mtiririko wa maji katika baadhi ya mito nchini vilikuwa kama ifuatavyo:- Mto Kiwira ulioko Bonde la Ziwa Nyasa ulikuwa na wastani wa **mita za ujazo 61.88** kwa sekunde ikilinganishwa na **mita za ujazo 25.89** kwa sekunde; Mto Wami **mita za ujazo 56.82** kwa sekunde ikilinganishwa na **mita za ujazo 18.69** kwa sekunde; Mto Ruvu **mita za ujazo 48.92** kwa sekunde, ikilinganishwa na wastani wa **mita za ujazo 36.21** kwa sekunde; Mto Ruaha Mkuu **mita za ujazo 42.72** kwa sekunde ikilinganishwa na wastani wa **mita za ujazo 9.91**, Mto Kihansi **mita za ujazo 18.43** kwa sekunde ikilinganishwa na **mita za ujazo 14.35**; Mto Kikuletwa katika Bonde la Pangani ulikuwa na **mita za ujazo 20.16** kwa sekunde ikilinganishwa na kiasi cha **mita za ujazo 14.66** kwa sekunde; Mto Ruvuma **mita za ujazo 11.13** kwa sekunde ikilinganishwa na wastani wa **mita za ujazo 8.31** kwa sekunde mwaka uliopita; Mto Kagera **mita za ujazo 265.93** kwa sekunde ikilinganishwa na **mita za ujazo 368.7** kwa sekunde; na Mto Mara **mita za ujazo 31.75** kwa sekunde ikilinganishwa na **mita za ujazo 56.06** kwa mwaka uliopita.

**15. Mheshimiwa Spika**, kutokana na ongezeko la mvua katika kipindi cha mwaka huo, wastani wa vina vya maji kwenye mabwawa umeongezeka ikilinganishwa na mwaka uliopita. Takwimu za ongezeko hilo katika baadhi ya mabwawa ni kama ifuatavyo:- Bwawa la Nyumba ya Mungu usawa wa maji ulikuwa **mita 684.81** juu ya usawa wa bahari, ikilinganishwa na **mita 683.94** mwaka uliopita; bwawa la Mtera **mita 691.685** ikilinganishwa na **mita 691.18**, Kidatu **mita 448.87** ikilinganishwa na **mita 446.33**, Kihansi **mita 1173.16** ikilinganishwa na **mita 1,144.64**; na bwawa la Mindu ni **mita 507.30** juu ya usawa wa bahari ikilinganishwa na **mita 506.45** mwaka uliopita.

**16. Mheshimiwa Spika**, vilevile, usawa wa maji katika Ziwa Victoria ulikuwa wastani wa **mita 1,133.41** juu ya usawa wa bahari ikilinganishwa na **mita 1,133.22** mwaka uliopita, Ziwa Tanganyika **mita 775.2** ikilinganishwa na **mita 775.0**, na Ziwa Nyasa lilikuwa na wastani wa **mita 475.92** ikilinganishwa na **mita 474.48** juu ya usawa wa bahari kwa mwaka uliopita. Kulingana na takwimu hizo, hali ya maji iliimarika ikilinganishwa na mwaka wa kihaidrolojia uliopita.

**17. Mheshimiwa Spika**, hata hivyo, katika mwaka wa kihaidrolojia ulioanza mwezi Novemba 2014, hali ya upatikanaji wa mvua ilionesa kuwa chini ya wastani na hivyo kuathiri mtiririko wa maji kwenye mito na vina katika mabwawa na maziwa. Vilevile, baadhi ya maeneo yameendelea kuathirika na uhaba wa maji kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kupungua kwa uwezo wa ardhi kuhifadhi maji; athari za mabadiliko ya tabianchi; ongezeko la shughuli za kibinadamu kwenye maeneo ya vyanzo vyaa maji; na kasi kubwa ya ongezeko la watu. Pamoja na changamoto hizo, mvua zinazoendelea kunyesha kwa sasa zinatarajiwa kuongeza wingi wa maji kwenye mito, mabwawa na maziwa na hivyo kuimarisha upatikanaji wa maji katika maeneo mengi nchini.

**18. Mheshimiwa Spika**, takwimu za kitaifa za rasilimali za maji zilizopo zinaonesha kuwa kiasi cha maji kwa sasa kwa kila Mtanzania ni wastani wa **mita za ujazo 1,952** kwa mwaka. Kutokana na kasi ya ongezeko la idadi ya watu nchini, kiasi hicho kinatarajiwa kupungua hadi kufikia **mita za ujazo 883** ifikapo mwaka 2035. Kiwango cha chini cha mahitaji ya maji kwa kila mtu kwa mwaka kinachokubalika kimataifa ni **mita za ujazo 1,700**. Hali hiyo inaashiria kwamba, hatua madhubuti zinahitajika kuchukuliwa katika utunzaji wa vyanzo vyaa maji, kujenga miundombinu ya kuongeza upatikanaji maji na kuboresha ufanisi katika matumizi yake. Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wa Sekta ya Maji inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kukabiliana na hali hiyo ili nchi yetu isifikie kiwango hicho cha upatikanaji wa maji kwa kila Mtanzania.

## 2.2 HUDUMA YA MAJI VIJIJINI

**19. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuboresha huduma ya maji vijijini kwa kujenga miradi mipyä, kupanua, na kukarabati miundombinu ya maji. Uboreshaji huo unatekelezwa kwa kuwashirikisha wananchi katika hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kupanga, kusanifu, kujenga, kusimamia na kuendesha miradi hiyo kulingana na Sera ya Maji ya mwaka 2002. Vilevile, Wizara yangu inaendelea na jukumu lake la kutafuta fedha, kuandaa miongozo ya utekelezaji na kutoa ushauri wa kitaalam ambapo Sekretarieti za Mikoa husimamia na kutoa ushauri wa kiufundi kwa Halmashauri katika kutekeleza miradi ya maji vijijini. Jitihada hizo hufanyika kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo, Serikali za Mitaa, wananchi, Sekta Binafsi na wadau wengine.

**20. Mheshimiwa Spika**, tathmini ya utekelezaji wa *BRN* kwa sekta zote **sita** imeonesha mafanikio makubwa ambapo Sekta ya Maji imeweza kufikia malengo yaliyowekwa kwa kiwango kikubwa. Mafanikio yaliyopatikana kutokana na mpango huo ni pamoja na kuongezeka kwa idadi ya wananchi wanaopata huduma ya maji kutoka wananchi **15,200,000** sawa na **asilimia 40** mwezi Juni, 2013 hadi kufikia wananchi **20,957,855** sawa na **asilimia 55.9** mwezi Aprili 2015, likiwa ni ongezeko la wananchi **milioni 5.76** wanaishi vijijini.

**21. Mheshimiwa Spika**, naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru wadau wote hususan Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Sekretarieti za Mikoa, Halmashauri na Washirika wa Maendeleo tulioshirikiana nao katika kufikia malengo hayo. Kazi hiyo ilikuwa kubwa na yenye changamoto nyingi, hivyo nawaomba tuendelee kushirikiana katika kutekeleza miradi ya Sekta ya Maji ili kufikia azma ya Serikali ya kuwapatia wananchi huduma ya maji safi na salama.

## 2.3 HUDUMA YA MAJI MIJINI

**22. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu imeendelea kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika maeneo ya mijini kuititia Mamlaka za Maji kwenye Miji Mikuu ya Mikoa **23** pamoja na Dar es Salaam; Miji Mikuu ya Wilaya **99**, Miji Midogo **14**; na Miradi **8** ya kitaifa. Kwa sasa takribani watu **milioni 7** wanapata huduma ya maji safi na salama kwa upande wa Miji Mikuu ya Mikoa, Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo pamoja na huduma inayotolewa na miradi ya kitaifa. Vilevile, wakazi wapatao **milioni 3** kwa upande wa Jiji la Dar es Salaam na baadhi ya maeneo ya Mkoaa wa Pwani wanapata huduma hiyo.

### 2.3.1 Huduma ya Majisafi katika Miji Mikuu ya Mikoa na Jiji la Dar es Salaam

#### (a) Miji Mikuu ya Mikoa

**23. Mheshimiwa Spika**, jukumu la Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira za Miji Mikuu ya Mikoa ni kutoa huduma ya maji safi na salama pamoja na uondoaji wa majitaka katika miji hiyo. Hadi mwezi Aprili 2015, mahitaji ya maji katika Miji Mikuu ya Mikoa ni **lita milioni 619** kwa siku ikilinganishwa na uzalishaji wa **lita milioni 385** kwa

siku. Wastani wa wakazi wanaopata huduma ya maji katika miji hiyo kwa sasa ni **asilimia 86** kwa wastani wa **saa 17** kwa siku. Idadi ya wateja waliounganishwa na huduma ya maji imeongezeka kutoka **336,898** mwezi Machi, 2014 hadi wateja **362,953** mwezi Aprili, 2015. **Asilimia 96** ya wateja waliounganishwa na huduma hiyo wamefungiwa dira za maji.

**24. Mheshimiwa Spika**, wastani wa upotevu wa maji kwenye miundombinu ya usambazaji maji katika miji mikuu ya mikoa umefikia **asilimia 35** ikilinganishwa na **asilimia 38** mwezi Machi, 2014. Upotevu huo wa maji unatokana na uchakavu wa miundombinu ya usambazaji wa maji, uharibifu wa miundombinu, pamoja na wizi wa maji unaofanywa na wateja wasio waaminifu. Wizara yangu inaendelea kuchukua hatua mbalimbali kukabiliana na upotevu wa maji ikiwemo kuzifanyia marekebisho Sheria zake ili kuzipa nguvu zaidi kwa watakaobainika na wizi wa maji pamoja na vifaa na uharibifu wa miundombinu ya maji. Vilevile, katika utekelezaji wa Mpango wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa (*BRM*), upotevu wa maji umepewa kipaumbele cha kwanza katika viashiria vya kupima utendaji (*KPIs*) wa Mamlaka za Maji Mijini ili kuzihamasisha Mamlaka hizo kutambua umuhimu wa kupunguza upotevu wa maji ili kuongeza makusanyo ya maduhuli katika Mamlaka zao.

**25. Mheshimiwa Spika**, moja ya majukumu ya Bodi za Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini ni kuandaa mikakati ya ukusanyaji wa maduhuli yanayotokana na ankara za matumizi ya maji. Hadi mwezi Aprili, 2015, makusanyo ya maduhuli kwa mwezi yameongezeka na kufikia **shilingi bilioni 7.28** ikilinganishwa na **shilingi bilioni 6.36** mwezi Machi, 2014. Ongezeko hilo linatokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa maji, wateja, mabadiliko ya bei za maji, kupungua kwa upotevu wa maji na juhudzi za Mamlaka katika kukusanya madeni kutoka kwa wateja kwa kutumia teknolojia za mawasiliano. Vilevile, mapato hayo yameziwezesha Mamlaka kuboresha huduma zinazotolewa kwa wateja ikiwa ni pamoja na kukarabati miundombinu na kugharamia shughuli za uendeshaji. Aidha, kupitia mpango wa “Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa” (*BRM*), Wizara imetua viashiria vya utendaji kazi (*Key Performance Indicators*) kwa kila Mamlaka ya Maji na kukubaliana viwango na malengo ya utekelezaji yakiwemo kuongeza uzalishaji, kuongeza idadi ya wateja, kupunguza upotevu wa maji na kuongeza makusanyo ya maduhuli.

#### (b) Jiji la Dar es Salaam

**26. Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Aprili 2015, mahitaji ya maji katika Jiji la Dar es Salaam na Miji ya Kibaha na Bagamoyo ni **lita milioni 450** kwa siku ikilinganishwa na uwezo wa mitambo wa kuzalisha maji wa **lita milioni 300** kwa siku ambazo ni sawa na **asilimia 77** ya mahitaji. Wastani wa **asilimia 68** ya wakazi wa Jiji wanapata huduma ya maji kwa wastani wa **saa 8** kwa siku. Wakazi wanaobaki hupata huduma ya maji kupitia visima, magati na huduma ya magari (*water bowsers*). Aidha, idadi ya wateja waliounganishwa na huduma ya maji ni **126,405** na kati ya hao, **asilimia 97** wamefungiwa dira za maji. Makusanyo ya maduhuli kwa mwezi ni **shilingi bilioni 3.31** na kiwango cha upotevu wa maji ni **asilimia 57**. Upotevu huo unatokana na wizi wa maji, uvujaji wa mabomba, uharibifu unaotokea wakati wa ukarabati wa miundombinu

ya barabara pamoja na uchakavu wa miundombinu. Serikali inaendelea kukabiliana na changamoto hizo na kuzipatia ufumbuzi hatua kwa hatua.

### **2.3.2 Huduma ya Majisafi katika Miradi ya Kitaifa, Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo**

**27. Mheshimiwa Spika**, hadi sasa kuna Mamlaka za Maji **99** za Miji Mikuu ya Wilaya na **14** za Miji Midogo ambazo hutoa huduma ya maji katika miji hiyo. Mamlaka hizo husimamiwa na Bodi za Wakurugenzi zinazoteuliwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu na uendeshaji wa Mamlaka hizo uko chini ya Halmashauri za Miji husika. Aidha, kuna miradi **8** ya maji ya kitaifa ambayo Bodi zake huteuliwa na Waziri wa Maji akishirikiana na Sekretarieti ya Mkoa husika.

**28. Mheshimiwa Spika**, mahitaji ya maji katika Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo kwa sasa ni **lita milioni 244.2** kwa siku ikilinganishwa na uzalishaji wa **lita milioni 99.2** kwa siku. Upatikanaji wa huduma ya maji ni **asilimia 60** ya wakazi wa miji hiyo ambapo wastani wa upatikanaji wa huduma ni **saa 9** kwa siku. Idadi ya wateja waliouanganishwa na huduma hiyo ni **107,313** na kati ya wateja hao **asilimia 58** wamefungiwa dira za maji. Kwa upande wa miradi ya kitaifa mahitaji ya maji ni **lita milioni 104.6** kwa siku ikilinganishwa na uzalishaji wa **lita milioni 51.6** kwa siku. Upatikanaji wa huduma ya maji ni **asilimia 60** ya wakazi wanaohudumiwa na miradi hiyo ambapo wastani wa upatikanaji wa huduma ni **saa 9** kwa siku. Idadi ya wateja waliouanganishwa ni **16,995** na kati ya hao, **asilimia 60** wamefungiwa dira za maji.

**29. Mheshimiwa Spika**, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo hairidhishi. Hivyo, Wizara yangu kwa kushirikiana na TAMISEMI inaendelea kuwekeza katika miundombinu ya maji na kuzijengea uwezo Mamlaka hizo ili kuongeza upatikanaji wa huduma ya majisafi katika miji hiyo. Lengo ni kuongeza ufanisi na kuziwezesha Mamlaka hizo kuijendesha kibiashara na kupunguza mzigo kwa Serikali.

### **2.3.3 Uondoaji wa Majitaka Mijini**

**30.** **Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Aprili, 2015 huduma ya uondoaji majitaka katika Miji ya Arusha, Moshi, Tanga, Dodoma, Mwanza, Mbeya, Iringa, Songea, Tabora, Morogoro na Dar es Salaam imefikia **asilimia 20**. Idadi ya wateja waliounganishwa kwenye mtandao wa majitaka katika miji hiyo imeongezeka kutoka **22,976** mwezi Machi, 2014 hadi kufikia wateja **24,346** mwezi Aprili, 2015. Hali ya uondoaji wa majitaka bado ni ya kiwango cha chini kutokana na mwamko mdogo wa wananchi kuijunga kwenye mtandao wa majitaka, miundombinu chakavu ya majitaka kwa baadhi ya miji inayohudumia maeneo machache, ongezeko kubwa la watu mijini pamoja na miji mingine kutokuwa na miundombinu ya majitaka.

## **2.4 KUJENGA UWEZO WA KITAASISI**

**31.** **Mheshimiwa Spika**, katika hotuba yangu ya mwaka jana nililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara inahitaji wataalam **8,749** kwa kipindi chote cha utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (2007-2025), ili kutekeleza majukumu kwa ufanisi na kufikia malengo yaliyokusudiwa. Wizara ilwasiliana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na kwa kuanzia, kupata kibali cha kuajiri wataalam **475**. Hadi mwezi Aprili 2015, jumla ya wataalam **318** kati ya wataalam **475** wameajiriwa na kupangiwa vituo vya kazi. Kati ya wataalam hao walioajiriwa, Wahandisi ni **96** na Mafundi Sanifu ni **222**. Ongezeko hilo limeifanya Sekta ya Maji kuwa na jumla ya wataalam **1,856** wanaosimamia na kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji.

### **3.0 UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2014/2015 NA MALENGO KWA MWAKA 2015/2016**

**32.** **Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2014/2015 na malengo ya mwaka 2015/2016 kwa Sekta ya Maji umejikita katika usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji, huduma ya majisafi na usafi wa mazingira vijijini na mijini na masuala mtambuka. Taarifa ya mapitio ya utekelezaji wa bajeti na malengo ya mwaka ujao imechambuliwa kwa undani katika aya zifuatazo.

#### **3.1 RASILIMALI ZA MAJI**

**33.** **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu kupitia Bodi za Maji za Mabonde ina wajibu wa kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji nchini. Usimamizi na uendelezaji huo unahusu kuchunguza, kutathmini na kuimarisha usimamizi wa rasilimali za maji ikiwa ni pamoja na rasilimali za maji shirikishi (*transboundary water resources*). Ili kuziwezesha Bodi za Maji kutekeleza majukumu yao, Wizara inazijengea uwezo na kuziimarisha. Kazi zinazotekelawa ni pamoja na kuandaa mipango shirikishi ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji, kusanifu na kusimamia ujenzi wa miundombinu ya kipaumbele.

##### **3.1.1 Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji**

###### **(a) Mwenendo wa Rasilimali za Maji**

**34.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu ilimarishe vituo vya kupima wingi na ubora wa rasilimali za maji juu na chini ya ardhi kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa takwimu na taarifa sahihi. Kazi zilizotekelawa ni pamoja na ujenzi wa vituo **tisa** katika mabonde ya Rufiji, Ruvuma na Pwani ya Kusini pamoja na Ziwa Victoria. Aidha, jumla ya vituo **118** vimekarabatiwa katika Mabonde ya Ziwa Rukwa vituo **16**, Ziwa Nyasa **(4)**, Ziwa Victoria **(3)**, Ziwa Tanganyika **(1)**, Pangani **(69)**, Rufiji **(22)** na Wami-Ruvu vituo **vitatu**. Kwa hiyo, hadi mwezi Aprili, 2015 kuna jumla ya vituo **633** vya kupima mwenendo wa rasilimali za maji na kati ya hivyo, vituo **321** ni vya kupima mtiririko wa maji mtoni, vituo **196** vya kupima wingi wa mvua, vituo **93** vya hali ya hewa na vituo **23** vya kupima usawa wa maji kwenye maziwa na mabwawa katika mabonde ya maji nchini.

**35.** **Mheshimiwa Spika**, kati ya vituo hivyo **633**, vituo **515** vinafanya kazi vizuri na kutumika kukusanya takwimu. Lengo ni kupata takwimu sahihi za hali ya maji nchini. Taarifa zinazopatikana kutokana na uchambuzi wa takwimu zinatumika katika utafiti wa masuala mbalimbali kwa ajili ya maandalizi ya miradi ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Katika mwaka 2015/2016, vituo vypya **90** vya kuchunguza mwenendo wa rasilimali za maji vitajengwa na vingine kukarabatiwa kwenye maeneo mbalimbali. **Jedwali Na. 2** linaonesha idadi ya vituo vya kuchunguza mwenendo wa maji katika Mabonde.

###### **(b) Kuhifadhi Mazingira na Vyanzo vya Maji**

**36. Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu inatekeleza Mpango Maalum wa Miaka Mitano wa Kuhifadhi na Kutunza Vyanzo vya Maji. Mpango huo ulianza kutekelezwa kwa kuhakikisha vyanzo vilivyobainishwa vinawekewa mipaka, kutengenezwa ramani na kuandaa taratibu za fidia ili wahuksika waweze kulipwa na maeneo hayo kutangazwa katika Gazeti la Serikali. Katika kutekeleza mpango huo, vyanzo **saba** vya maji katika Bonde la Ziwa Rukwa vilitangazwa kuwa maeneo tengefu. Hadi mwezi Aprili 2015, vyanzo **31** vimewekewa mipaka tayari kwa ajili ya kutangazwa na vyanzo **28** vipo katika hatua mbalimbali za upimaji, uwekaji mipaka na kutengeneza ramani. Aidha, elimu inaendelea kutolewa kwa jamii kuhusu umuhimu wa utunzaji na uhifadhi wa vyanzo vya maji, madhara ya uharibifu wa vyanzo vya maji, na elimu ya Sheria na Kanuni mbalimbali za usimamizi wa rasilimali za maji. **Jedwali Na. 3** linaonesha vyanzo vilivyowekewa mipaka (*demarcated water sources*) na vilivyo katika hatua mbalimbali za kuwekewa mipaka.

**37. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/2016, Wizara yangu imepanga kutangaza maeneo **18** ya vyanzo vya maji kuwa maeneo tengefu. Vilevile, Wizara itaendelea kubaini maeneo zaidi ya vyanzo vya maji na kuweka mipaka kwenye maeneo yaliyoainishwa ili kuyakinga dhidi ya uharibifu wa mazingira. Lengo ni kuhakikisha usalama wa vyanzo na upatikanaji wa uhakika wa maji kwa maendeleo endelevu.

**38. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu iliendelea kuunda na kuziimarisha Jumuiya za Watumia Maji ili ziweze kusimamia rasilimali za maji katika ngazi ya watumia maji. Hadi mwezi Aprili 2015, Jumuiya **25** ziliundwa na kujengewa uwezo katika mabonde ya Ziwa Victoria, Ziwa Rukwa, Rufiji, Ruvuma na Pwani ya Kusini, Wami-Ruvu, na Pangani ili ziweze kushiriki katika kulinda, kutunza na kusimamia rasilimali za maji katika mabonde hayo. Vilevile, Wizara imetangaza maeneo **matatu** kuwa mabonde madogo ya maji (*catchments*) ili maeneo hayo yaweze kuanzisha Ofisi za Mabonde Madogo na kuunda Kamati. Maeneo hayo ni Umba-Zigi na Kikuletwa katika Bonde la Pangani na Ruaha Mkuu katika Bonde la Rufiji. Kamati ya Bonde Dogo la Ruaha Mkuu tayari imeshaundwa. Kamati hizo zitasimamia rasilimali za maji katika ngazi ya mabonde madogo na kuweza kuzisimamia Jumuiya za Watumia Maji zitakazokuwa chini yao. Katika mwaka 2015/2016, Wizara yangu imepanga kuunda Jumuiya za Watumiaji Maji **33** na Kamati za Mabonde Madogo **18** pamoja na kuzijengea uwezo Jumuiya **91**.

**39. Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza Sheria **Na. 20** ya Mazingira ya mwaka 2004 na Kanuni zake, Wizara yangu ilifanya tathmini za athari kwa mazingira na kijamii kwa mabwawa **sita** ya Itobo, Nkiniziwa, Uchama, Enguikument I, Enguikument II na Leken yaliyopo katika Bonde la Kati. Mabwawa **matano** yalipata vibali vya mazingira ili ujenzi wa mabwawa hayo uanze. Bwawa la Uchama halikupata kibali cha mazingira kwa sababu eneo la chanzo cha bwawa hilo limejengwa makazi ya watu. Hata hivyo, ujenzi wa Bwawa la Leken umeanza chini ya usimamizi wa Halmashauri ya Wilaya ya Monduli. Hadi mwezi Aprili 2015, mabwawa **manne** yaliyobaki yalikuwa yamefanyiwa usanifu upya na makabrasha ya zabuni yameandalwa kwa ajili ya kupata Mkandarasi

wa ujenzi unaotarajiwa kuanza mwaka ujao wa fedha. Aidha, rasimu za taarifa ya tathmini za athari kwa mazingira na jamii kwa ajili ya miradi ya mabwawa ya Farkwa na Ndembera na barabara inayoelekea eneo litakapoengwa Bwawa la Kidunda zimewasilishwa *NEMC* kwa hatua zaidi. Katika mwaka 2015/2016, Wizara yangu imepanga kukarabati mabwawa **manane** ya ukubwa wa kati katika maeneo kame nchini.

**(c) Kudhibiti Uchafuzi wa Vyanzo vya Maji**

**40. Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza jukumu la kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji, jumla ya sampuli **381** za maji zilichukuliwa na kupimwa kwenye maabara katika mabonde ya Wami-Ruvu, Ziwa Nyasa, Ziwa Victoria na Rufiji. Vilevile, jumla ya viwanda **40** vilikaguliwa ili kuangalia utekelezaji wa Sheria na Kanuni zinazosimamia mazingira na rasilimali za maji katika mabonde ya Pangani na Wami-Ruvu. Ukaguzi huo ulibaini kuwa mifumo ya kusafisha majitaka katika baadhi ya viwanda haifanyi kazi vizuri na viwanda vingine vinatiririsha majitaka bila kuyatibu na kusababisha uchafuzi wa vyanzo vya maji.

**41. Mheshimiwa Spika**, hatua stahiki zimechukuliwa kwa viwanda vyenye mifumo mibovu ya majitaka na kutakiwa kuikarabati na kwa viwanda visivyo na mifumo hiyo kuhakikisha vinajenga. Vilevile, viwanda hivyo vimeagizwa kutathmini athari za kimazingira na kijamii ili kuwa na mipango mikakati ya utunzaji wa vyanzo hivyo. Aidha, katika kuimarisha udhibiti wa uchafuzi wa vyanzo vya maji, maeneo **210** yanayoweza kuleta uchafuzi katika vyanzo vya maji (*pollution hotspots*) yalitambuliwa katika mabonde ya Ruvuma na Pwani ya Kusini, Wami-Ruvu, Ziwa Nyasa na Pangani na hatua mbalimbali kuchukuliwa. Katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kuhakikisha uchafuzi wa vyanzo vya maji unadhibitiwa na Sheria na Kanuni zinafuatwa ili kulinda vyanzo hivyo.

**(d) Kutafuta Vyanzo Vipya vya Maji**

**42. Mheshimiwa Spika**, katika juhudi za Wizara yangu za kuongeza upatikanaji wa maji, vyanzo mbalimbali vya maji viliendelea kuainishwa, kufanyiwa tathmini na usanifu kwa ajili ya kuhifadhiwa na kutunzwa. Katika mwaka 2014/2015, jumla ya vyanzo vya maji **114** vilitambuliwa kwenye mabonde ya Ziwa Rukwa vyanzo **94**, Ziwa Nyasa (**17**), Rufiji (**1**), Wami-Ruvu (**1**) na Ziwa Tanganyika (**1**) kwa ajili ya kuvihifadhi na kuvilinda. Aidha, maeneo **413** yalifanyiwa utafiti wa maji chini ya ardhi ili kubaini maeneo yanayofaa kwa ajili ya uchimbaji wa visima. Kwa mwaka 2015/2016, Serikali itaendelea kutafiti maji chini ya ardhi katika maeneo mengine zaidi. Vilevile, kazi za upembuzi yakinifu, uchunguzi wa kina wa miamba, usanifu na utayarishaji wa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa ya Farkwa na Ndembera zitaendelea. Katika mwaka 2015/2016, Wizara imepanga kuchimba visima **20** na kukarabati visima 30 vya kuchunguza mwenendo wa maji chini ya ardhi, pamoja na kuendelea na taratibu za kutafuta fedha ili kuajiri Wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa vyanzo vipya vya maji.

**43. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Wizara yangu imeendelea kutafuta vyanzo vya maji katika maeneo mbalimbali nchini kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China na Serikali ya Misri. Katika mwaka 2014/2015, Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya China imekamilisha uchimbaji wa visima **55** katika Wilaya za Kisarawe visima **30** na Kilosa visima **25** Vilevile, utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi wa uchimbaji wa visima **30** kwa kushirikiana na Serikali ya Misri unaendelea. Hadi mwezi Aprili 2015, uchimbaji wa visima **11** katika Wilaya za Mwanga kisima **kimoja**, Same **(8)** na Kiteto **(2)** umekamilika na uchimbaji wa visima vingine **8** Wilayani Kiteto unaendelea. Katika mwaka 2015/2016, visima **11** vilivyobaki vitachimbwa katika Wilaya za Bariadi visima **(2)** na Itilima **(9)**.

**44. Mheshimiwa Spika**, Wizara inahakikisha kuwa taratibu za kitaalam za utafiti wa maji chini ya ardhi na uchimbaji wa visima unafanywa kwa umakini ili visima vinavyochimbwa viwe na ubora unaostahili kwa matumizi endelevu. Hadi mwezi Aprili 2015, Wizara yangu ilitoa leseni **saba** kwa kampuni za uchimbaji visima vya maji na leseni **moja** kwa kampuni ya utafiti wa maji chini ya ardhi. Leseni hizo zimeanza kutolewa upya kuanzia mwezi Julai 2014 kutokana na kuanza kutumika kwa Kanuni za utafiti wa maji chini ya ardhi na uchimbaji wa visima ambazo zilifuta vibali vyote vilivyotolewa awali. Kulingana na hali hiyo, nazihimiza kampuni zote kuomba upya leseni ili wafanye kazi zao kwa mujibu wa Sheria. Aidha, hadi mwezi Machi 2015, jumla ya visima vya maji **570** vilichimbwa na kusajiliwa katika maeneo mbalimbali nchini. Kati ya hivyo, visima **233** vilichimbwa na Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa (*DDCA*) na visima **337** vilichimbwa na kampuni binafsi. Katika mwaka 2015/2016, Serikali itaendelea kusimamia watafiti na wachimbaji visima wote ili kupata takwimu za uchimbaji wa visima nchini. Kwa kuwa uzoefu umeonesha maji chini ya ardhi yanaweza kuwa na kemikali ambazo ni sumu kwa binadamu, lazima maji yatokanayo na uchimbaji wa visima yapimwe kwanza kabla ya kutumiwa.

**45. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Uingereza kupitia Idara yake ya Maendeleo ya Kimataifa (*DFID*), inatekeleza Mradi wa Kufanikisha Uhakika wa Maji (*Achieving Water Security*) kwenye eneo la Uendelezaji Kilimo Ukanda wa Kusini Tanzania - *Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania (SAGCOT)*. Mradi huo utakaogharimu kiasi cha **Paundi za Uingereza milioni 5**, unasimamiwa na Bodi ya Maji ya Bonde la Rufiji na umepangwa kutekelezwa kwa miaka mitatu kuanzia mwezi Machi 2013 hadi Machi, 2016. Aidha, mradi huo utaimarisha shughuli za usimamizi wa rasilimali za maji kwa ajili ya kukusanya takwimu zitakazowezesha kufanya maamuzi ya kutumia rasilimali hiyo kwenye eneo la SAGCOT. Vilevile, mradi utaunda Jumuiya za Watumiaji Maji na kutoa mafunzo mbalimbali kuhusu usimamizi na utunzaji wa rasilimali za maji.

**(e) Matumizi Bora ya Rasilimali za Maji**

**46. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Bodi za Maji za Mabonde ina wajibu wa kusimamia matumizi bora ya maji kwa kutoa vibali vya kutumia maji na kutiririsha majitaka kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizopo. Hadi mwezi Aprili 2015, jumla ya vibali vypa **421** vya kutumia maji vilitolewa katika mabonde ya Ruvuma na Pwani ya Kusini **(15)**, Pangani **(34)**, Rufiji **(191)**, Wami-Ruvu **(44)**, Ziwa Victoria **(13)**,

Ziwa Rukwa (51) na Ziwa Tanganyika (73). Aidha, jumla ya vibali **10** vya kutiririsha majitaka vilitolewa katika mabonde ya maji ya Wami-Ruvu (3), Ziwa Victoria (6) na Pangani (1). Vilevile, zoezi la kuwatambua watumiaji maji kwa matumizi mbalimbali lilifanyika. Katika zoezi hilo, jumla ya watumiaji maji **67** walitambuliwa na kubainika kuwa hawana vibali katika mabonde ya Ziwa Victoria, Ziwa Rukwa, Ziwa Nyasa na Bonde la Kati. Elimu kuhusu taratibu za kisheria za matumizi endelevu ya maji ilitolewa kwa wahusika wasio na vibali na kuagizwa kuomba vibali vya kutumia maji hayo. Katika mwaka 2015/2016, Wizara yangu imepanga kutoa vibali **600** vya watumiaji maji katika vyanzo mbalimbali vya maji nchini.

**(f) Mipango Shirikishi ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji**

**47. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu iliendelea na uandaaji wa Mipango Shirikishi ya Kusimamia na Kuendeleza Rasilimali za Maji (*Integrated Water Resources Management and Development Plans – IWRM&D*) katika mabonde yote tisa nchini. Hadi mwezi Aprili 2015, mipango hiyo katika mabonde ya Ruvuma na Pwani ya Kusini, na Bonde la Kati imekamilika. Utayarishaji wa Mipango Shirikishi katika mabonde ya Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa, Ziwa Rukwa na Rufiji unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2015. Katika mwaka 2015/2016, Mtaalam Mshauri anayeandaa Mpango Shirikishi katika Bonde la Wami-Ruvu anatarajiwa kuanza kazi mwezi Julai, 2015 na kukamilisha mwezi Desemba, 2015. Mpango huo utatayarishwa kwa kutumia Tathmini ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji iliyofanywa na JICA katika Bonde hilo.

**(g) Kuimarisha Bodi za Maji za Mabonde**

**48. Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha hali ya utendaji kazi wa Bodi za Maji za Mabonde, Wizara yangu imeendelea kuzijengea uwezo Bodi hizo kwa kutoa mafunzo kwa watumishi, kujenga ofisi, kununua vitendea kazi na kufanya tafiti mbalimbali. Lengo ni kuhakikisha kuwa Bodi hizo zinaongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yake ya kusimamia, kutunza, kuhifadhi na kuendeleza rasilimali za maji nchini.

**49. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, watumishi **203** wa mabonde yote **tisa** walipatiwa mafunzo ya muda mfupi na semina mbalimbali kama ifuatavyo; Bonde la Pangani watumishi **12**, Rufiji (52), Ruvuma na Pwani ya Kusini (21), Ziwa Victoria (21), Bonde la Kati (28), Ziwa Tanganyika (10), Ziwa Nyasa (15), Ziwa Rukwa (25) na watumishi **19** kutoka Bonde la Wami-Ruvu. Mafunzo hayo yalihusu usimamizi wa mikataba ya kimataifa katika rasilimali za maji; ukaguzi wa mazingira; usalama wa mabwawa; uhasibu; ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (*Public Private Partnership-PPP*); na mifumo ya kielektroniki kuhusu utunzaji na uhifadhi wa rasilimali za maji.

**50. Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Aprili 2015, ujenzi wa Ofisi za Bodi za Maji za Mabonde uliendelea na umefikia katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Katika Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Victoria ujenzi umefikia **asilimia 90**, Ziwa Tanganyika **asilimia 60**, Bonde la Kati **asilimia 60** na ujenzi wa Ofisi ya Bonde Dogo la Kilombero iliyopo

Ifakara katika Bonde la Rufiji umekamilika. Ujenzi wa Ofisi hizo unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2015 kwa Bonde la Ziwa Victoria na mwezi Septemba 2015 katika mabonde ya Ziwa Tanganyika na Bonde la Kati. Kwa mabonde ya Wami – Ruvu na Pangani, usanifu wa kina wa ujenzi wa ofisi za mabonde hayo unaendelea. Mchakato wa kuwapata Wakandarasi wa ujenzi wa ofisi unaendelea katika Mabonde **manne** ambayo ni Bonde la Ziwa Nyasa kwenye miji ya Songea na Njombe; Bonde la Ruvuma na Pwani ya Kusini (Mtwara, Lindi, Tunduru na ofisi ya watumia maji-Likonde); Bonde la Rufiji (Iringa, na ofisi za Watumia maji Kimani na Mkoji); na katika Bonde la Ziwa Rukwa (Mbeya na Sumbawanga). Katika mwaka 2015/2016, Wizara yangu itaa jiri wakandarasi na kuanza ujenzi wa ofisi hizo.

**51. Mheshimiwa Spika**, vilevile, Wizara yangu imeendelea kuzijengea uwezo Bodi za Maji za Mabonde katika kufanya utafiti mbalimbali katika rasilimali za maji nchini. Katika mwaka 2014/2015, utafiti umefanya katika mabonde ya Wami-Ruvu, Ziwa Rukwa na Bonde la Kati. Utafiti huo unahu su upotevu wa maji katika Mto Ruvu kwenye eneo kati ya Kidunda na Ruvu Darajani; pamoja na utafiti kuhusu uwiano wa maji (*water balance*) katika maziwa ya Rukwa na Manyara. Katika mwaka 2015/2016, utafiti huo unatarajiwa kukamilika na kuanza utafiti mwengine utakaohusu kiwango cha kuja kwa mchanga/udongo na usafirishaji wake (*Sediment yield and transport modeling*) kwenye Mto Mbwemkuru katika Bonde la Ruvuma na Pwani ya Kusini.

**(h) Ukusanyaji wa Maduhuli**

**52. Mheshimiwa Spika**, jukumu mojawapo la Bodi za Maji za Mabonde ni kuweka malengo, kuanda na kutekeleza mikakati ya ukusanyaji wa maduhuli yanayotokana na ada za matumizi ya maji. Mapato hayo hutumika katika usimamizi, utunzaji na uendelezaji wa rasilimali za maji nchini. Hadi mwezi Aprili 2015, jumla ya **shilingi bilioni 2.15** zilikusanya sawa na **asilimia 84** ya lengo la **shilingi bilioni 2.6** zilizopangwa kukusanya katika mwaka 2014/2015. Katika mwaka 2015/2016, Bodi za Maji za Mabonde zimelenga kukusanya kiasi cha **shilingi bilioni 3.02** kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato. **Jedwali Na. 4** linaonesha makusanyo ya maduhuli mwaka 2014/2015 na makadirio ya makusanyo kutoka Bodi za Maji za Mabonde kwa mwaka 2015/2016.

**(i) Udhibiti wa Migogoro katika Matumizi ya Maji**

**53. Mheshimiwa Spika**, ni jukumu la Bodi za Maji za Mabonde kuhakikisha kuwa rasilimali za maji zinatumika katika uwiano sahihi kwa watumiaji kufuatana na sheria, taratibu na kanuni zilizopo. Migogoro inayojitokeza katika matumizi ya maji husuluhishwa na Bodi za Maji za Mabonde kwa kushirikiana na Jumuia za Watumiaji Maji. Usuluhishi unaposhindikana katika ngazi hiyo, vyombo vya kisheria hutumika kutatua migogoro hiyo. Katika mwaka 2014/2015, migogoro **17** ya watumiaji maji ilijitokeza na kutatuliwa kwenye Mabonde ya Maji ya Pangani, Wami-Ruvu, Bonde la Kati na Rufiji. Katika mwaka 2015/2016, Serikali itaendelea kutoa elimu ya ugawaji na utunzaji wa rasilimali za maji ili kupunguza migogoro baina ya watumiaji maji.

## (j) Usimamizi wa Rasilimali za Maji Shirikishi

54. **Mheshimiwa Spika**, nchi yetu ina jumla ya mabonde **tisa** na kati ya hayo, mabonde **saba** yanavuka mipaka ya nchi yetu na hivyo kuwa na ulazima wa kushirikiana na nchi nyingine **17** kwa kuunda vyombo vya pamoja vya kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali za maji. Nchi hizo ni Angola, Botswana, Burundi, Ethiopia, Eritrea, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Kenya, Malawi, Misri, Msumbiji, Namibia, Rwanda, Sudan, Sudani Kusini, Uganda, Zambia na Zimbabwe. Ushirikiano wa kitaasisi na nchi hizo umeendelea kutekelezwa kama ifuatavyo:-

### (i) Bonde la Mto Nile

55. **Mheshimiwa Spika**, Umoja wa Ushirikiano wa Nchi za Bonde la Mto Nile (*Nile Basin Initiative - NBI*) unaundwa na jumla ya nchi **11** ambazo ni Burundi, Ethiopia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Kenya, Misri, Rwanda, Sudan, Sudani Kusini, Uganda na Tanzania. Katika umoja huo nchi ya Eritrea ni mtazamaji (*observer*). Umoja huo ni chombo cha mpito kuelekea kwenye uundwaji wa Kamisheni ya Bonde la Mto Nile. Madhumuni ya kuanzishwa kwa umoja huo ni kusimamia matumizi ya maji yenye uwiano na haki baina ya nchi wanachama, kusimamia utekelezaji wa miradi ya kuhifadhi Bonde la Mto Nile, mazingira, nishati, kilimo, mafunzo na kujenga uwezo kwa taasisi zilizopo katika nchi husika.

56. **Mheshimiwa Spika**, katika kufikia malengo hayo nchi shiriki **sita** za Burundi, Ethiopia, Rwanda, Uganda, Kenya, na Tanzania zilisaini Mkataba wa Msingi wa Ushirikiano (*CFA*) katika Bonde la Mto Nile na hivyo kukidhi matakwa ya kuingia hatua ya kuridhia (*ratification*) mkataba huo. Ninapenda kuchukua fursa hii kulishukuru Bunge lako Tukufu kwa kupitia na kujadili mkataba huo ambao uliwasilishwa katika Bunge la **19** na hatimaye kuridhiwa tarehe 26/03/2015. Tanzania imekuwa nchi ya **tatu** kuridhia baada ya nchi za Ethiopia na Rwanda. Kamisheni ya Bonde la Mto Nile itaundwa pindi nchi **sita** zitakaporidhia mkataba huo. Katika mwaka 2015/2016, Tanzania itaendelea kuzishawishi nchi za Burundi, Uganda, Sudani Kusini, Kenya na Sudan zirimdhie ili Kamisheni iundwe.

### (ii) Kuhifadhi Mazingira ya Ziwa Victoria

57. **Mheshimiwa Spika**, madhumuni ya utekelezaji wa Mradi wa Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria (*Lake Victoria Environmental Management Project - LVEMP*) ni kuimarisha usimamizi wa pamoja wa rasilimali za Bonde la Ziwa Victoria kwa kudhibiti uharibifu wa mazingira katika ziwa hilo. Nchi shiriki katika usimamizi wa bonde hilo ni Kenya, Rwanda, Burundi, Uganda na Tanzania. Kwa upande wa Tanzania, mradi huo umeimarisha taasisi zinazohusika na hifadhi ya maji na samaki; kukarabati mifumo ya kusafisha majitaka katika miji ya Mwanza, Musoma na Bukoba; pamoja na miradi midogo ya kijamii katika Halmashauri za Wilaya zinazozunguka ziwa hilo. Halmashauri hizo ambazo zimeingizwa kwenye Awamu ya Pili ya utekelezaji wa mradi huo ni Maswa, Itilima, Busega, Bariadi, Magu, Meatu, Kwimba, Sengerema, Geita, Chato, Muleba, Karagwe, Kyerwa na Misenyi.

**58. Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Aprili, 2015 katika kutekeleza Awamu ya Pili ya mradi huo, miradi midogo **341** ya kijamii (*Co – Development Driven Interventions*) yenye thamani ya **Dola za Marekani milioni 8.3** imefikia hatua mbalimbali za utekelezaji na kati ya miradi hiyo, **116** imekamilika na ipo tayari kukabidhiwa kwa jamii. Aidha, miradi mingine **24** ya kijamii yenye thamani ya **Dola za Marekani milioni 5.7** inatekelezwa katika Wilaya za Musoma Mjini, Bukoba Mjini, Maswa, Bariadi, Itilima, Meatu, Ksimba, Magu, Ukerewe, Misenyi, Misungwi, Illemela na Nyamagana. Miradi hiyo **24** inajumuisha uhifadhi wa maeneo ya **mota 60** kutoka kwenye kingo za Mto Simiyu na Mto Duma katika Halmashauri za Wilaya za Busega, Magu, Ksimba, Bariadi, Meatu na Maswa pamoja na uendelezaji wa teknolojia ya majiko sanifu na banifu katika Wilaya ya Maswa. Miradi iliyotajwa katika Halmashauri hizo **sita** imekamilika.

**59. Mheshimiwa Spika**, miradi **minne** inayohusisha miundombinu ya usafishaji majitaka yenye thamani ya **Dola za Marekani milioni 3.5** imeanza kutekelezwa. Mradi wa kusafisha na kutupa majitaka (*Sludge Disposal Facility*) katika Manispaa ya Bukoba umekamilika. Miradi mingine inayoendelea ni ya uunganishaji wa mfumo wa majitaka ya majumbani kwenye mtandao mkuu wa majitaka Jijini Mwanza; mradi wa ujenzi wa mabwawa ya majitaka katika eneo la Bweri, Manispaa ya Musoma; na ukarabati wa mfumo wa kusafisha majitaka katika machinjo ya Jiji la Mwanza. Katika mwaka 2015/2016, Wizara yangu itaendelea kukamilisha miradi iliyobaki na kuikabidhi kwa jamii.

### (iii) Bonde la Mto Mara

**60. Mheshimiwa Spika**, Bonde la Mto Mara ni eneo muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi pamoja na bayoanuai zilizopo. Bonde hilo linahusisha nchi mbili za Kenya na Tanzania na miradi mbalimbali ya pamoja inatekelezwa chini ya uratibu wa Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria (*Lake Victoria Basin Commission - LVBC*). Katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu iliendelea kushiriki katika utekelezaji wa Mradi wa Masuala ya Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (*Planning for Resilience in East Africa through Policy, Adaptation, Research and Economic Development-PREPARED*). Vilevile, Hati ya Makubaliano (*MoU*) kwa ajili ya usimamizi shirikishi wa rasilimali za maji katika Bonde la Mto Mara chini ya uratibu wa *Lake Victoria Basin Commission* ipo katika hatua za mwisho kukamilika. Aidha, utekelezaji wa mradi wa Bwawa la Borenga litakalotumika kwa shughuli za binadamu; mifugo; uzalishaji wa nishati ya umeme; na kilimo cha umwagiliaji katika vijiji **16** kwenye Wilaya za Butiama, Serengeti na Tarime unaendelea. Hadi sasa, upembusi yakinifu na usanifu wa bwawa hilo umekamilika na taratibu za kupata fedha na kuajiri Mkandarasi wa ujenzi zimeanza. Mradi huo pamoja na mingine unaratibiwa na *Nile Equatorial Lakes Subsidiary Action Plan (NELSAP)* chini ya *Nile Basin Initiative, NBI*.

**61. Mheshimiwa Spika**, chini ya uratibu wa *NELSAP* maandalizi ya Mipango ya Usimamizi wa Hifadhi ya Maji katika sehemu ya Bonde la Mto Mara (*Sub-Catchment Management Plans*) kwenye maeneo ya Tobora (**kilomita za mraba 364**) na Somonche (**kilomita za mraba 682**); pamoja na uainishaji na upimaji wa maeneo ya

mfano unaendelea. Vilevile, mikutano na wananchi kwa kuzingatia jinsia ili kupata maoni mbalimbali kuhusu utunzaji wa mabonde madogo katika maeneo hayo ilifanyika. Aidha, Serikali za Tanzania, Kenya pamoja na *NELSAP* zitasaini Hati ya Makubaliano ya kutekeleza miradi iliyopangwa.

#### (iv) Bonde la Mto Songwe

**62. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Malawi inatekeleza Awamu ya Pili ya Programu ya Kuendeleza Bonde la Mto Songwe. Awamu hiyo inahusu kazi za usanifu wa kina wa miundombinu ya rasilimali za maji na maandalizi ya uwekezaji. Miundombinu hiyo ni kwa ajili ya kuzuia mafuriko, kuzalisha umeme, kilimo cha umwagiliaji, matumizi ya maji majumbani, ufugaji samaki na uwekezaji katika Sekta ya Utalii. Vilevile, umeme utakaozalishwa utaunganishwa kwenye gridi ya Taifa ya nchi za Malawi na Tanzania na kusambazwa kwenye vijiji vilivyo ndani ya eneo la Bonde. Aidha, chini ya awamu hiyo, maandalizi ya awali ya kuanzisha Kamisheni ya Pamoja ya Kusimamia Programu na kujenga uwezo kwa watekelezaji wa programu katika ngazi za Halmashauri hadi Taifa yako tayari.

**63. Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Aprili 2015, kazi zilizotekeliza ni pamoja na kukamilisha Dira ya Maendeleo ya Bonde la Mto Songwe inayolenga mwaka 2050; mapitio ya upembuzi yakinifu wa mwaka 2003; na Tathmini ya Kimkakati ya Athari za Kimazingira na Kijamii (*SESA-Strategic Environmental and Social Impact Assessment*). Aidha, rasimu ya mwisho ya Mfumo wa Kitaasisi (*Convention on establishment of Songwe River Commission*) kwa ajili ya kuanzisha Kamisheni ya Pamoja ya kusimamia Programu ya kuendeleza Bonde la Mto Songwe imekamilika na itawasilishwa Bungeni kwa kufuata taratibu zilizopo kwa ajili ya kuridhiwa. Vilevile, Mtaalam Mshauri amewasilisha rasimu za Programu ya miaka **10** ya Kuendeleza Bonde la Mto Songwe; Mpango Biashara wa Kamisheni ya Kuendeleza Bonde la Mto Songwe (*Songwe River Basin Commission Business Plan*); Tathmini ya Athari za Kimazingira na Kijamii; na rasimu ya Mpango Kazi wa Kuwahamisha na Kuwalipa Fidia waathirika wa mradi (*Resettlement Action Plan*). Rasimu hizo zimepitwa na kutolewa maoni na wadau kwa ajili ya maboresho.

**64. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea na usanifu wa kina kwa miradi ya kipaumbele katika uwekezaji ambayo ni Bwawa la Songwe Chini (*Lower Songwe dam*) linaloambatana na miundombinu ya kuzalisha umeme megawati **180.2**; skimu **mbili** za kilimo cha umwagiliaji zenyenye jumla ya hekta **6,200** (hekta **3,050** upande wa Malawi na hekta **3,150** nchini Tanzania); miundombinu ya usafirishaji umeme; na maandalizi ya nyaraka za zabuni kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu hiyo. Pamoja na mafanikio hayo, kazi ya usanifu wa miundombinu kwa ajili ya kudhibitiwa mkondo wa Mto Songwe; na usanifu wa miradi ya maji ya kunywa kwa ajili ya miji midogo ya Songwe nchini Malawi na Kasumulu kwa upande wa Tanzania zinaendelea. Kazi hizo zinatarajija kukamilika mwezi Juni, 2015.

**65. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/2016, Serikali itakamilisha taratibu za kuridhia Azimio la kuanzisha Kamisheni ya Pamoja ya Kusimamia Bonde la Mto Songwe. Vilevile, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Malawi itaendelea kutafuta

wafadhili mbalimbali ili kutekeleza Awamu ya tatu ya mradi huo na kuunda Sekretarieti ya mpito ya Kamisheni kwa ajili ya kuanza kusimamia utekelezaji wa miradi ya awali. Miradi hiyo inahusu mradi wa maji ya kunywa kwa vijiji vilivyopo kwenye Bonde la Mto Songwe ambao unalenga kuwapatia huduma ya maji safi na salama wastani wa **asilimia 22.5** ya wakazi wa bonde hilo kwa upande wa Malawi na **asilimia 18.7** kwa upande wa Tanzania. Mradi huo unakadiriwa kugharimu **Dola za Marekani milioni 1.5.** Mradi mwagine ni wa kuandaa mfumo wa kuratibu haidrolojia katika bonde (*Hydrological Monitoring System*) ambao unakadiriwa kugharimu **Dola za Marekani 425,000.**

## (v) Ziwa Tanganyika

**66. Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imeendelea na usimamizi wa pamoja na uendelezaji wa rasilimali za maji ya Ziwa Tanganyika kwa kushirikiana na nchi za Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na Zambia. Ziwa Tanganyika linaendelea kukumbwa na changamoto ya kupungua kwa kina cha maji kama inavyojidhihirisha katika bandari za Kigoma upande wa Tanzania; na Kalemie, Uvira na Moba kwa upande wa DRC hivyo, kuathiri matumizi ya bandari hizo. Mionganoni mwa sababu zinazochangia tatizo la kupungua kwa kina cha maji ni kubomoka kwa banio la Mto Lukuga uliopo DRC unaotoa maji kutoka Ziwa Tanganyika kupeleka Mto Kongo.

**67. Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na changamoto hizo na kwa kuwa waathirika wakuu ni Tanzania na DRC, nchi ambazo zinamiliki kwa pamoja **asilimia 86** ya Ziwa hilo, Marais wa Serikali zote mbili walitoa maelekezo kwa Mawaziri wa Maji wa Tanzania na DRC kukutana ili kujadili na kupata ufumbuzi wa changamoto husika. Mkutano wa kwanza wa Mawaziri ulifanyika tarehe 16/04/2014, Mjini Dodoma ambapo tulikubaliana kushirikiana katika maeneo yanayohusu usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji za Bonde la Ziwa Tanganyika.

**68. Mheshimiwa Spika**, kabla ya kuanza utekelezaji wa makubaliano hayo, ililazimu masuala muhimu yafanyike ili kuweka msingi wa utekelezaji, ambapo kila nchi ilitakiwa kuteua wataalam watakaouna kamati ya pamoja ya kushughulikia mradi wa ujenzi wa banio la Mto Lukuga pamoja na masuala ya usimamizi wa rasilimali za maji. Aidha, ilikubalika kwamba mkutano wa pili ufanyike Kalemie DRC ambapo Mawaziri wangezindua Kamati hiyo ya pamoja. Mkutano huo ulifanyika tarehe 16-17 Agosti, 2014 na ulimalizika kwa kutoa azimio la pamoja (*Ministerial Declaration*) lenye makubaliano ya msingi yafuatayo:-

- (i) Kuendeleza ushirikiano wa dhati wa kikanda na kati ya nchi zetu mbili kwa kuzingatia yaliyomo kwenye mkataba wa kuanzisha Mamlaka ya Ziwa Tanganyika;
- (ii) Kuimarisha na kuendeleza jitihada na mikakati ya pamoja ya kushughulikia kwa ujumla wake, tatizo la kupungua kwa kina cha maji ya Ziwa Tanganyika; na
- (iii) Kuandaa Hati ya Makubaliano (*MoU*) kati ya nchi zetu mbili kwa kuzingatia maeneo ya ushirikiano tuliyokubaliana wakati wa mikutano ya Mawaziri iliyofanyika Dodoma na Kalemie.

**69. Mheshimiwa Spika**, kamati ya pamoja ya wataalam ilifanya kikao chake cha pili Jijini Dar es Salaam tarehe 16-18 Februari, 2015 kwa lengo la kukamilisha rasimu ya pamoja ya Hati ya Makubaliano (*MoU*) ya ushirikiano wa pamoja wa usimamizi wa rasilimali za maji ya Bonde la Ziwa Tanganyika na ujenzi wa banio kwenye Mto Lukuga. Kila nchi iliwasilisha rasimu hiyo kwa mamlaka husika kupata maoni kwa ajili ya kuboresha kabla ya kusainiwa. Baada ya taratibu zote za kisheria katika kila nchi kukamilika, hati hiyo ilisainiwa tarehe 07/05/2015, Jijini Kinshasa-DRC. Katika mwaka

2015/2016, Serikali ya Tanzania itaendelea kutekeleza shughuli zilizoainishwa kwenye *MoU* na pia kushirikiana kwa karibu na nchi za Burundi, Zambia na Sekretarieti ya Mamlaka ya Ziwa Tanganyika.

### **3.1.2 Ubora na Usafi wa Maji**

**70. Mheshimiwa Spika**, Sera ya Maji (2002), Sheria za Usimamizi wa Rasilimali za Maji **Na. 11** na Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira **Na.12** za mwaka 2009, zinaelekeza mamlaka zote za kiutawala na kiutendaji nchini kuhakikisha maji yanayotumiwa na wananchi kwa shughuli za kiuchumi na kijamii yanafikia viwango vya ubora unaokubalika kitaifa na kimataifa. Maji safi na salama ni msingi muhimu katika kulinda afya za wananchi dhidi ya magonjwa yatokanayo na maji. Katika kutekeleza matakwa ya Sera kuhusiana na vyanzo na ubora wa maji, Wizara yangu kuitopia mtandao wa Maabara za Ubora wa Maji za Kanda na Mikoa iliendelea kuhakiki ubora wa maji katika vyanzo na mitandao ya kusambaza maji.

**71. Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Aprili 2015, jumla ya sampuli **4,442** zilikusanywa na kufanyiwa uchunguzi wa kimaabara wa kemikali na makrobaolojia kati ya sampuli za maji **8,000** zilizopangwa kuchunguzwa kwa mwaka 2014/2015. Hali ya ubora wa maji kwa matumizi mbalimbali ni kama ifuatavyo:-

#### **(a) Ubora wa Maji kwa Matumizi ya Majumbani**

**72. Mheshimiwa Spika**, Wizara ilihakiki hali ya ubora wa maji katika vyanzo kwenye Halmashauri, mitandao ya maji mijini, taasisi na vyanzo vya maji vya watu binafsi ambapo jumla ya sampuli **3,882** zilichunguzwa. Matokeo ya uchunguzi yalionesha sampuli **3,175** sawa na **asilimia 82** zilikuwa na viwango vinavyokubalika kitaifa. Sampuli **707** hazikukidhi viwango kutokana na kuwa na kiwango kikubwa cha chumvi pamoja na vimelea vya wadudu hususan, kwenye visima vifupi na maji juu ya ardhi. Aidha, maji ya visima hivyo yalitibiwa kwa kuwekewa dawa ya kuua vimelea na visima vinaendelea kutumika.

#### **(b) Ubora wa Maji kwa Matumizi ya Viwanda**

**73. Mheshimiwa Spika**, katika kufuutilia hali ya ubora wa maji yanayotumiwa viwandani, jumla ya sampuli **364** kutoka viwanda vya samaki vya Kagera, Mwanza, Mara, Dar es Salaam na kiwanda cha sukari cha Kagera zilichunguzwa. Matokeo ya uchunguzi huo yalibainisha kuwa maji yanayotumiwa na viwanda hivyo yanakidhi viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa. Wizara itaendelea kuchukua tahadhari ya kuhakikisha kuwa maji yanayotumika katika viwanda vya usindikaji vyakula yanakidhi viwango vya ubora wa maji unaokubalika ili kulinda afya ya mlaji.

#### **(c) Mwenendo wa Ubora wa Maji katika Vyanzo**

**74. Mheshimiwa Spika**, usafi na usalama wa maji hutegemea hali ya mazingira yanayozunguka vyanzo. Katika kudhibiti vyanzo visichafuliwe inabidi kufuutilia mwenendo wa ubora wa maji katika vyanzo. Hadi mwezi Aprili 2015, jumla ya sampuli za maji **322** kutoka katika vyanzo mbalimbali zilichunguzwa na matokeo yalionesha kuwa maji katika vyanzo hivyo yana ubora unaokubalika kwa matumizi ya kijamii na kiuchumi pamoja na ustawi wa mfumo wa ikolojia.

#### **(d) Ubora wa Maji kwa ajili ya Ujenzi na Utafiti**

**75. Mheshimiwa Spika**, usalama na uimara wa miundombinu ya Sekta ya Ujenzi ikiwemo barabara na majengo unategemea kiwango cha kemikali kwenye maji yanayotumika. Kwa kuzingatia hilo, jumla ya sampuli **22** za maji kwa ajili ya matumizi ya ujenzi kutoka kwa Wakandarasi mbalimbali wa majengo na barabara zilichunguzwa ubora wake. Uchunguzi huo ulibaini kuwa baadhi ya sampuli hizo zina kiwango kikubwa cha madini ya *sulphate* yanayoweza kuathiri muunganiko wa saruji, kokoto na mchanga na hivyo, kudhoofisha uimara wa barabara na majengo. Ushauri wa kitaalam kuhusu uchanganyaji wa maji (*blending*) ili kupata kiwango sahihi cha madini kwenye maji yanayotumika kwenye ujenzi ultolewa kwa Wakandarasi hao.

**76. Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu kwa kushirikiana na Chuo cha Utafiti wa Uvuvi (*Tanzania Fisheries Research Institute-TAFIRI*) ilifuatilia mwenendo wa ubora wa maji katika Rasi ya Nyegezi kwenye Ziwa Victoria ambapo sampuli za maji **13** zilichunguzwa. Matokeo ya uchunguzi yalibaini kuendelea kuongezeka kwa kiwango cha madini ya *phosphorus* na *nitrate*. Ongezeko hilo linasababisha kuwepo kwa mwani (*algae*) ambao unaathiri mazalia ya samaki. Hivyo, Wizara yangu inaendelea kushirikiana na taasisi na watu binafsi katika kulinda na kuhifadhi mazingira ya Ziwa Victoria.

#### **(e) Ubora wa Majitaka**

**77. Mheshimiwa Spika**, kama nilivyoeleza hapo awali, vyanzo vya maji vinaweza kuathiriwa na shughuli za kibinadamu ikiwemo utiririshaji wa majitaka kutoka majumbani na viwandani kwenye maeneo ya vyanzo vya maji. Katika kutathmini ubora wa majitaka yanayotiririshwa, sampuli **524** zilichunguzwa kati ya sampuli **1,000** zilizopangwa kwa mwaka 2014/2015. Vielelezo ambavyo vinazingatiwa kwa kipimo cha lita moja ya majitaka ni *Biological Oxygen Demand (BOD)* ambayo haitakiwi kuzidi **miligramu 30**, *Chemical Oxygen Demand (COD)* **miligramu 60**, *Nitrates miligramu 20* na *Phosphorous miligramu 6*. Matokeo ya uchunguzi yalionesha **asilimia 93** ya sampuli zilikidhi viwango vya kurudishwa kwenye mazingira. Wizara inaendelea kukagua na kutoa ushauri wa kitaalam kuhusu uboreshaji wa mabwawa na mifumo ya kutibu majitaka kwa mamlaka husika ili kulinda mazingira dhidi ya uchafuzi.

#### **(f) Ubora wa Madawa ya Kusafisha na Kutibu Maji**

**78. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka za Maji na vyombo vya usambazaji maji vijijini vinalazimika kutumia madawa ya kutibu maji yanayozalishwa na kusambazwa kwa matumizi ya majumbani. Viwango vya ubora wa madawa yanayotumika hutakiwa kuthibitishwa kabla ya matumizi husika kwa lengo la kulinda afya za wananchi na usalama wa maji kwa ujumla. Katika mwaka 2014/2015, jumla ya sampuli **24** za madawa mbalimbali ya kusafisha na kutibu maji zilichunguzwa na kukidhi viwango. Madawa hayo ni pamoja na *Calcium hypochlorite*, *Aluminium Sulphate*, *Poly-Aluminium Chlorite*, *Soda Ash*, *Magna floc* na *Algal Floc*. Wizara imeendelea kuzishauri taasisi za

umma na binafsi kuhakiki ubora wa madawa ya kusafisha na kutibu maji kabla ya kununuliwa, kwa lengo la kunusuru rasilimali fedha inayoweza kupotea kwa kununua madawa yasiyofaa kwa matumizi yaliyolengwa.

**(g) Juhudi za Kuondoa Madini ya *Fluoride* katika Maji ya Kunywa na Matumizi ya Nyumbani**

**79. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, maandalizi ya kupata benki ya takwimu na kuchora ramani inayoonesha maeneo yaliyoathiriwa na uwepo wa madini ya *fluoride* kwa wingi katika maji imeendelea kufanyika ili kuandaa ramani inayoonesha ukanda wa *fluoride (fluoride belt)* hapa nchini. Kazi iliyofanyika ni kutambua vyanzo vyote vya maji katika Halmashauri za Wilaya za Arusha Mjini, Karatu, Arumeru, Longido, Monduli na Ngorongoro Mkoani Arusha; Wilaya za Simanjiro, Hanang, Babati, Mbulu na Kiteto Mkoani Manyara. Katika kutekeleza kazi hiyo, jumla ya vyanzo vya maji **954** vimekaguliwa na maji kufanyiwa uchunguzi wa kemikali na kuangalia uwepo wa madini ya *fluoride*. Zoezi la kuhakiki takwimu zilizopatikana linaendelea ili kupata takwimu sahihi zitakazowekwa kwenye ramani hiyo na vilevile kupata benki ya takwimu ya madini ya *fluoride (fluoride database)* hapa nchini.

**80. Mheshimiwa Spika**, katika kupanua wigo wa upatikanaji wa teknolojia ya uondoaji wa madini ya *fluoride*, kituo cha utafiti wa kemikali ndani ya maji cha Ngurdoto kimeanza utafiti kwenye maeneo yenye madini ya *phosphate* yanayowezesha kutengeneza *artificial hydroxyl apatite* inayotumika katika uondoaji wa madini ya *fluoride* kama zilivyo chengachenga za mifupa ya ng'ombe. Maeneo yaliyoanza kufanyiwa utafiti wa ubora wa udongo wenyе madini ya *phosphate* ni Matombo Mkoani Morogoro, Mlima Panda (Mbeya) na Minjingu Mkoani Arusha. Vilevile, elimu kuhusu uondoaji madini ya *fluoride* kwa kutumia chengachenga za mifupa ya ng'ombe imeendelea kutolewa kwa jamii kuititia warsha, makongamano na maadhisho ya Wiki ya Maji.

**81. Mheshimiwa Spika**, Wizara imepokea mtambo wa majaribio wa kusafisha na kutibu maji kutoka Kampuni ya Marekani (*International Water Company*). Mtambo huo umefanyiwa majaribio ya awali na umeonesha kuwa na uwezo wa kuondoa madini ya *fluoride*. Chanzo cha maji chenye madini ya *fluoride* ya kiwango cha **miligramu 20** kwa kila lita moja ya maji kilifanyiwa majaribio, ambapo mtambo huo umeweza kupunguza kiwango hicho hadi kufikia kiasi cha **miligramu 0.06**. Mtambo huo wa kisasa unatumia nishati ya jua, upopo na umeme wa kawaida hivyo, unaweza kutumika katika ngazi ya jamii kwa maeneo ya vijijini na mijini. Kwa sasa majaribio ya ziada yanaendelea ili kujua uwezo wa chujio (*filter media*) ina uwezo wa kusafisha maji kwa kiwango gani kabla ya chujio hilo kubadilishwa. Matokeo ya majaribio hayo yatatoa mwelekeo kwa Wizara kuweza kutoa mwongozo juu ya matumizi ya teknolojia hiyo mpya kwa Halmashauri na Mamlaka za Maji zilizo kwenye maeneo yaliyoathiriwa na madini ya *fluoride*.

**82. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/2016, Wizara yangu itaendelea kutekeleza mkakati wa kuondoa madini ya *fluoride* katika maji ya kunywa na kupikia kwa kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya kuondoa *fluoride* katika ngazi ya kaya na mitambo **1,000** ya kuondoa madini ya *fluoride* kwenye maji itasambazwa. Katika ngazi

ya jamii mitambo itajengwa kulingana na mahitaji. Kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali, utafiti wa kupata mitambo ya kisasa yenye gharama nafuu utaendelea. Aidha, kazi ya kubaini vyanzo vya maji vilivyoathirika na madini ya *fluoride* itaendelea katika mikoa iliyopo kwenye ukanda wa *fluoride*.

**(h) Maabara za Maji kupata Ithibati (Accreditation)**

**83. Mheshimiwa Spika**, katika hotuba yangu ya mwaka jana, nililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa Maabara ya Maji Jijini Mwanza ilikuwa imefikia hatua nzuri ya kupata ithibati. Napenda kuliarifu Bunge lako kuwa, tarehe 30/03/2015, Maabara hiyo imepata ithibati. Mafanikio hayo yametokana na Bodi ya Taasisi inayotoa ithibati katika nchi za Kusini mwa Afrika (*Southern Africa Development Community Accreditation Services - SADCAS*) kuthibitisha kuwa Maabara imetimiza vigezo vyote vya kiutawala na kiutendaji vilivytakiwa. Aidha maabara ya Mwanza imekabidhiwa rasmi cheti cha ithibati tarehe 15/05/2015 na kupewa namba maalum “TEST – 50011” ikianisha uwezo wa kuweza kupima viashiria 15 vya kemikali katika maji (*Chemical Analysis to ISO/IEC17025:2005*). Hivyo, kufanikiwa kupata kwa ithibati kunatoa fursa nyingi kwani kwa sasa kazi zake zinatambulika kitaifa na kimataifa. Vilevile, kuanzia mwezi Juni 2015, Maabara ya Mwanza itaanza kuonekana kwenye tovuti ya SADCAS ambayo ni [www.sadcas.org](http://www.sadcas.org).

**84. Mheshimiwa Spika**, kupatikana ithibati kwa Maabara ya Mwanza, kumeongeza ari kwa maabara nyingine kuanza mchakato unaolenga kukidhi viwango vya kitaifa na kimataifa. Katika kutekeleza hayo, Maabara za Maji za Dar es Salaam na Iringa zimeanza mafunzo ya uandaaji wa miongozo ya usimamizi (*Quality Management Systems*) ambayo ni kigezo kikubwa cha maabara kupata ithibati. Aidha, kwa kutumia uzoefu uliopatikana katika mchakato mzima wa kupata ithibati kwa Maabara ya Mwanza, maabara nyingine zote zitaendelea na ushiriki wa mazoezi ya kujipima kiutendaji kwa kuchunguza sampuli kitaifa na kimataifa (*Proficiency Testing*) ili matokeo hayo yaendelee kubaini maeneo muhimu zaidi ya kufanya maboresho katika maabara hizo.

**(i) Utekelezaji wa Mpango wa Usalama wa Maji**

**85. Mheshimiwa Spika**, usalama wa maji unahitaji kuwa na mpango wa usimamizi na ufuutiliaji kuanzia kwenye chanzo hadi kwa mtumiaji. Wizara yangu imeanza kutekeleza Mpango wa Usalama wa Maji (*Water Safety Plan*) kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii pamoja na Shirika la Afya Duniani ili uweze kutumika katika mamlaka zinazotoa huduma za usambazaji maji. Majaribio ya mpango huo yanafanyika katika Mamlaka ya Maji Kigoma na Chombo cha Watumia Maji cha Mbande-Kongwa. Wataalam wa kada mbalimbali katika mamlaka hizo wamepata mafunzo yaliyohusisha Washauri wa Maji wa Mikoa, Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya kutoka katika maeneo ya majaribio.

**86. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Maji (*International Water Association – IWA*) ilitoa mafunzo

kuhusu uandaaji wa Mipango ya Usalama wa Maji kwa wataalam **35** kutoka Maabara za Ubora wa Maji; Mamlaka za Maji za Mtwara, Iringa, Kigoma; pamoja na Mradi wa Kitaifa wa Masasi-Nachingwea. Mafunzo hayo yaliwezesha wataalam kubaini njia mbalimbali zinazoweza kuathiri usalama wa maji siyo kwenye chanzo cha maji pekee, bali hata ndani ya mifumo ya kutibu na kusambaza maji. Wataalam hao watashirikiana na Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini pamoja na Vyombo vya Watumiaji Maji katika kuandaa mipango ya usalama wa maji kwa taasisi hizo. Katika mwaka 2015/2016, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na taasisi na mashirika mbalimbali ili kuboresha hali ya usalama wa maji kwa ajili ya kulinda afya za wananchi. Katika kutekeleza hayo, Wizara itaandaa miongozo ya utekelezaji wa Mipango ya Usalama wa Maji katika ngazi za Mamlaka za Maji na Vyombo vya Watumia Maji Vijijini (COWSOs).

**(j) Mafunzo kwa Watumishi wa Maabara**

**87. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha kuwa watumishi wa kada ya uchunguzi wa ubora wa maji wanaendelea kutoa huduma stahiki kwa wananchi, watumishi **90** walipata mafunzo katika nyanja mbalimbali. Mafunzo hayo yalihusisha *Global Information System (GIS)*, *Good Laboratory Practices (GLP)*, *ISO 17025:2005*, *Best Microbiology Practice for laboratory accreditation* na *Laboratory Information Management System*. Katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kuwajengea uwezo watumishi ili waendelee kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

**(k) Ujenzi na Ukarabati wa Maabara za Maji**

**88. Mheshimiwa Spika**, katika juhudzi za Wizara yangu kuboresha na kusogeza karibu zaidi huduma za ubora wa maji kwa wananchi, Wizara inakarabati na kujenga maabara mpya za maji katika mikoa mbalimbali. Hadi mwezi Aprili 2015, ujenzi wa Maabara ya Kigoma umefikia **asilimia 65**, Singida **asilimia 55**; ukarabati wa Maabara ya Bukoba umefikia **asilimia 65**, na Shinyanga **asilimia 60**. Vilevile, zabuni za kujenga maabara za Mtwara na Mbeya pamoja na ukarabati wa majengo ya maabara katika Miji ya Songea na Sumbawanga zilitangazwa mwezi Februari, 2015. Mapitio ya michoro (*architectural and structural drawings*) kwa ajili ya ujenzi wa maabara za Morogoro, Tanga na Arusha yamefanyika mwezi Machi, 2015 na zabuni za ujenzi wa maabara hizo zitatangazwa baada ya taratibu za kifedha kukamilika. Aidha, mkataba kwa ajili ya upanuzi na ukarabati wa jengo la Maabara Kuu ya Maji Dar es Salaam upo katika hatua za mwisho kusainiwa.

**89. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/2016, Wizara yangu itaendelea kuzijengea uwezo maabara za maji nchini kwa kuzipatia vifaa vya kisasa vya kufanya uchunguzi na hivyo kuongeza tija. Vilevile, mazingira ya kufanya kazi za kiuchunguzi yataboreshwu zaidi ili kuongeza ari ya utendaji kazi na kulinda afya za watumishi. Aidha, Wizara yangu itaendelea kutekeleza mkakati wa usimamizi wa ubora wa maji na kudhibiti uchafuzi kwa kuchunguza sampuli **10,000** kutoka vyanzo mbalimbali vya maji na sampuli **1,500** za majitaka zitahakikiwa ubora wake kabla ya kutiririshwa kwenye vyanzo vya maji. Vilevile, elimu kuhusu ubora wa maji na ushauri wa kitaalam utatolewa

kwa taasisi na vyombo vinavyotoa huduma ya usambazaji maji safi na salama vijiji na mijini.

## 3.2 HUDUMA YA MAJI VIJIJINI

### 3.2.1 Mpango wa “Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa” (*Big Results Now – BRN*)

**90. Mheshimiwa Spika**, Serikali ilianda mpango mkubwa wa kupeleka maji safi na salama vijijini chini ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (*Water Sector Development Programme*) ilioanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2007/2008. Programu hiyo iligubikwa na urasimu mkubwa katika utekelezaji wake uliosababishwa na masharti yaliyowekwa kabla ya kuanza kwa mradi ikiwa ni pamoja na:-

- (i) Kupata kibali (*No Objection*) cha Benki ya Dunia katika uteuzi wa Wahandisi Washauri (*Wasimamizi*) wa kila mradi kabla ya kuanza ujenzi;
- (ii) Kupata kibali cha Wizara ya Maji katika kuteua Wakandarasi wa ujenzi wa kila mradi;
- (iii) Kupata michango ya wananchi wanaonufaika na mradi inayofikia **asilimia 5** ya thamani ya mradi kabla ya ujenzi kuanza;
- (iv) Kuhitajika kwa Halmashauri kutoa elimu, kuanzisha na kusajili Vyombo vya Watumiaji Maji (*COWSOs*) katika kila eneo la mradi kabla ya ujenzi wa mradi wowote kuanza; na
- (v) Baadhi ya Halmashauri kutaka kupokea fedha zote zinazotosha kujenga mradi kabla ya mradi husika kuanza kujengwa.

**91. Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Juni, 2012, Wilaya **12** tu kati ya **132** zilikuwa zimetimiza masharti hayo na kuanza utekelezaji. Kutokana na hali hiyo, kuanzia mwezi Julai, 2013, Wizara kupitia Mpango wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa (*BRN*) iliondoa urasimu huo ili kuharakisha uandaaji na utekelezaji wa miradi ya maji vijijini. Katika kutekeleza mpango huo, madaraka yote ya kubuni, kuandaa, kutekeleza na kusimamia miradi ya maji vijijini yalikasimiwa kwa Halmashauri za Wilaya ili kuwa na miradi na huduma endelevu. Vilevile, bajeti ilitengwa katika Sekretarieti za Mikoa kwa ajili ya kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa kazi za ujenzi wa miradi. Aidha, Wizara inaendelea kutekeleza majukumu yake ya kutafuta fedha, kuandaa miongozo, kutoa utaaliam unaohitajika na kuzijengea uwezo Halmashauri kwa kuzipatia wataalam wa nyanja mbalimbali wakiwemo wahandisi na mafundi sanifu.

**92. Mheshimiwa Spika**, kabla ya kuanza kutekeleza mpango wa *BRN*, idadi ya wakazi wa vijijini waliokuwa wananufaika na huduma ya maji safi ni wastani wa watu **200,000** hadi **400,000** kwa mwaka. Baada ya kuondolewa kwa urasimu na kuanza kutekelezwa kwa mpango wa *BRN*, jumla ya miradi ya maji **248** kwenye Halmashauri **98** ilijengwa kwa kipindi cha mwaka mmoja. Utekelezaji huo uliongeza idadi ya wakazi wa vijijini wanaopata huduma ya maji safi na salama kutoka wakazi **milioni 15.2** mwezi Julai, 2013 hadi wakazi **milioni 17.8** mwezi Juni 2014, sawa na ongezeko la wakazi **milioni 2.6**.

**93. Mheshimiwa Spika**, mpango wa *BRN* kwa Sekta ya Maji umejielekeza katika utoaji wa huduma ya usambazaji maji na usafi wa mazingira vijijini kwa kutekeleza kazi za ujenzi wa miradi mipy; ukarabati wa miundombinu chakavu; upanuzi wa miradi iliyopo; na uendeshaji na matengenezo (*operation and maintenance*). Ujenzi wa miradi mipy unahuishisha miradi ya vijiji 10 kwa kila Halmashauri na miradi ya kimkakati. Miradi ya upanuzi na ukarabati inahuishisha utekelezaji wa miradi ya matokeo ya haraka kwa kujenga miundombinu kutoka kwenye vyanzo vikiwemo mabwawa, visima virefu na chemichemi. Vilevile, uendeshaji na matengenezo unahusu kuvijengea uwezo Vyombo vya Watumiaji Maji na ukusanyaji wa taarifa za utekelezaji.

### 3.2.2 Utekelezaji wa *BRN* kwa Miradi ya Maji Vijijini

**94. Mheshimiwa Spika**, baada ya Serikali kutekeleza mpango wa *BRN* kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia mwezi Julai 2013 mpaka mwezi Juni 2014, iliona umuhimu wa kujitathmini kwa kuajiri Mtaalam Mshauri kupima utekelezaji wa mpango huo kwa sekta zote sita zilizoanza kutekeleza *BRN*. Kazi hiyo ilifanywa na Kampuni ya PricewaterhouseCoopers (PwC) na kuthibitishwa na Kamati ya Watu Mashuhuri Duniani (Committee of Eminent Persons) mwezi Januari, 2015. Matokeo ya tathmini hiyo yameonesha mafanikio makubwa kwa upande wa Sekta ya Maji ambapo imeweza kufikia **asilimia 80** ya malengo yaliyowekwa na kuongoza kwa kiwango cha juu kati ya Sekta zilizoanza kutekeleza mpango wa *BRN*.

**95. Mheshimiwa Spika**, mafanikio yaliyopatikana kutokana na mpango wa *BRN* ni pamoja na kuongezeka kwa idadi ya wananchi wanaopata huduma ya maji vijijini kutoka wananchi **15,200,000** sawa na **asilimia 40** mwezi Juni, 2013 hadi kufikia wananchi **20,957,855** sawa na **asilimia 55.9** mwezi Aprili, 2015. Hili likiwa ni ongezeko la zaidi ya wananchi **milioni 5.76** wanaopata huduma ya maji katika kipindi hicho cha utekelezaji wa mpango huo. Lengo ni kufikia **asilimia 74** ifikapo mwezi Juni, 2016.

**96. Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia malengo ya *BRN* ya kuhakikisha miradi ya maji vijijini inatekelezwa kitaalam kwa ufanisi na haraka, Wizara yangu imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kufanikisha utekelezaji wa mpango huo. Hatua hizo ni pamoja na kuajiri wataalam ambao wamepangiwa vituo vya kazi katika ngazi za Wizara, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri. Hadi mwezi Aprili 2015, jumla ya wataalam **318** wa fani mbalimbali za kiufundi walajiriwa. Hatua nyingine zilizochukuliwa ni kupunguza muda wa ununuzi wa Wataalam Washauri na Wakandarasi kutoka siku **210** hadi siku **97** kwa kuondoa vibali visivyo vya lazima; na kuendelea na ujenzi wa miradi ya maji hata kama michango ya wananchi haijakamilika. Aidha, Wizara imeendelea kuwahamasisha wananchi kutoa michango itakayotumika kwa ajili ya uendeshaji na matengenezo ya miradi hiyo baada ya ujenzi kukamilika.

**97. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu ilitengewa **shilingi bilioni 270.98** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji vijijini. Hadi mwezi Aprili 2015, kati ya fedha hizo, **shilingi bilioni 76.52** sawa na **asilimia 28** zilitolewa na kutumwa kwenye Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa. Matumizi ya fedha hizo, kiasi cha

**shilingi bilioni 73.09** yalilenga utekelezaji na usimamizi wa miradi ya maji ya vijiji 10 kwa kila Halmashauri; na **shilingi bilioni 3.43** zilizobaki zilielekezwa kwenye miradi mingine ya maji vijijini ambayo inahusisha miradi yenye kuleta matokeo ya haraka, ujenzi wa mabwawa na gharama za ziada (*incremental cost*) za usimamizi na ufuatiliaji wa miradi. Vilevile, kiasi kingine cha **shilingi bilioni 6.71** kilikasimiwa kupitia Mafungu ya Mikoa kwenda kwenye Halmashauri, OWM-TAMISEMI na Wizara zinazoshiriki katika kutekeleza Kampeni ya Kitaifa ya Usafi wa Mazingira Vijijini.

### 3.2.3 Mpango wa *BRN* kwa mwaka 2015/2016

98. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/2016, Wizara yangu itaendelea kujenga, kupanua na kukarabati miundombini ya maji vijijini chini ya mpango wa *BRN*. Jumla ya **shilingi bilioni 269.57** zimepangwa kutumika, na kati ya hizo **shilingi bilioni 167.82** ni fedha za ndani na **shilingi bilioni 101.75** ni fedha za nje. Katika kutekeleza miradi hiyo, vijiji **534** vitanufaika kwa kupatiwa miradi ya maji ambapo vituo **9,757** vya kuchotea maji vitajengwa na kuhudumia jumla ya wakazi **2,439,462** waishio vijijini. **Majedwali Na. 5a na 5b** yanaonesha mgawo wa fedha zitakazotumwa katika Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa kutekeleza miradi ya maji vijijini na kwa ajili ya usimamizi wa miradi ya maji katika ofisi ya mkoa kwa mwaka 2015/2016.

### 3.2.4 Hali ya Utekelezaji wa Miradi ya Maji Vijijini

99. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kutekeleza jumla ya miradi **1,814** ya maji vijijini katika Halmashauri zote nchini. Miradi hiyo inahusu ujenzi wa miradi ya vijiji 10, miradi ya kimkakati, miradi ya upanuzi na ukarabati pamoja na miradi inayofadhiliwa na wadau mbalimbali. Hadi mwezi Aprili 2015, jumla ya miradi ya maji **975** katika vijiji **1,206** yenyе jumla ya vituo **24,129** vya kuchotea maji imekamilika kwenye Halmashauri **148**. Utekelezaji huo umewanufaisha wakazi **milioni 5.75** waishio vijijini na kuongeza idadi ya watu wanaopata huduma ya majisafi vijijini kufikia **20,957,855** sawa na **asilimia 55.9**. **Jedwali Na. 6** linaonesha orodha ya vijiji **1,206** vilivyopata huduma kutoka kwenye miradi iliyokamilika chini ya mpango wa *BRN* pamoja na wakazi walionufaika na miradi hiyo.

100. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea kutekeleza miradi **839** iliyobaki katika vijiji **1,115** inayohitaji jumla ya **shilingi bilioni 234.6** kuikamilisha. Miradi hiyo imefikia hatua mbalimbali za utekelezaji na ikikamilika itahudumia watu **5,594,493**. Kati ya miradi hiyo, utekelezaji wa miradi **262** kwenye vijiji **311** upo kati ya **asilimia 71** hadi **asilimia 95**, na jumla ya **shilingi bilioni 40.14** zinahitajika kuikamilisha miradi hiyo itakayohudumia watu **1,732,800**. Kufanikiwa kwa lengo hilo kutategemea upatikanaji wa fedha zilizopangwa kwa wakati. **Jedwali Na. 7** linaonesha miradi **262** ambayo utekelezaji wake upo kati ya **asilimia 71** na **asilimia 95**.

#### (a) Ujenzi wa Miradi Mipyä

##### (i) Miradi ya Kimkakati

##### *Mradi wa Maji Tabora*

**101. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Japan inatekeleza mradi wa maji katika vijiji **19** kwenye Wilaya zote **saba** za Mkoa wa Tabora. Mradi unatekelezwa katika awamu mbili; Awamu ya Kwanza ilianza mwezi Septemba, 2009 na kukamilika mwezi Mei, 2011 kwa kukarabati visima virefu na vifupi **46**; kuandaa Mpango Mahsusini wa Maji Vijijini kwa Mkoa; kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa miradi ya maji katika vijiji **19**; na kuandaa makadirio ya gharama za ujenzi na makabrasha ya zabuni.

**102. Mheshimiwa Spika**, Awamu ya Pili ya mradi huo inayogharimu **Yeni za Kijapani bilioni 1.56** sawa na **shilingi bilioni 25.2** imeanza kutekelezwa mwezi Aprili, 2014. Utekelezaji unahusu uchimbaji wa visima virefu, ujenzi wa matanki ya maji, ujenzi wa nyumba ya pampu na ulazaji wa mabomba katika vijiji **19** kwenye Wilaya zote za Mkoa wa Tabora. Hadi mwezi Aprili 2015, jumla ya visima **38** vimekamilika na kupata maji safi katika Halmashauri za Wilaya za Sikonge, Kaliua, Uyui, Nzega, Urambo, Igunga na Manispaa ya Tabora. Vilevile, kazi ya ujenzi wa matanki ya maji; ujenzi wa nyumba ya pampu; na ulazaji wa mabomba katika vijiji vya Mabama (Wilaya ya Uyui) na Kakola (Manispaa ya Tabora) kwa pamoja umefikia wastani wa **asilimia 70**. Aidha, vifaa vya kisasa vya kutafiti maji chini ya ardhi vyenye thamani ya **shilingi milioni 615.39** vimenunuliwa na kukabidhiwa ofisi ndogo ya Tabora katika Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Tanganyika. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2016 na utawanufaisha zaidi ya wakazi **40,352** wa Wilaya hizo.

#### ***Mradi wa Maji Bungu - Korogwe***

**103. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la *World Vision* inatekeleza mradi wa Maji wa Bungu uliopo katika Wilaya ya Korogwe. Mradi huo unahusu upanuzi na ukarabati. Utekelezaji wa mradi huo umeendelea katika vijiji vya Msasa, Bungu, Bungu-Msiga na Manka na hadi sasa wakazi **9,306** wameanza kunufaika na huduma ya maji safi. Katika mwaka 2014/2015, kazi zilizotekeliza na kukamilika ni ujenzi wa tanki lenye ujazo wa **lita 90,000** katika Kitongoji cha Sinai-Kwebago kijiji cha Bungu; ulazaji wa mabomba urefu wa **Kilomita 5.3** kutoka tanki la Gare hadi Kijiji cha Bungu-Msiga; pamoja na kujenga vituo **vitano** vya kuchotea maji. Katika mwaka 2015/2016, Wizara yangu itakamilisha miradi ya maji katika vijiji viliviyobaki vya Mlunghi, Kwemshai na Ngulu. Kukamilika kwa miradi hiyo, wakazi **18,460** wa vijiji **saba** vya Bungu, Bungu-Msiga, Kwemshai, Ngulu, Mlunghi, Msasa na Manka watanufaika na huduma ya maji safi na salama.

#### ***Mradi wa Maji wa Same – Mwanga – Korogwe***

**104. Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha wananchi wa maeneo ya Wilaya za Same, Mwanga na Korogwe wanapata huduma ya maji safi, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (*BADEA*) na Mfuko wa Maendeleo wa Nchi Zinazozalisha Mafuta (*OFID*) inatekeleza mradi wa Same-Mwanga-Korogwe. Mkataba wa ujenzi wa Fungu la Kwanza la Mradi (*Contract Package I*) kwa Awamu ya Kwanza, umesainiwa tarehe 20/11/2014 kati ya Wizara na Mkandarasi kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 41.36**. Katika kutekeleza mradi huo, Serikali itachangia **Dola**

**za Marekani milioni 19.36**, mchango wa *BADEA* ni **Dola za Marekani milioni 10** na *OFID* itachangia **Dola za Marekani milioni 12**.

**105. Mheshimiwa Spika**, Mkandarasi wa Awamu ya Kwanza ya mradi ameshaanza kazi na atatekeleza mradi huo kwa kipindi cha miezi 31. Mradi utakamilika mwezi Juni, 2017. Kazi zitakazotekelawa ni kujenga choteo la maji (*intake*) katika Bwawa la Nyumba ya Mungu; mtambo wa kutibu maji eneo la Njia Panda; kulaza bomba kuu lenye kipenyo cha **milimita 1,000** umbali wa **kilomita 2.5** kutoka kwenye choteo la maji hadi mtambo wa kutibu maji; na kulaza bomba lenye kipenyo cha **milimita 900** umbali wa **kilomita 10.3** kutoka kwenye mtambo wa kutibu maji hadi matanki ya kituo cha kusukuma maji Kisangara.

**106. Mheshimiwa Spika**, katika hatua ya maandalizi ya Awamu ya Pili ya mradi, mikataba ya mkopo wa fedha (*Loan Agreements*) imesainiwa kati ya mwezi Oktoba na Desemba, 2014 ambapo *BADEA* itatoa **Dola za Marekani milioni 12, Kuwait Fund Dola za Marekani milioni 34** na *Saudi Fund* itachangia **Dola za Marekani milioni 25**. Mkataba wa mkopo wa fedha kutoka *OFID* wa **Dola za Marekani milioni 15** umesainiwa tarehe 08/04/2015.

**107. Mheshimiwa Spika**, kazi zitazotekelawa katika Awamu ya Pili ya mradi ni ujenzi wa mtambo wa kusukuma maji na ulazaji wa bomba kuu kutoka eneo la Kisangara hadi tanki la Kiverenge; ujenzi wa matanki **mawili** yenye ujazo wa **lita milioni 7.5** kila moja eneo la Kiverenge na kulaza mabomba ya kupeleka maji kutoka Kiverenge hadi miji ya Mwanga na Same; ujenzi wa tanki lenye ujazo wa **lita milioni 6** katika Mji wa Mwanga na tanki lenye ujazo wa **lita milioni 9** katika Mji wa Same; pamoja na kulaza mabomba ya kusambaza maji katika Miji ya Same na Mwanga. Aidha, Serikali inaendelea na taratibu za kumwajiri Mtaalam Mshauri kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa Awamu ya pili ya Mradi. Ujenzi wa mradi unatarajiwa kuanza mwezi Septemba, 2015 baada ya kumpata Mkandarasi. Mradi utakapokamilika utahudumia jumla wakazi **456,931** wa Miji ya Same na Mwanga. Awamu ya tatu ya utekelezaji wa mradi huo itahusisha jumla ya vijiji **38** vya Wilaya za Same vijiji **16**, Mwanga (**17**) na Korogwe (**5**).

#### ***Mradi wa Maji Masoko - Rungwe***

**108. Mheshimiwa Spika**, mradi wa Masoko ulianza kutekelezwa mwezi Septemba, 2010 na kutegemewa kukamilika mwezi Novemba, 2011 kulingana na mkataba. Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ilisitisha mkataba na Mkandarasi kwa kushindwa kutekeleza kazi kulingana na viwango vya usanifu. Hata hivyo, Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe inaendelea na taratibu za usuluhishi na kutafuta Mkandarasi wa kukamilisha mradi huo. Katika mwaka 2015/2016, Wizara yangu imetenga jumla ya **shilingi bilioni 1.76** kwa ajili ya kumalizia kazi zilizobaki ili kuharakisha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wakazi wa Masoko.

#### ***Mradi wa Maji Mkoani Kigoma***

**109. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Ubelgiji inatekeleza miradi ya maji katika vijiji vya Halmashauri za Mkoa wa Kigoma (*Water and Sanitation Kigoma Region Projects - WaSKiP*). Miradi hiyo itagharimu **shilingi bilioni 20.6**, kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 18.13** sawa na **Euro milioni 8** zitatolewa na Serikali ya Ubelgiji na **shilingi bilioni 2.44** zitatolewa na Serikali ya Tanzania. Hadi mwezi Aprili 2015, mpango wa utekelezaji wa miradi hiyo umeanza kwa kubainisha jumla ya vijiji **26** vya kipaumbele katika Halmashauri zote za Mkoa wa Kigoma. Mpango huo umeonesha kuwa jumla ya wakazi **200,000** watanufaika na huduma ya maji. Mradi huo unatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano, kuanzia mwaka 2014/2015. Katika mwaka 2015/2016, Serikali imetenga kiasi cha **shilingi bilioni 1.04** sawa na **Euro 650,000** kwa ajili ya kuanza ujenzi wa mradi huo. **Jedwali Na. 8** linaonesha orodha ya vijiji **26** vya kipaumbele katika Halmashauri zote mkoani Kigoma.

**(ii) Miradi yenyе Kuleta Matokeo ya Haraka (*quickwins*)**

***Mradi wa Maji kwa Vijiji 100 Vinavyopitiwa na Bomba Kuu kutoka Ziwa Victoria hadi Kahama-Shinyanga***

**110. Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa maji wa vijiji **100** vilivyopo pembezoni mwa bomba kuu la maji kutoka Ziwa Victoria hadi Miji ya Kahama na Shinyanga. Mradi huo unahusu uboreshaji wa huduma ya upatikanaji wa maji kwenye vijiji **40** vya awali vilivytambuliwa katika Halmashauri za Misungwi, Kwimba, Shinyanga na Msalala.

**111. Mheshimiwa Spika**, mradi huo umeanza kutekelezwa na hadi mwezi Aprili 2015, upimaji na usanifu ulikamilika katika vijiji **31** kati ya vijiji **40** kwenye Halmashauri za Msalala na Shinyanga. Vijiji **tisa** vinavyobaki vitatekelezwa katika mwaka 2015/2016. Gharama ya ujenzi wa mradi kwenye vijiji hivyo **31 ni shilingi bilioni 2.59** na utekelezaji wake upo katika hatua mbalimbali kama ifuatavyo: Ujenzi wa vituo **16** vya kuchotea maji na mabirika **manne** ya kunyweshea mifugo katika vijiji **vinne** vya Magobeko, Nyashimbi, Kakulu na Butegwa kwenye Halmashauri ya Msalala umekamilika; ujenzi wa vituo **tisa** vya kuchotea maji na mabirika **mawili** ya kunyweshea mifugo katika vijiji vingine **sita** vilivyopo Halmashauri ya Shinyanga utakamilika ifikapo mwezi Juni, 2015; na ujenzi wa vituo **nane** vya kuchotea maji na mabirika **mawili** ya kunyweshea mifugo katika vijiji **viwili** vya Mwasekagi na Mwakatolya katika Halmashauri ya Shinyanga umeanza na utakamilika mwezi Oktoba, 2015.

***Mradi wa Maji wa Ntomoko***

**112. Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imeendelea kutekeleza mradi wa maji wa Ntomoko uliolenga kuhudumia vijiji **18** katika Halmashauri za Kondo na Chemba. Kutokana na kuongezeka kwa idadi ya wakazi katika vijiji vinavyokusudiwa kuhudumiwa na mradi huo ikilinganishwa na uwezo wa chanzo kilichopo, iliamuliwa kuwa vijiji vitakavyohudumiwa viwe **10** ambapo ukarabati wa mtandao wa mabomba ya usambazaji maji kwa sasa umefikia **asilimia 40**. Vijiji hivyo ni Makirinya, Kirere cha Ng'ombe, Lusangi, Hamai, Songolo, Madaha, Churuku, Kimkima, Jinjo na Jangalo. Kwa

vijiji **vinane** vilivyobaki iliamuliwa vichimbwe visima na utekelezaji wake upo katika hatua mbalimbali. Hadi mwezi Aprili 2015, ujenzi wa miundombinu katika vijiji vya Jenjeluse na Goima umefikia **asilimia 98**; Kijiji cha Mtakuja **asilimia 95** na Kijiji cha Mlongia **asilimia 80**. Uchimbaji wa visima katika vijiji vya Mapango na Chandama umekamilika na vimepata maji, utafiti wa kina unaendelea katika vijiji vya Igunga na Itolwa ili kupata maeneo bora ya kuchimba visima. Katika mwaka 2015/2016, Wizara imetenga jumla ya **shilingi bilioni 1.6** kwa ajili ya kumalizia kazi zilizobaki ili huduma ya maji ipatikane kwa wananchi wa vijiji hivyo.

#### ***Mradi wa Maji Chiwambo - Masasi***

**113. Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa mradi wa maji Chiwambo unaendelea na hadi mwezi Aprili, 2015 ulazaji wa mabomba kwa umbali wa **kilomita 24.8** umekamilika; ujenzi wa matanki **mawili** yenyeye ujazo wa **lita 50,000** kila moja katika vijiji vya Nagaga-Mitesa na Chiungutwa unaendelea, ukarabati wa matanki **manne** yenyeye ujazo wa **lita 25,000** kila moja umekamilika kwenye vijiji vya Luatala, Nagaga, Mpeta na Namalenga; ukarabati wa tanki **moja** lenye ujazo wa **lita 75,000** na kichoteo (*sump*) katika Kijiji cha Mitesa umefikia **asilimia 70**. Vilevile, kazi nyingine zinazoendelea ni pamoja na kukarabati nyumba ya mtambo wa kusukuma maji (*pump house*) ambayo utekelezaji wake umefikia **asilimia 50** na ujenzi wa vituo **36** vya kuchotea maji umefikia **asilimia 90**. Katika mwaka 2015/2016, Wizara itakamilisha kazi zilizobaki ili kuweza kuwapatia huduma ya maji wakazi wapatao **84,082** wa Kata **saba** za Lulindi, Lupumbulu, Namalenga, Chiungutwa, Sindano, Mchauru na Mbuyuni.

#### **(iii) Usambazaji wa Maji kutoka Visima Virefu na Vyanzo vya Maji Juu ya Ardhi**

**114. Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Aprili, 2015 jumla ya **shilingi bilioni 2.28** zilitumika kwa ajili ya kuendelea kutekeleza miradi ya kuleta matokeo ya haraka. Miradi hiyo ilihuisha ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya usambazaji maji kutoka kwenye visima virefu na vyanzo vingine juu ya ardhi. Katika mwaka 2015/2016, jumla ya **shilingi bilioni 93.58** zitatumika kutekeleza miradi ya kuleta matokeo ya haraka. Kati ya fedha hizo, **shilingi bilioni 75.4** zitatumika kwa ajili ya kuendeleza miradi ya maji ya visima virefu na vyanzo vingine vya maji juu ya ardhi. Vilevile, **shilingi bilioni 18.18** zitatumika kutekeleza miradi ya usambazaji maji kutoka kwenye mabwawa. Jumla ya vituo **9,123** vya kuchotea maji vitajengwa katika vijiji **376** ambapo wananchi **2,280,893** watanufaika na huduma ya maji safi.

#### **(iv) Upanuzi na Ukarabati wa Miradi ya Kitaifa**

**115. Mheshimiwa Spika**, upanuzi na ukarabati wa miradi ya kitaifa iliyoainishwa katika Mpango wa *BRN*, unahusu miradi **mitatu** ya kitaifa ya Makonde, Wang'ombe na Handeni Trunk Main (*HTM*).

#### ***Upanuzi na Ukarabati wa Mradi wa Kitaifa Makonde***

**116. Mheshimiwa Spika**, kazi zinazotekeliza zinahusu upanuzi na ukarabati wa miundombinu ya maji kutoka Mradi wa Kitaifa wa Makonde hadi kwenye vijiji vilivyomo pembezoni mwa mradi. Upembuzi yakinifu wa miundombinu chakavu umekamilika kwenye vijiji vilivyopo katika Halmashauri za Wilaya za Newala, Tandahimba na Mtwara Vijiji. Upembuzi huo ulibainisha kazi zote zinazotakiwa kufanyika ili kuboresha huduma ya maji katika eneo la mradi. Kazi hizo ni ununuzi na ufungaji wa vifaa vya mfumo wa umeme, viungio vya mabomba ya maji pamoja na vipuri vya mitambo ya kusukuma maji. Katika mwaka 2015/2016, Serikali imetenga **shilingi milioni 800** kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Uingereza kuitia Idara yake ya Maendeleo ya Kimataifa (*DFID*) imekamilisha upembuzi yakinifu wa kubaini gharama za kutekeleza mradi wa kutoa maji kutoka katika chanzo cha Mkunya kwenda katika Vijiji vya Chihanga, Mapili, Chikwedu, Chiunjira na Mpilipili vyenye wakazi wapatao **7,659** watakaonufaika na mradi huo. Ujenzi unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2015/2016.

#### ***Upanuzi wa Mradi wa Kitaifa Wanging'ombe***

**117. Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa kazi katika mradi huo utahusisha kusambaza maji kwenye vijiji vilivyopo pembezoni mwa bomba kuu kutoka vyanzo vya maji vya Mbukwa na Mtitafu hadi Wilayani Mbarali, Mkoa wa Mbeya. Upanuzi wa mradi huo wa kitaifa utafanyika baada ya kukamilika kwa ukarabati wa bomba kuu. Katika mwaka 2015/2016, Serikali imetenga **shilingi milioni 300** kwa ajili ya upanuzi wa mtandao wa mabomba ya kusambaza maji kwenda katika vijiji hivyo.

#### ***Upanuzi na Ukarabati wa Mradi wa Kitaifa Handeni (Handeni Trunk Main - HTM)***

**118. Mheshimiwa Spika**, upanuzi na ukarabati wa mradi huo unaendelea kwenye vijiji mbalimbali katika Halmashauri za Wilaya za Handeni, Korogwe na Kilindi. Hadi mwezi Aprili 2015, kazi zilizofanyika ni pamoja na ukarabati wa mabomba na valvu kutoka banio la Mandera hadi mtambo wa kutibu maji wa Tabora; kutoka mtambo wa kutibu maji wa Tabora hadi kituo cha kusukuma maji cha Kwamatuku; kutoka Kwamatuku hadi kwenye tanki la maji la Bongi; kutoka tanki la Bongi hadi Kwamkono; na njiapanda ya bomba kuu hadi tanki la maji la Komsala. Kukamilika kwa kazi hizo kumewanufaisha wakazi **50,000** kupata huduma ya maji katika Vijiji vya Vibaoni, Kwamasaka, Kwamgondi, Bangala, Kiva, Kibindu, Magamba, Bogolwa, Kwankonje na Kwachaga.

**119. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/2016, Serikali imetenga **shilingi milioni 500** kwa ajili ya kumalizia kazi zilizobaki. Kazi hizo ni pamoja na kuchimba mtaro wa kulaza bomba; kubadilisha mabomba na valvu maeneo ya tanki la Komsala hadi Michungwani; kubadilisha mabomba na valvu kutoka tanki la Bongi kwenda kwenye nyumba ya mitambo ya Sinden; na kununua mabomba, viungio, dira za maji na vifaa vingine vya matengenezo.

#### **3.2.5 Ujenzi wa Miradi Mingine ya Maji Vijiji**

**120. Mheshimiwa Spika**, katika jitihada za kuboresha hali ya upatikanaji wa maji vijijini, hususan katika maeneo kame, Serikali imeendelea kushirikiana na taasisi, mashirika na asasi mbalimbali katika kujenga miradi ya maji, ikiwemo ukarabati wa mabwawa yaliyopo, ujenzi wa mabwawa mapya na uvunaji wa maji ya mvua.

**(a)      Ukarabati na Ujenzi wa Mabwawa**

**121. Mheshimiwa Spika**, uwepo wa mabwawa ya maji ni ufumbuzi wa kero ya uhaba wa maji, hasa katika maeneo kame na kwenye vyanzo vyenye uwezo mdogo wa kutoa maji. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali imeendelea kukarabati mabwawa yaliyopo na kukamilisha ujenzi wa mabwawa katika maeneo mbalimbali nchini yakiwemo bwawa la Sasajila lililopo katika Wilaya ya Chamwino, Mkoani Dodoma; bwawa la Iguluba (Iringa Vijiini); bwawa la Habiya (Itilima - Simiyu); bwawa la Sekeididi (Kishapu – Shinyanga); bwawa la Matwiga (Chunya – Mbeya); bwawa la Kawa (Nkasi – Rukwa); bwawa la Wegero (Butiama – Mara); bwawa la Mwanjoro (Meatu – Simiyu); na bwawa la Kidete (Kilosa – Morogoro). Utekelezaji wa kazi hizo umefikia hatua mbalimbali na katika mwaka 2015/2016, Serikali imetenga jumla ya **shilingi bilioni 8** ili kukamilisha kazi hizo.

**122. Mheshimiwa Spika**, pamoja na jitihada nilizozieleza hapo juu, Serikali imepanga kujenga mabwawa mengine kwenye maeneo kame hasa vijijini ili kupunguza kero ya uhaba wa maji unaoendelea kuwakabili wananchi wa maeneo hayo. Katika mwaka 2015/2016, Serikali itanza kutekeleza miradi hiyo kwa kufanya upembuzi yakinifu kwenye maeneo kame na kubaini maeneo yanayofaa kujenga mabwawa hayo.

**(b)      Uvunaji wa Maji ya Mvua**

**123. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa utekelezaji wa miradi ya uvunaji wa maji ya mvua kuititia mapaa ya majengo, Wizara yangu imetoa miongozo kwa kila Halmashauri kutunga Sheria ndogo zenyne kuzitaka Taasisi, Asasi na watu binafsi kujenga miundombinu ya uvunaji wa maji ya mvua kwenye majengo yao. Vilevile, Sheria hizo zinalenga kuhakikisha kuwa michoro ya majengo yote yanayojengwa inajumuisha mifumo ya kuvuna maji ya mvua kabla ya ujenzi wa majengo hayo kuidhinishwa. Katika kutekeleza agizo hilo, Halmashauri **28** zimetunga Sheria ndogo kuhusu uvunaji wa maji ya mvua kutoka kwenye mapaa na Halmashauri zilizobaki zinaendelea na mchakato wa kutekeleza agizo hilo. Hadi mwezi Aprili 2015, matanki **800** ya **lita 1,000** hadi **5,000** yamejengwa kwenye maeneo mbalimbali kama shule, zahanati na taasisi nyingine katika Halmashauri zote nchini.

**3.2.6    Uendeshaji na Matengenezo**

**(a)      Takwimu za Vituo vya Kuchotea Maji  
(Water Point Mapping System)**

**124. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu iliendelea kutekeleza kazi ya kuainisha vituo vya kuchotea maji katika maeneo ya vijijini kwa

kutumia mfumo wa kompyuta uitwao *Water Point Mapping System-WPMS*. Kuainishwa kwa vituo hivyo, kumewezesha kufahamu kwa urahisi na usahihi takwimu za uendeshaji wa miundombinu ya maji na kuandaa ramani za vituo vya maji. Takwimu zinazopatikana huwezesha Halmashauri kufahamu hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika vijiji. Aidha, takwimu hizo zinapatikana kwenye tovuti ya Wizara ya Maji [www.maji.go.tz](http://www.maji.go.tz) na kuangalia *WPMS*.

**125. Mheshimiwa Spika**, zoezi hilo ni endelevu na limesaidia kupata takwimu sahihi na zilizoboresha kwa baadhi ya maeneo nchini. Hivyo, kupata taarifa sahihi za vituo vinavyotoa maji na visivyotoa maji kwa wakati husika. Kwa kuzingatia umuhimu wa upatikanaji wa takwimu sahihi, mwezi Machi 2015, Wizara yangu iliendesha zoezi la kuboresha taarifa hizo kwa kushirikiana na Wahandisi wa Halmashauri katika Halmashauri **67** kutoka Mikoa **10** ya Mwanza, Geita, Simiyu, Tabora, Singida, Kagera, Shinyanga, Dodoma, Kigoma na Mara. Matokeo yilibaini idadi ya vituo vipyta **6,228** vya kuchotea maji na kufanya jumla ya vituo vilivyopo kwenye mikoa hiyo kufikia **33,082** kwa sasa. Katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kuboresha takwimu za vituo vya kuchotea maji katika Halmashauri zilizobaki.

**126. Mheshimiwa Spika**, mukutano mkuu wa kikanda Barani Afrika kuhusu matumizi ya mfumo wa *Water Point Mapping (WPMS)* ulifanyika mwezi Februari, 2014 katika Hoteli ya *Ledger Plaza Bahari Beach*, jijini Dar es Salaam. Washiriki wa Mukutano huo walikuwa ni Wataalam wa Sekta ya Maji pamoja na Wadau kutoka ndani na nje ya nchi. Lengo la mukutano huo lilikuwa ni kujadili changamoto zinazoukabili mfumo huo katika ukusanyaji wa takwimu na utoaji wa taarifa kwa wakati kuhusu upatikanaji wa huduma ya maji vijijini. Katika kufikia lengo hilo, Mukutano ulitoa maazimio ya utekelezaji yanayojumuisha hatua nne zifuatazo:-

- (i) Kutoa mafunzo stahiki kwa wakusanyaji wa takwimu katika ngazi za Wilaya na kukusanya takwimu za vituo vya kuchotea maji katika maeneo ambayo yalikuwa hayafikiwi ili kuhuisha taarifa kwenye mfumo;
- (ii) Kurasimisha matumizi ya mfumo wa *WPMS* ili kuhakikisha taasisi za watendaji katika Sekta ya Maji zinawasilisha taarifa katika kila kipindi cha robo mwaka kama ilivyo katika mifumo mingine;
- (iii) Kutoa taarifa ya hali halisi ya vituo vya kuchotea maji ikiwa ni pamoja na ubora wa maji na upatikanaji wake; na
- (iv) Kuoanisha mfumo huo na mifumo mingine ya kielektroniki kama *PLANREP*, *EPICOR*, *MIS* ili taarifa hizo ziwe zinapatikana kwa haraka na kwa gharama nafuu.

**(b) Vyombo vya Watumiaji Maji**

**127. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeweka sheria, kanuni na taratibu zitakazohakikisha kuwa miradi ya maji iliyokamilika inakuwa endelevu kwa kuunda

Vyombo vya Watumiaji Maji (COWSOs) kwa ajili ya kusimamia miradi hiyo. Kulingana na Kifungu **Na. 31** cha Sheria **Na. 12** ya mwaka 2009 ya Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, Halmashauri zinaelekezwa kusajili COWSOs kwa mujibu wa sheria ili uendeshaji na usimamizi wa miradi hiyo kuwa endelevu. Wizara yangu, imetoa miongozo ya usajili ikiwemo uteuzi wa Wasajili katika Halmashauri na namna vyombo vitakavyoendeshwa; kuongeza idadi ya wataalam kwenye miradi; na kutoa mafunzo kwa wasimamizi wa skimu za miradi. Vilevile, Wizara imeandaa Mkakati wa Uendelevu wa Miradi ya Maji Vijijini (*National Rural Water Supply Sustainability Strategy*) ambao utekelezaji wake utaanza katika mwaka wa fedha 2015/2016.

**128. Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Aprili, 2015, idadi ya vyombo vya watumiaji maji vilivyojiliwa kisheria imefikia **909** kutoka vyombo **373** mwezi Juni, 2014. Katika mwaka 2015/2016, Serikali itaendelea kutoa mafunzo kwa viongozi wa vyombo hivyo, kuhimiza uundwaji zaidi wa vyombo vya watumiaji maji na kusitiza wasajili kuongeza kasi ya usajili kwa miradi iliyopo na mingine itakayojengwa. Vilevile, Halmashauri zinatakiwa ziandae mipango kazi ya kutoa elimu kwa wananchi. Elimu hiyo inahusu usajili wa vyombo hivyo na uwasilishaji wa taarifa ya utekelezaji wa mipango hiyo kila robo mwaka.

### **3.3 HUDUMA YA MAJI MIJINI**

**129. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu iliendelea kutekeleza Programu ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini kwa kujenga, kupanua na kukarabati mifumo ya majisafi na uondoaji majitaka pamoja na kuzijengea uwezo Mamlaka zote za maji za Miji Mikuu ya Mikoa na Jiji la Dar es Salaam; Miji Mikuu ya Wilaya; Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa. Lengo ni kuwapatia wananchi wengi zaidi huduma ya maji safi na salama pamoja na huduma ya usafi wa mazingira katika maeneo yao. Vilevile, katika kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji kuititia mfumo wa "Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa" (BRM), nimesaini mikataba ya matarajio ya kazi na viashiria vya utendaji (*Key Performance Indicators – KPIs*) na kila Mwenyekiti na Mtendaji Mkuu wa Mamlaka za Majisafi za Miji Mikuu ya Mikoa yote likiwemo Jiji la Dar es Salaam na Miradi ya Kitaifa ili kupima ufanisi wa utoaji wa huduma katika maeneo yao.

#### **3.3.1 Kuboresha Huduma za Maji Mijini**

##### **(a) Miradi ya Maji katika Miji Saba**

**130. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Serikali iliendelea kutekeleza miradi ya kukidhi mahitaji ya huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika miji **saba** ya **Bukoba, Musoma, Lindi, Kigoma, Sumbawanga, Mtwara** na **Babati**. Utekelezaji huo unashirikisha Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD), Serikali ya Ujerumani kuititia Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KfW) na Umoja wa Ulaya.

### **(i) Manispaa za Musoma na Bukoba**

**131. Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa miradi ya majisafi kwa Manispaa za Musoma na Bukoba, unatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (*AFD*). Utekelezaji huo unahusu ujenzi wa mitambo ya kusafisha na kusukuma maji pamoja na ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji katika miji hiyo.

**132. Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Aprili, 2015 utekelezaji wa mradi wa Bukoba unaogharimu **shilingi bilioni 27.54** umefikia **asilimia 85**. Aidha, kwa upande wa Manispaa ya Musoma, mradi huo unagharimu **shilingi bilioni 40.62** na utekelezaji wake umefikia **asilimia 80**. Mnamo tarehe 22/03/2015, **Mhe. Dkt. Mohamed Gharib Bilal**, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliweka jiwe la msingi kwenye Mradi wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Musoma. Miradi hiyo inatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2015.

### **(ii) Manispaa za Lindi, Kigoma na Sumbawanga**

**133. Mheshimiwa Spika**, kwa Manispaa za **Lindi, Kigoma na Sumbawanga**, ujenzi wa miradi ya maji na usafi wa mazingira inatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani na Umoja wa Ulaya. Ujenzi wa miradi hiyo unagharimu kiasi cha **Euro milioni 62.59** na unahusu uchimbaji wa visima; ujenzi wa mabanio, chujio, matanki na vituo vya kuchotea maji; ulazaji wa bomba kuu na mabomba ya usambazaji maji.

### ***Manispaa ya Lindi***

**134. Mheshimiwa Spika**, Serikali katika kuboresha huduma za maji Lindi Mjini ilitekeleza kazi za muda wa kati kwa kukarabati na kupanua miundombinu ya maji ya katika Manispaa hiyo kwa gharama ya **shilingi bilioni 4.7**. Kazi zilizotekeliza na kukamilika ni pamoja na ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji ya umbali wa **kilomita 47**; ujenzi wa tanki lenye ujazo wa **lita 680,000**; uunganishaji wa umeme kwenye vyanzo vya visima virefu vya Kitunda umbali wa **kilomita 25**; kufunga booster pumps **mbili** katika kituo cha kusukuma maji cha *Kawawa Road*; na ufungaji wa dira za maji **2,030**. Mradi huo ulizinduliwa na **Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakati wa Maadhimisho ya Wiki ya Maji Kitaifa tarehe 23/3/2013. Kukamilika kwa mradi huo kumeongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita 1,163,000** hadi **lita 2,400,000** kwa siku.

**135. Mheshimiwa Spika**, katika mipango ya muda mrefu, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani na Umoja wa Ulaya inatekeleza mradi wa ujenzi wa miundombinu ya majisafi katika Manispaa ya Lindi kwa gharama ya **Euro Milioni 11.91**. Kazi zinazotekeliza ni pamoja na uchimbaji wa **visima virefu 10**; ujenzi wa chujio la maji; ujenzi wa matanki **mawili** ya maji ya **ujazo wa lita milioni 3** na **milioni 2**; ulazaji wa

bomba kuu la maji umbali wa **kilomita 11.5**; mabomba ya kusambaza maji umbali wa **kilomita 27**; ujenzi wa **vituo 85** vya kuchotea maji; ujenzi wa mabwawa **mawili** ya kutibu majitaka; na ununuzi wa gari la uondoshaji wa majitaka. Hadi mwezi Aprili 2015, uchimbaji wa visima umekamilika na utekelezaji wa mradi kwa ujumla umefikia **asilimia 48**. Mradi huo utakamilika mwezi Novemba, 2015 na utaongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 2.4** kwa siku hadi **lita milioni 7.1** kwa siku.

#### **Manispaa ya Kigoma**

**136. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani na Umoja wa Ulaya inatekeleza mradi wa ujenzi wa miundombinu ya majisafi katika Manispaa ya Kigoma kwa gharama ya **Euro Milioni 15.16**. Kazi zinazotekelizwa ni pamoja na ujenzi wa kichoteo cha maji; ujenzi wa kituo cha kusukumia maji; ujenzi wa matanki **sita** ya maji ya ujazo wa **lita milioni 2** kila moja na tanki moja la ujazo wa **lita 500,000**; ulazaji wa bomba kuu umbali wa **kilomita 16.9** na mabomba ya kusambaza maji umbali wa **kilomita 122.8**; ujenzi wa vituo **200** vya kuchotea maji; ujenzi wa mabwawa **mawili** ya kutibu majitaka; na ununuzi wa gari la uondoshaji wa majitaka. Hadi mwezi Aprili 2015, utekelezaji wa kazi hizo umefikia **asilimia 31**. Mradi huo utakamilika mwezi Novemba, 2015 na utaongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 12** kwa siku hadi **lita milioni 26** kwa siku na kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wakazi wa Manispaa ya Kigoma/Ujiji hadi mwaka 2020.

#### **Manispaa ya Sumbawanga**

**137. Mheshimiwa Spika**, Serikali ilitekeleza mradi wa upanuzi wa miundombinu ya maji katika Manispaa ya Sumbawanga (*immediate works*) kwa gharama ya **shilingi bilioni 5.31**. Kazi zilizotekelizwa ni pamoja na ukarabati wa mabomba ya kusambaza maji umbali wa **kilomita 46**; uchimbaji wa visima virefu **vinane** vyenye uwezo wa kuzalisha **lita milioni 4** kwa siku; ulazaji wa bomba kuu la umbali wa **kilomita 9**; kununua na kufunga pampu **nne** na kuunganisha umeme kwenye chanzo pamoja na ujenzi wa *collector tank* la ujazo wa **lita 500,000**. Kazi hizo zilikamilika na kuongeza upatikanaji maji kutoka **asilimia 62** hadi **asilimia 70** ya wakazi wa Manispaa ya Sumbawanga.

**138. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani na Umoja wa Ulaya, kwa sasa inatekeleza mradi wa ujenzi wa miundombinu ya majisafi katika Manispaa ya Sumbawanga kwa gharama ya **Euro Milioni 14.99**. Kazi zinazotekelizwa ni pamoja na kuchimba visima virefu **17** na kufunga pampu; kulaza bomba kuu umbali wa **kilomita 16**; ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji umbali wa **kilomita 68**; kujenga *booster station mbili*; ujenzi wa mtambo wa kusafisha na kutibu maji; ujenzi wa matanki **sita** ya maji yenye ujazo wa jumla ya **lita milioni 7**; upanuzi wa mtambo wa kusafisha maji kwa kujenga chujio; ujenzi wa vituo **56** vya kuchotea maji; kujenga mabwawa **mawili** ya kutibu majitaka na kununua magari **matatu** ya uondoshaji wa majitaka. Utekelezaji wa kazi hizo upo kwenye hatua mbalimbali na kwa ujumla utekelezaji umefikia **asilimia 43**. Mradi ukikamilika, utaongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 5.4** kwa siku kwa sasa hadi **lita milioni 19** kwa siku.

### **(iii) Manispaa za Mtwara na Babati**

**139. Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa mradi wa majisafi na usafi wa mazingira katika Miji ya **Mtwara** na **Babati** unatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani chini ya Programu ya *Millennium Development Goals Initiative (MDGI-EU)*. Jumla ya **Euro milioni 8.72** zilitengwa na Serikali ya Ujerumani kupitia KfW kwa ajili ya utekelezaji wa mradi katika miji hiyo. Wizara yangu iliajiri Mtaalam Mshauri kwa ajili ya kupitia taarifa ya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali pamoja na kuainisha kazi zitakazotekelawa kulingana na kiasi hicho cha fedha. Kwa sasa Mtaalam huyo anakamilisha mapitio ya usanifu na utayarishaji wa makabrasha ya zabuni. Kazi hiyo itakamilika mwezi Juni, 2015 na ujenzi unatarajiwa kuanza mwezi Oktoba, 2015.

#### **(b) Miradi ya Maji ya Kukidhi Mahitaji ya Muda Mrefu**

##### **(i) Mradi wa Maji Tabora**

**140. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Uswisi kupitia Shirika lake la Maendeleo (SECO) imekamilisha mradi wa ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya maji katika Manispaa ya Tabora. Mradi huo uligharimu **Dola za Marekani milioni 4.84** na kazi zilizotekelawa ni pamoja na ukarabati wa mtandao wa maji mjini Tabora kwa **kilomita 27**; ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa **kilomita 2.7**; ununuzi wa pampu **mbili** za kusukuma maji pamoja na transfoma **mbili**; ujenzi wa matanki **matatu** yenyewe ujazo wa **lita 750,000** kila moja; ununuzi wa dira za maji **5,000**; upanuzi wa chanzo; na kujenga kituo cha kutibu maji (*post chlorination*). Kukamilika kwa mradi huo kumeongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 9.6** hadi **lita milioni 15** na kuwanufaisha wakazi **171,526** wa Manispaa ya Tabora.

**141. Mheshimiwa Spika**, vilevile, Serikali kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji inaendelea kutekeleza mradi wa ukarabati na upanuzi wa chujio la maji katika kituo cha Igombe Mjini Tabora, unaogharimu **Dola za Marekani milioni 4.74**. Mradi huo unalenga kuzalisha **lita milioni 30** kwa siku na utakapokamilika utawapatia huduma ya maji ya kutosheleza mahitaji ya wakazi wa Manispaa ya Tabora hadi kufikia mwaka 2032. Uzalishaji kwa sasa ni **lita milioni 15** na mahitaji halisi ya sasa ni **lita milioni 24.5** kwa siku. Kazi zinazoendelea kutekelezwa ni pamoja na kufunga pampu kubwa **tatu**; na kulaza bomba lenye urefu wa **mita 240** na kipenyo cha **milimita 400** kutoka bwawani hadi kwenye machujio. Hadi mwezi Aprili 2015, ujenzi wa mradi huo umefikia **asilimia 40** na utakamilika mwezi Agosti, 2015.

##### **(ii) Mradi wa Maji Mjini Dodoma**

**142. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu iliendelea kutekeleza mradi wa kuboresha huduma ya majisafi na uondoaji wa majitaka katika Chuo Kikuu cha Dodoma unaogharimu **shilingi bilioni 27.7**. Kazi zinazoendelea kutekelezwa ni pamoja na ujenzi wa matanki makubwa **matatu** yenyewe jumla ya **lita**

**milioni 12** ya kuhifadhi maji katika maeneo ya Chimwaga **lita milioni 4.5**, Luangu (**lita milioni 4.5**) na *Informatics* (**lita milioni 3**); na kulaza mabomba makubwa yenyе urefu wa **kilomita 12.2** na mabomba ya kusambaza maji urefu wa **kilomita 9.6**. Vilevile, ujenzi utaendelea katika kituo cha kusukuma maji eneo la Makulu na uunganishaji wa umeme; kujenga mtandao wa majitaka wenye urefu wa **kilomita 18.05** kwa bomba kuu na **kilomita 8** za mabomba ya kukusanya majitaka; pamoja na ujenzi wa mabwawa ya kutibu majitaka katika eneo la wastani wa **hekta 108**.

**143. Mheshimiwa Spika**, mradi huo uliwekwa jiwe la msingi tarehe 22/03/2014 na **Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda**, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania siku ya kilele cha Maadhimisho ya Wiki ya Maji. Hadi mwezi Aprili 2015, utekelezaji wa kazi hizo umefikia **asilimia 94** na mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2015. Mradi huo utakapokamilika, jumla ya wakazi **100,000** kwenye maeneo ya mradi watapata huduma bora ya majisafi na uondoaji wa majitaka na hivyo, kuondoa kero ya upatikanaji wa huduma hizo.

**144. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Korea Kusini inatekeleza mradi wa uboreshaji wa huduma ya majisafi katika Mji wa Dodoma kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 49.62**. Kazi zinazotekelze wa ni pamoja na uchimbaji wa visima **vitatu** na ukarabati wa visima **21** katika eneo la Mzakwe. Kazi hizo zitakapokamilika uwezo wa kuzalisha na kusafirisha maji utaongezeka kutoka **lita milioni 32** kwa siku za sasa hadi kufikia **lita milioni 61.5** kwa siku. Hadi mwezi Aprili 2015, jumla ya visima **17** vimekarabatiwa na uchimbaji wa visima **viwili** umekamilika.

**145. Mheshimiwa Spika**, kazi nyingine zinazotekelze wa ni ujenzi wa mtandao wenye urefu wa **kilomita 6.5**; ujenzi wa barabara ya urefu wa **kilomita 5** kwenda kwenye visima; ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa **kilomita 31.2** kutoka Mzakwe hadi Mjini Dodoma ambapo jumla ya **kilomita 22.2** zimekamilika; ujenzi wa tanki eneo la Itega lenye uwezo wa **lita milioni 7** na eneo la Itega lenye uwezo wa **lita milioni 5.5**; ukarabati wa mitambo ya kusukuma maji; ujenzi wa *booster station* eneo la Mailimbili; ununuzi wa mitambo/vifaa vya kisasa vya kutibu maji; na kujenga maabara ya kisasa ya kupima ubora wa majisafi na majitaka. Utekelezaji wa mradi kwa ujumla umefikia **asilimia 95** na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2015. Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wakazi wa Mjini Dodoma kutoka **asilimia 87** hadi **asilimia 95**. Mradi huo uliwekewa jiwe la msingi na **Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 01/09/2014 katika eneo la tanki la Itega.

### (iii) **Mradi wa Maji Jijini Arusha**

**146. Mheshimiwa Spika**, mradi wa maji wa Moshono Jijini Arusha, umelenga kuboresha huduma ya maji kwa wakazi wa Kata za Moshono na Engutoto ambao idadi yao ni **28,124**. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni uchimbaji wa kisima kirefu ambacho ujenzi wake umekamilika. Kazi nyingine ni uboreshaji wa chanzo cha maji ya chemichemi ya Machare; ujenzi wa tanki lenye uwezo wa kuhifadhi maji **lita milioni 2.5**;

kulaza bomba kuu la kupeleka maji kutoka kwenye kisima hadi kwenye tanki; na kulaza mabomba ya kusambaza maji kwenye mitaa yote ya Kata ya Moshono. Kazi hizo hazikufanyika kutokana na wananchi wanaolima ndani ya eneo la chanzo cha maji Machare kugoma kupisha uboreshaji wa chanzo na ujenzi wa tanki kwenye eneo la Kilima lenye upana wa **mita 35** na urefu **mita 35**. Katika kutafuta ufumbuzi wa suala hilo, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Arusha inaendelea kujadili suala hilo na viongozi wa ngazi ya Kata hadi Mkoa pamoja na kutumia Sheria zilizopo ili kuweza kutatua tatizo hilo na mradi uweze kutekelezwa. Katika mwaka 2015/2016, Serikali imetenga kiasi cha shilingi **bilioni 2.78** ili kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Jiji la Arusha.

**147. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na AfDB imepanga kuboresha huduma ya upatikanaji wa majisafi na usafi wa mazingira katika Jiji la Arusha. Mradi huo utagharimu **Dola za Marekani milioni 218**. Kazi zitakazotekelawa ni pamoja na ujenzi wa chanzo cha maji ya Mto Malala; Uchimbaji wa visima virefu vipatavyo **18**; ujenzi wa mtambo wa kutibu maji; ulazaji wa bomba za kusambaza maji umbali wa **kilomita 200**; ujenzi wa matanki **17** ya kuhifadhia maji ya ujazo tofauti; ukarabati na upanuzi wa mfumo wa majitaka; ujenzi wa mabwawa **14** mapya ya kutibu majitaka; ujenzi wa maabara ya maji; na kujenga uwezo wa taasisi na watumishi. Mradi huo unatarajiwu kuanza kutekelezwa katika mwaka 2015/2016 na kukamilika mwaka 2020. Kukamilika kwa mradi huo kutaboresha huduma ya maji katika Jiji la Arusha kwa kuongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 46.87** kwa siku hadi **lita milioni 86.24** kwa siku, sawa na ongezeko la **asilimia 86**. Aidha, huduma ya uondoaji majitaka itaboreshwa kutoka **asilimia 7.6** ya eneo la Jiji kwa sasa hadi **asilimia 30**.

#### (iv) Mradi wa Maji Mjini Singida

**148. Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa mradi wa uboreshaji wa miundombinu ya majisafi katika Mji wa Singida umekamilika na ulikabidhiwa kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Singida tarehe 31/07/2014. Mradi huo umefadhiliwa na Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Kiarabu (BADEA) pamoja na Mfuko wa Maendeleo wa Nchi zinazozalisha Mafuta (*OPEC Fund for International Development-OFID*) kwa gharama ya **shilingi bilioni 32.53**. Ujenzi huo ulihusu uchimbaji wa visima **saba** kati ya hivyo, visima **viwili** maeneo ya Mwankoko na visima **vitano** katika maeneo ya Irao; ujenzi wa matanki **mawili** katika maeneo ya *Airport*; kulaza bomba kuu la maji hadi kwenye matanki; na ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji katika eneo la Mandewa. Hadi mwezi Aprili 2015, kazi za kuunganisha mabomba madogo kwenye bomba kuu katika maeneo ya Unyankindi, Mitunduruni, Itungukia, Minga, Misuna, Kibaoni na Kindai; na uunganishaji wateja **1,000** kwenye mtandao wa maji katika maeneo hayo zimekamilika. Kazi zinazoendelea ni ujenzi wa chemba na ufungaji wa *control valves* kwenye mtandao huo na zitakamilika mwezi Juni, 2015.

#### (v) Mradi wa Maji Morogoro Mjini

**149. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la MCC la Marekani ilikamilisha mradi wa kupanua na kuboresha upatikanaji wa

huduma ya majisafi katika Manispaa ya Morogoro kwa gharama ya **shilingi bilioni 10**. Kazi zilizotekelawa ni pamoja na kukarabati matanki **matatu**; ulazaji wa bomba kuu la maji la urefu wa **kilomita 1.8**; kupanua chujio la maji la Mafiga; na kujenga mtambo wa kusafisha maji wa Mambogo. Mradi huo ulizinduliwa rasmi tarehe 22/08/2014 na **Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kukamilika kwa mradi huo kumeweza kuongezeka kwa wakazi wanaopata huduma ya maji safi na salama kutoka **asilimia 75.4** kabla ya mradi hadi **asilimia 85** kwa sasa.

#### (vi) **Mradi wa Maji Songea Mjini**

**150. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu iliendelea na mradi wa kukarabati chanzo cha Mto Ruhila Mjini Songea kwa kujenga banio la maji (*weir*) ili kukabiliana na upungufu wa maji wakati wa kiangazi. Utekelezaji wa mradi huo unagharimu **shilingi bilioni 2.6** na fedha hizo zinatolewa na Serikali. Utekelezaji wa mradi huo umefikia **asilimia 42** na unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2015 na kuwanufaisha wakazi **164,162** wa Mji wa Songea.

#### (vii) **Huduma ya Maji Mjini Mtwara**

##### **Kuboresha Upatikanaji wa Maji Mjini Mtwara**

**151. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani chini ya Programu ya *Millennium Development Goals Initiative (MDGI-EU)* inatekeleza ujenzi wa mradi wa muda kati (*Intermediate works*) wa kuboresha huduma ya majisafi kwa Mji wa Mtwara. Hadi mwezi Aprili 2015, Mtaalam Mshauri anaendelea kukamilisha mapitio ya usanifu na utayarishaji wa makabrasha ya zabuni, kazi ambayo itakamilika mwezi Juni, 2015 na ujenzi wa mradi utaanza mwezi Agosti, 2015. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2016 na kuongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 9** kwa siku za sasa hadi **lita milioni 14** kwa siku. Vilevile, upatikanaji wa huduma ya maji kwa wakazi wa Mji wa Mtwara utaongezeka kutoka **asilimia 81** kwa sasa hadi **asilimia 90**.

##### **Mradi wa Kutoa Maji Mto Ruvuma Kupeleka Mtwara-Mikindani**

**152. Mheshimiwa Spika**, katika mipango ya muda mrefu ya kuboresha huduma ya maji Mjini Mtwara-Mikindani, Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa kutoa maji kutoka Mto Ruvuma kupeleka Mtwara-Mikindani na vijiji **26** pamoja na vitongoji vitakavyopitiwa na bomba kuu ndani ya kilomita 12. Kazi zitakazotekelawa ni pamoja na ujenzi wa chanzo kutoka Mto Ruvuma, chujio la kutibu maji, nyumba ya mtambo wa kusukuma maji, matanki **26**, tanki kuu la ujazo wa **lita milioni 30** ambalo litajengwa eneo la Mangamba, vituo vya kuchotea maji **234**; na ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji umbali wa **kilomita 63**. Hadi mwezi Aprili 2015, Mtaalam Mshauri amekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali na anaendelea na usanifu wa kina, kuandaa michoro pamoja na makabrasha ya zabuni. Kazi hizo zinatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2015. Aidha, Serikali kuitia Wizara ya Fedha, tayari imewasilisha maombi kwenda Serikali ya China kuitia *China Development Bank* kwa ajili ya kupata fedha za

kutekeleza ujenzi wa mradi huo. Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 9** kwa siku za sasa hadi **lita milioni 120** kwa siku. Ongezeko hilo litatosheleza mahitaji ya watu pamoja na kasi ya viwanda vinavyoendelea kujengwa vikiwemo veya saruji na gesi katika Mji wa Mtwara.

**(c) Mradi wa Maji katika Miji ya Geita, Sengerema na Nansio**

**153. Mheshimiwa Spika**, mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira wa Ziwa Victoria (*LWATSAN II*) unatekelezwa katika Miji ya Geita, Sengerema na Nansio kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 30.4**. Mradi huo unatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*) na unasimamiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza. Kazi zinazotekelawa zimegawanyika katika vipindi nya muda mfupi na muda mrefu. Kazi za muda mfupi zimekamilika. Kazi hizo ni ununuzi wa vifaa kama magari, pipipiki, trekta, tela, magari makubwa na madogo ya majitaka, vifaa nya kukusanya taka ngumu; uchimbaji wa visima vipywa **vitatu**; na kusafisha visima **vitano** nya zamani.

**154. Mheshimiwa Spika**, kazi za muda mrefu zinazoendelea ni kujenga na kuboresha miundombinu ya majisafi, mifumo ya utoaji wa huduma ya usafi wa mazingira na mitaro ya maji ya mvua. Utekelezaji wa kazi hizo katika Miji ya Sengerema, Nansio na Geita ni kama ifuatavyo:-

**(i) Mji wa Sengerema**

**155. Mheshimiwa Spika**, kazi ya ujenzi wa miundombinu ya majisafi na mradi wa usafi wa mazingira ilianza mwezi Oktoba, 2014 kwa gharama ya **shilingi bilioni 20.06**. Kazi zinazotekelawa ni ujenzi wa chanzo kipywa cha Nyamazugo cha kutoa maji kutoka Ziwa Victoria na ujenzi wa matanki **matano** ya kuhifadhi maji kwenye maeneo ya Ibondo (**lita 150,000**); Igogo (**lita milioni 1.5**); Kilabela (**lita 100,000**); Mwabaluhi (**lita 500,000**) na Bukala (**lita 350,000**) na kulaza mabomba yenye umbali wa **kilomita 71.3**. Mradi utakamilika mwezi Februari, 2016 na utaongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 2.34** za sasa kwa siku hadi **lita milioni 6.02** na hivyo kuongeza upatikanaji wa huduma ya majisafi kutoka **asilimia 33** hadi **asilimia 85**. Kwa upande wa mradi wa usafi wa mazingira, kazi zinazotekelawa ni ujenzi wa mabwawa ya kutibu majitaka eneo la lyogelo; kujenga vyoo kwenye shule **tatu** za msingi za Ibondo, Ngweli na Mwabaluhi na kujenga dampo la kisasa kwa ajili ya kutupa taka ngumu eneo la Ibondo.

**(ii) Mji wa Nansio**

**156. Mheshimiwa Spika**, miradi inayotekelawa ni ya kuimarisha huduma ya majisafi na kuboresha usafi wa mazingira. Miradi hiyo ilianza kutekelezwa mwezi Februari, 2015 kwa gharama ya **shilingi bilioni 10.9**. Kazi zinazofanyika kwa upande wa uimarishaji wa huduma ya majisafi ni kujenga chanzo kipywa cha maji kutoka Ziwa Victoria; kujenga kituo cha kusukuma maji chenye uwezo wa kusuma maji **lita 270,000** kwa saa; kujenga kituo cha kutibu maji chenye uwezo wa **lita milioni 6.45** kwa siku; kufunga pampu zenyne uwezo wa kusukuma maji **lita 270,000** kwa saa; kujenga matanki **mawili** katika

maeneo ya Nebuye (**lita 350,000**) na Malegeya (**lita milioni 3**) na kulaza bomba za chuma umbali wa **kilomita 5.6** na mabomba ya usambazaji maji umbali wa **kilomita 14**. Mradi utakamilika mwezi Februari, 2016 na kunufaisha wakazi **60,000** ikilinganishwa na wakazi **30,000** kabla ya mradi. Vilevile, kwa upande wa uboreshaji wa huduma za usafi wa mazingira, kazi zinazotekelizwa ni ujenzi wa mabwawa ya kutibu majitaka eneo la Bukongo yenye uwezo wa **lita 50,000**, kujenga vyoo viwili kwenye shule za msingi za Nansio na Nakoza na kujenga dampo la kisasa la kutupia taka ngumu eneo la Bukongo.

**(iii) Mji wa Geita**

**157. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia programu ya *LV-WATSAN* inatekeleza mradi wa kuboresha huduma ya maji safi na usafi wa mazingira katika Mji wa Geita. Hadi mwezi Aprili 2015, taarifa ya tathmini ya zabuni ya kumpata Mkandarasi imeidhinishwa na *AfDB* tarehe 09/04/2015. Gharama ya mradi ni **shilingi bilioni 6.67**. Mkataba wa ujenzi utasainiwa mwishoni mwa mwezi Mei, 2015 na ujenzi utaanza mwezi Julai, 2015. Kazi zitakazotekelizwa kwa upande wa mradi wa kuboresha upatikanaji wa huduma ya majisafi ni pamoja na uchimbaji wa visima virefu **vitatu**; kufunga pampu; kuvuta umeme kwenye kila kisima; kujenga nyumba ya mtambo wa kusukuma maji kwenye kila kisima; kujenga matanki **manne** ya kuhifadhi maji kwenye maeneo ya Kagera A (**lita 500,000**); Buhalahala (**lita 135,000**); Shule ya Msingi Waja (**lita 135,000**), na Kituo cha Mabasi (**lita 45,000**); na kulaza bomba kuu umbali wa **kilomita 3** na mabomba ya kusambaza maji umbali wa **kilomita 17.5**. Aidha, kwa upande wa mradi wa kuboresha huduma za usafi wa mazingira, kazi zitakazotekelizwa ni kujenga mabwawa ya kutibu majitaka eneo la Usindakwe yenye uwezo wa **lita 50,000**; vyoo **viwili** kwenye Shule za Msingi za Mbugani na Nyankumbu; na dampo la kisasa la kutupa taka ngumu eneo la Usindakwe.

**(d) Mradi wa Maji Geita kutoka Ziwa Victoria:- Uwekezaji wa Serikali na Mgodi wa Dhahabu wa Geita (GGML)**

**158. Mheshimiwa Spika**, Hati ya Makubaliano (*Limited Distribution Network Agreement*) ya kuanza kutekeleza awamu ya pili ya mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria hadi Mji wa Geita ambao unagharamiwa na Serikali kwa kushirikiana na Mgodi wa Dhahabu wa Geita (*Geita Gold Mining Limited – GGML*) ilisainiwa tarehe 31/05/2014. Mchango wa Serikali ni **Dola za Marekani 400,000** na GGML ni **Dola za Marekani milioni moja**. Mradi huo unahusu ujenzi wa mtandao wa majisafi wenye urefu wa **kilomita 35**; vituo **15** vya kuchotea maji; na magati (*water kiosks*) **matano**. Mkandarasi alianza kazi mwezi Desemba, 2014 na hadi mwezi Aprili 2015, mradi huo umefikia **asilimia 70** ya utekelezaji. Mradi huo utakamilika mwezi Julai, 2015 na utaongeza upatikanaji wa huduma ya maji katika mji wa Geita kutoka **asilimia 12.5** za sasa hadi **asilimia 56**.

**(e) Mradi wa Maji katika Miji ya Muleba, Mutukula na Kamachumu**

**(i) Mji wa Muleba**

**159. Mheshimiwa Spika** Wizara inatekeleza Awamu ya Pili ya miradi ya usambazaji wa maji kwenye maeneo ya Muleba Mjini ambayo hayapati huduma ya maji safi. Maeneo hayo ni Omundangara, Kamanengo *National Housing* (maeneo ya Magereza), Bukono na Bujumbi. Katika mwaka 2015/2016, kazi zitakazotekelawa ni pamoja na uchimbaji wa kisima kirefu, kufunga pampu na ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji yenyе urefu wa **kilomita 21.5**. Kukamilika kwa kazi hiyo kutaongeza uzalishaji wa maji kwa mji wa Muleba kutoka **lita 560,000** kwa siku hadi **lita milioni 1.7**. Kwa sasa mradi unahudumia wakazi **11,563**, ambao kati ya hao wakazi **10,063** ni wa Mji wa Muleba na **1,500** ni wa Vijiji vya Bwata, Kamishango, Kabare na Katanga. Mradi utakapokamilika utawanufaisha zaidi ya wakazi **29,000**.

**(ii) Mji wa Mutukula**

**160. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bukoba imeendela kusimamia kazi za ukarabati wa miundombinu ya maji katika Mji wa Mutukula ili kuhakikisha mji huo unapata huduma ya maji. Kazi zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka huo ni pamoja na:- usafishaji wa visima **viwili** na kuvifanyia majoribio; ufungaji wa umeme kwenye kisima cha Kasharu; kubadilisha bomba kuu kutoka kwenye kisima hadi tanki lenye uwezo wa **lita 900,000**; ununuzi wa vifaa vya umeme kwa ajili ya pampu; na kurekebisha mfumo wa usambazaji maji kutoka kwenye tanki hadi kwenye magati. Hadi mwezi Aprili 2015, usafishaji wa visima **viwili** umekamilika, ufungaji wa umeme unaendelea ambapo nguzo **16** zimejengwa na ufungaji wa nyaya za umeme upo kwenye hatua za mwisho. Mradi huo utakamilika mwezi Juni, 2015.

**(iii) Mji wa Kamachumu**

**161. Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Muleba inatekeleza miradi ya maji katika Mji wa Kamachumu chini ya mpango wa *quickwins*. Usanifu wa mradi huo umekamilika na gharama za ujenzi zinakadiriwa kuwa **shilingi bilioni 1.5**. Kazi zitakazotekelawa ni pamoja na ujenzi wa vyanzo **viwili** vya maji; ulazaji wa bomba la umbali wa **kilomita 27**; ujenzi wa matanki mawili ya kuhifadhi maji ya ujazo wa **lita 135,000** na **lita 90,000**; na ujenzi wa vituo **31** vya kuchotea maji. Halmashauri inaendelea na taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi na mradi utaanza katika mwaka 2015/2016 na utakapokamilika utawanufaisha wakazi wapatao **23,289**.

**(f) Miradi Mipyä katika Eneo la Ziwa Victoria**

**162. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu imeanza utekelezaji wa mradi wa uboreshaji wa huduma ya majisafi katika Jiji la Mwanza na Mji ya Magu, Misungwi na Lamadi pamoja na mradi wa uondoaji wa majitaka katika Mji ya Bukoba na Musoma. Miradi hiyo inatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (*European Investment Bank-EIB*) na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (*French Development Agency-AFD*) kwa gharama ya **Euro milioni 104.5**. Mchango wa Serikali ni **Euro milioni 14.5**, na *EIB* pamoja na *AFD* watachangia jumla

ya **Euro milioni 90**. Mtaalam Mshauri ameanza kazi ya upembuzi yakinifu, usanifu na uandaaji wa makabrasha ya zabuni kwa upande wa mradi wa uboreshaji wa huduma ya majisafi na kazi hizo zitakamilika mwezi Aprili, 2016 na ujenzi utaanza mwaka 2016/2017.

**163. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu iliendelea kutekeleza miradi ya majitaka kwa Mji ya Bukoba na Musoma. Katika Mji wa Bukoba utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa mabwawa ya kusafisha majitaka kuitia Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Ziwa Victoria (*Lake Victoria Environmental Management Project - LVEMP*) umekamilika mwezi Desemba, 2014 kwa gharama ya **shilingi bilioni 2.54**. Kukamilika kwa mradi huo kumeboresha huduma ya uondoaji majitaka katika Mji wa Bukoba. Kazi zinazotekelawa katika Mji wa Musoma zinagharamiwa na Serikali kwa kushirikiana na AFD. Kazi hizo ni pamoja na ujenzi wa mabwawa ya kumwaga majitaka (*sludge digester*) katika eneo la Bweri ambao umefikia **asilimia 70** na utakamilika mwezi Julai 2015. Vilevile, taratibu za ununuzi wa magari **mawili** ya kuondoa majitaka zinaendelea na magari hayo yanatarajiwa kupatikana mwaka 2015/2016.

#### (g) Miradi ya Maji katika Mji ya Ziwa Tanganyika

**164. Mheshimiwa Spika**, Serikali ikishirikiana na nchi za Zambia, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Rwanda zinatekeleza Mradi wa Majisafi na Usafi wa Mazingira katika eneo la Ziwa Tanganyika (*LT-WATSAN*) unaosimamiwa na Shirika la Makazi la Umoja wa Mataifa (*UN-HABITAT*). Mradi huo ulifanyiwa upembuzi yakinifu mwaka 2011 katika Mji ya Kigoma, Kasulu, Mpanda, Namanyere, Uvinza na Kasanga. Kazi zinazotarajiwa kutekeleza ni pamoja na ujenzi wa mitandao ya majisafi na usafi wa mazingira, ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua na uondoaji wa taka ngumu pamoja na kuzijengea uwezo taasisi husika. Hata hivyo, utekelezaji wake haukuanza kutokana na kutopatikana kwa fedha. Serikali inaendelea na jitahada za kutafuta fedha ili kuweza kutekeleza mradi huo na kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika miji hiyo.

**165. Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa mradi wa maji wa Mji wa Kigoma unaotekelawa na Serikali kwa kushirikiana na AfDB kwa gharama ya **Euro 170,000** upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Kazi zinazotekelawa ni pamoja na ujenzi wa tanki la ujazo wa **lita 150,000** ambalo limefikia **asilimia 98**; ununuzi wa mabomba ya umbali wa **kilomita 6**; Kazi zilizokamilika ni ununuzi wa mabomba ya umbali wa **kilomita 1**, dira za maji **692** pamoja na ufungaji wa kifaa cha kudhibiti matumizi ya umeme (*power factor correction*).

#### 3.3.2 Kuboresha Huduma ya Maji katika Mji ya Mpanda, Njombe na Bariadi

**166. Mheshimiwa Spika**, Serikali kuitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, inaendelea kutekeleza miradi ya huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika miji ya Mpanda, Njombe na Bariadi. Miji hiyo ni makao makuu ya Mikoa mipya ya Katavi,

Njombe na Simiyu ambayo hali ya upatikanaji wa huduma na miundombinu ya maji bado ipo chini. Utekelezaji wa miradi ya maji katika miji hiyo ni kama ifuatavyo:-

#### (a) Mji wa Mpanda

**167. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu ilituma **shilingi milioni 550** kwa ajili ya kutekeleza mradi wa maji katika Mji wa Mpanda ili kukabiliana na uhaba wa maji. Kazi zilizokamilika ni ujenzi wa tanki la maji la Kazima lenye uwezo wa **lita milioni moja**; nyumba **mbili** za watumishi na kufunga *solar panel* **nne** katika maeneo ya Kazima na Ikolongo; ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji umbali wa **kilomita 48**; kulaza bomba kuu umbali wa **kilomita 13.6** kwenye eneo la Ikolongo; kununua na kufunga pampu **moja**; na kununua dira za maji **4,000**.

**168. Mheshimiwa Spika**, kukamilika kwa kazi hizo kumeongeza uzalishaji wa maji hadi **lita milioni 5** kwa siku ikilinganishwa na **lita milioni 3.4** kabla ya kutekeleza mradi huo. Vilevile, muda wa upatikanaji wa maji umeongezeka kutoka **saa sita** mara mbili kwa wiki hadi **saa sita** kwa siku. Katika mwaka 2015/2016, Serikali imetenga kiasi cha **shilingi bilioni 4** ili kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Mji wa Mpanda.

**169. Mheshimiwa Spika**, vilevile, Wizara yangu inaendelea na mazungumzo na Kampuni ya Ostap ya nchini Austria ambayo imeonesha nia ya kutekeleza mradi wa kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Mpanda. Hadi sasa Kampuni hiyo imeelekezwa kuwasilisha Andiko la Mradi (*Project Proposal*) pamoja na mpangokazi (*workplan*) kwa ajili ya kupitiwa na kuwasilishwa Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango kwa hatua zaidi.

#### (b) Mji wa Njombe

**170. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara yangu imetuma **shilingi bilioni 1.38** kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa maji katika Mji wa Njombe. Kazi zinazotekeliza ni ujenzi wa chanzo cha Mto Nyenga; ulazaji wa bomba kubwa umbali wa **kilomita 14.3**; ujenzi wa matanki **3** yenye ujazo wa **lita 135,000** kila moja katika maeneo ya Magereza, *Airport* na Nazareti; ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji umbali wa **kilomita 16.58** katika maeneo ya *Airport*, Kambarage, Igeleke na Nzengelendete na ununuza wa dira **1,000**. Hadi mwezi Aprili 2015, mradi huo umefikia **asilimia 81** na utakamilika mwezi Julai, 2015. Mradi huo utakapokamilika hali ya upatikanaji wa huduma ya maji itaongezeka kutoka **asilimia 43** hadi **asilimia 81**. Katika mwaka wa fedha 2015/2016, Serikali imetenga **shilingi bilioni 3** kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Njombe.

### (c) Mji wa Bariadi

171. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu iliendelea kukamilisha miradi ya maji katika Mji wa Bariadi. Kazi zilizokamilika ni uchimbaji wa visima **vitano** na kuweka umeme kwenye visima **vitatu**; kuongeza mtandao wa mabomba umbali wa **kilomita 5.76**; na ujenzi wa tanki lenye ujazo wa **lita 50,000** eneo la Kidinda. Katika mwaka wa fedha 2015/2016, Serikali itaendelea kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa kumalizia kazi za kuunganisha visima vipyta **vitano** kwenye mtandao wa maji; kujenga matanki **mawili** ya maji yenye ujazo wa **lita 135,000** katika eneo la Somanda na **lita 680,000** eneo la Sima. Vilevile, kazi nyingine ni pamoja na kuongeza mtandao wa mabomba umbali wa **kilomita 9.65** katika maeneo ya Sima, Malambo na Somanda; kujenga nyumba ya mtambo wa kusukuma maji na kulaza bomba kuu la kupandisha maji kwenye matanki; ujenzi wa kituo cha kuchotea maji; na kufunga dira za maji kwa wateja **400**. Mradi huo utakapokamilika, utaboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kutoka **asilimia 30** hadi **asilimia 50**. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumanii kuitia KfW imepanga kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Bariadi. Hadi mwezi Aprili 2015, Mtaalam Mshauri anaendelea na kazi ya upembizi yakinifu, usanifu na kuandaa makabrasha ya zabuni na utakamilika mwezi Januari, 2016.

#### 3.3.3 Usanifu wa Miradi ya Maji katika Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo

172. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu imeendelea na kazi za kuajiri Wataalam Washauri ili kufanya upembizi yakinifu, usanifu na kuandaa makabrasha ya zabuni katika Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo. Hadi mwezi Aprili 2015, Mtaalam Mshauri amewasilisha taarifa ya upembizi yakinifu kwa Miji ya Biharamulo, Muleba, Ngara, Karagwe, Chato na Bunazi (Kagera) na anaendelea na usanifu wa kina pamoja na utayarishaji wa makabrasha ya zabuni katika Miji ya Namanyere, Chala, Matai na Laela (Rukwa); Inyonga na Mpanda (Katavi). Mtaalam Mshauri amesaini Mkataba tarehe 19/03/2015 na kazi hizo zitakamilika mwezi Januari, 2016. Kwa upande wa Miji ya Manyoni na Kiomboi mkoani Singida, Mtaalam Mshauri amekamilisha kazi ya usanifu kwa Mji wa Manyoni, na kwa Mji wa Kiomboi usanifu utakamilika mwezi Juni, 2015.

173. **Mheshimiwa Spika**, taratibu za kuwapata Wataalam Washauri kwa ajili ya kufanya kazi ya upembizi yakinifu, usanifu na kuandaa makabrasha ya zabuni zinaendelea kwa Miji ya Mombo, Songe, Lushoto, Kasela, Mkinga, Korogwe na mradi wa kitaifa wa *Handeni Trunk Main - HTM* katika Mkoa wa Tanga; Mji wa Kakonko mkoani Kigoma; mradi wa maji kutoka Mto Ugala hadi Miji ya Urambo na Kaliua (Tabora); Miji ya Mangaka, Ruangwa na Liwale (Lindi); Miji ya Kibaya, Mbulu, Magugu, Galapo, Dareda na Bashnet (Manyara); Miji ya Mahenge, Ifakara, Dakawa na Mikumi (Morogoro); na Miji ya Chamwino, Bahi na Kondoa mkoani Dodoma. Katika mwaka 2015/2016, Wizara yangu itaendelea na juhudii za kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa miradi ya maji kwa miji ambayo usanifu umekamilika.

### **3.3.4 Miradi ya Kutoa Maji kutoka Ziwa Victoria Kupeleka Miji Mbalimbali**

#### **(a) Miji ya Bariadi, Lagangabilili, Mwanhuzi, Sumve na Malya**

**174. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeajiri Mtaalam Mshauri wa kufanya usanifu na uandaaji wa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya mradi wa majisafi kutoka Ziwa Victoria kwenda Miji ya Bariadi, Lagangabilili na Mwanhuzi. Mtaalam Mshauri amewasilisha taarifa ya awali (*Inception report*) mwezi Machi, 2015. Ujenzi wa mradi huo utaanza katika mwaka wa fedha 2015/2016. Mradi huo utakapokamilika utanufaisha wakazi wa miji hiyo pamoja na vijiji **40** vilivyopo umbali wa kilomita 12 kandokando ya bomba kuu kutoka kwenye Ziwa Victoria. Aidha, Wizara imeagiza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza kufanya upembuzi yakinifu ili kubaini chanzo mbadala cha kupeleka maji katika miji midogo ya Sumve na Malya kutoka Magu au Ngudu. Baada ya kazi hiyo kukamilika usanifu wa kina utafanyika na ujenzi kuanza.

#### **(b) Mji wa Ngudu**

**175. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu ilikamilisha mradi wa upanuzi wa mtando wa maji kutoka tanki la Mhalo kwenda Mji wa Ngudu. Mradi huo ulizinduliwa rasmi tarehe 11/10/2014 na **Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kukamilika kwa mradi huo kumewanufaisha wakazi wapatao **36,417** wanaoishi katika Mji wa Ngudu na vitongoji vyake pamoja na wakazi wa vijiji linapopita bomba kuu la maji.

#### **(c) Miji ya Isaka, Kagongwa, Tinde, Kishapu, Kolandoto, Maganzo na Mwadui**

**176. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu iliajiza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama-Shinyanga (*KASHWASA*) kufanya usanifu na kuandaa gharama za utekelezaji wa mradi wa kutoa maji kutoka Ziwa Victoria kupeleka katika Miji ya Isaka, Kagongwa na Tinde. Hadi sasa kazi ya usanifu inaendelea na ujenzi wa mradi huo utatekelezwa na *KASHWASA* chini ya usimamizi wa Wizara kama iliyofanyika kwa mradi wa majisafi wa Wilaya ya Ngudu. Vilevile, *KASHWASA* inaendelea kutekeleza mradi wa kupeleka maji katika Miji ya Kishapu, Kolandoto, Maganzo na Mgodi wa Almasi wa Mwadui. Mradi huo uko katika hatua za awali za ujenzi ambapo uchimbaji wa mtaro na ulazaji wa mabomba unaendelea. Mradi utakapokamilika utawanufaisha wakazi wapatao **58,155** wanaoishi katika miji hiyo pamoja na wakazi wa vijiji vilivyopo pembezoni mwa bomba kuu la maji.

#### **(d) Miji ya Tabora, Igunga, Nzega, Sikonge, Urambo na vijiji vya Wilaya ya Uyui**

**177. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/2016, Serikali itaanza upanuzi wa mradi wa maji wa Ziwa Victoria kutoka katika Kijiji cha Solwa hadi Miji ya Tabora, Igunga, Nzega na vijiji vilivyomo ndani ya kilomita 12 kila upande vinavyopitiwa na bomba kuu. Vilevile, mradi utahudumia baadhi ya vijiji vya Wilaya ya Uyui, Miji ya Sikonge na Urambo. Mradi huo utahusisha ujenzi wa matanki, ulazaji wa mabomba na ukarabati wa mitando ya usambazaji maji katika miji hiyo. Hadi mwezi Aprili, 2015 upembuzi yakinifu

umekamilika. Kwa sasa, Mtaalam Mshauri anakamilisha usanifu wa kina, michoro na uandaaji wa makabrasha ya zabuni. Kiasi cha **Dola za Marekani Milioni 268.35** kimepatikana kutoka Serikali ya India na Mkataba wa Makubaliano ya Kifedha utasainiwa mwezi Juni, 2015, na ujenzi utaanza katika mwaka wa fedha 2015/2016.

### 3.3.5 Miradi katika Jiji la Dar es Salaam

**178. Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu inaendelea kutekeleza miradi ya kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira kwa Jiji la Dar es Salaam, na miji ya Kibaha na Bagamoyo ili kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji safi, salama na ya kutosha. Hadi mwezi Aprili, 2015 miradi inayoendelea kutekelezwa ni kama ifuatavyo:-

#### (a) Ujenzi wa Bwawa la Kidunda

**179. Mheshimiwa Spika,** Mtaalam Mshauri amekamilisha kazi ya tathmini ya athari za kimazingira na kijamii (*ES/A*) ya bwawa na barabara inayounganisha barabara kuu ya Dar-Morogoro na eneo la ujenzi wa bwawa hilo. Tathmini hiyo imewasilishwa Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*) kwa ajili ya uhakiki na kutolewa kibali cha ujenzi. Aidha, taratibu za kuandaa zabuni kwa ajili ya ujenzi wa mradi huo zinatarajiwa kuanza mara baada ya kupata kibali kutoka *NEMC*.

**180. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2014/2015, ulipaji wa fidia kwa ajili ya watakaohamishwa kupisha ujenzi wa bwawa na barabara inayoelekea katika eneo la ujenzi, ulifanyika kati ya mwezi Agosti na Septemba 2014. Jumla ya **shilingi bilioni 7.3** zilitumika kulipa fidia kwa wananchi **2,603**. Hata hivyo, baadhi yao wamelalamikia viwango vya fidia waliyopata. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (*DAWASA*) imeanzisha dawati la kupokea malalamiko. Hadi mwezi Aprili 2015, uhakiki ulifanyika kwa wakazi ambaa wamelipwa fidia. Uhakiki huo ulibaini kuwa fidia kwa wakazi **341** zilikuwa na kasoro. Kwa sasa, Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro inaboresha takwimu za fidia kwa wakazi hao ili watakaostahili waweze kulipwa fidia stahiki. Hivi sasa utaratibu wa kuwagawia viwanja wananchi watakaoothirika na ujenzi wa bwawa unaendelea pamoja na ujenzi wa shule, ofisi ya walimu, ofisi ya kijiji na zahanati umeanza kwa kutumia kampuni ya Jeshi la Wananchi-Mzinga.

**181. Mheshimiwa Spika,** Serikali kuititia *DAWASA* iliingia makubaliano (*MoU*) na Kampuni ya M/s AVIC ya China tarehe 23/6/2014 ya kushirikiana katika kujenga bwawa la Kidunda. Makubaliano hayo yalihusu kutafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza mradi wa ujenzi wa bwawa la Kidunda na tukio la uwekaji saini makubaliano hayo lilishuhudiwa na Makamu wa Rais wa China wakati wa ziara yake hapa nchini. Mradi wa ujenzi wa Bwawa la Kidunda utahusu pia ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme cha **megawati 20**, njia ya kusafirisha umeme kutoka Kidunda hadi Chalinze na barabara yenye **kilomita 75** kutoka Ngerengere hadi Kidunda. Serikali inaendelea na majadiliano na Serikali ya Watu wa China ili kupata fedha za kutekeleza mradi huo ambaa unakadirwa kugharimu **shilingi bilioni 473**.

**(b) Visima Virefu vya Kimbiji na Mpera**

**182. Mheshimiwa Spika**, kazi ya uchimbaji wa visima virefu **20** vya uzalishaji maji vya Kimbiji na Mpera ilipangwa kukamilika mwezi Novemba, 2014. Hata hivyo, kazi hiyo ilichelewa kukamilika kutokana na kuchelewa kuwasili kwa mabomba ya kujengea visima (*casings and screens*) kutoka nje ya nchi. Wizara yangu kupitia DAWASA ilimwandikia Mkandarasi kuhusu uamuzi wa kumtoza gharama za kuchelewesha mradi (*liquidated damages*) kuanzia tarehe 3/11/2014. Hadi mwezi Aprili 2015, Mkandarasi amekamilisha kuchimba visima **vinne**. Mradi huo utakamilika mwezi Desemba, 2015 na utahudumia wakazi wa maeneo ya Mkuranga, Kongowe, Chanika, Ukonga, Pugu, Kinyerezi, Mbagala, Kigamboni, Kurasini, Mtoni na Kisarawe.

**183. Mheshimiwa Spika**, aidha, Mkandarasi wa kuchimba visima **vinane** vya uchunguzi wa mwenendo wa maji chini ya ardhi amekamilisha uchimbaji wa visima **saba** kati ya **vinane** vilivyopangwa kuchimbwa katika maeneo ya Mwasonga, Mkuranga, Kibada, Buyuni, Changani, Chanika na Nzasa-Chanika. Mradi huo utakamilika mwezi Juni, 2015.

**(c) Upanuzi wa Mtambo wa Ruvu Juu na Ulazaji wa Bomba Kuu kutoka Mlandizi hadi Kimara**

**184. Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu inatekeleza mradi wa upanuzi wa mtambo wa Ruvu Juu na ulazaji wa bomba kuu kutoka Mlandizi hadi Kimara. Hadi mwezi Aprili 2015, ujenzi wa upanuzi wa Mtambo wa Ruvu Juu unaogharimu **Dola za Marekani milioni 39.7** umefikia **asilimia 70** na utakamilika mwezi Agosti, 2015. Kukamilika kwa upanuzi wa mtambo huo, kutaongeza uwezo wa kuzalisha maji kutoka **lita milioni 82** kwa siku hadi **lita milioni 196** kwa siku. Aidha, mradi wa ujenzi wa bomba kuu kutoka Mlandizi hadi Kimara unaogharimu **Dola za Marekani milioni 59.3**, umefikia **asilimia 45** ya utekelezaji wake na utakamilika mwezi Septemba, 2015. Kukamilika kwa ujenzi huo kutapunguza kero ya uhaba wa maji katika Miji ya Mlandizi na Kibaha pamoja na maeneo ya Kiluvya, Kibamba, Changanyikeni, Mbezi, Kimara, Kibangu, Makuburi, Tabata, Segerea, Vingunguti, *Airport*, Ukonga na Kipawa katika Jiji la Dar es Salaam ambayo yana uhaba mkubwa wa maji.

**(d) Upanuzi wa Mradi wa Maji Ruvu Chini**

**185. Mheshimiwa Spika**, kukamilika kwa mradi wa upanuzi wa chanzo cha maji cha Ruvu Chini na mtambo wa kusafisha maji (*Treatment Plant*) kumeongeza uwezo wa mtambo wa kuzalisha maji kutoka **lita milioni 180** hadi **lita milioni 270** kwa siku. Kazi inayoendelea ni ulazaji wa bomba kuu umbali wa **kilomita 55.93** ambapo hadi mwezi Aprili, 2015 ulazaji wa bomba hilo umekamilika kwa **kilomita 53**. Utekelezaji wa mradi kwa ujumla umefikia **asilimia 97**. Mradi huo umechelewa kukamilika kutokana na vikwazo katika njia ya bomba kama vile nyaya za mawasiliano, nguzo za umeme na kesi zilizopo mahakamani zinazowahusu waliojenga juu ya bomba. Mradi huo utakamilika mwezi Juni, 2015 na kupunguza kero ya maji kwa wakazi wote wanaotumia

maji kutoka wa Ruvu Chini unaohusisha maeneo ya Bagamoyo na vitongoji vyake, Bunju, Mabwepande, Boko, Tegeta, Kunduchi, Mbezi Beach, Mbezi Juu, Salasala, Kawe, Makongo, Chuo Kikuu, Mikocheni, Msasani, Masaki, Mwananyamala, Kinondoni, Magomeni, Sinza, Manzese, Ubungo, Mabibo, Kigogo, Buguruni, Ilala, maeneo yote ya katikati ya jiji la Dar es Salaam pamoja na Kurasini na Bandarini. Aidha, Serikali imekamilisha ukarabati wa matanki ya kuhifadhi maji yaliyopo Chuo Kikuu cha Ardhi. Kukamilika kwa miradi ya Ruvu Juu na Ruvu Chini kutawezesha maeneo yote ambayo yana mabomba ya kusambaza maji, maarufu kama “**mabomba ya mchina**” ambayo hayapati maji, kuanza kutoa maji.

#### **(e) Ukarabati na Upanuzi wa Mfumo wa Kusambaza Majisafi**

**186. Mheshimiwa Spika**, Serikali ilimwajiri Mtaalam Mshauri kwa ajili ya kufanya usanifu wa mradi wa kusambaza maji na kuunganisha wateja kwenye maeneo kutoka Mbezi hadi Kiluvya; na Tegeta hadi Bagamoyo. Usanifu huo ulikamilika katika mwaka 2013/2014. Kutokana na gharama kubwa ya mradi iliyoainishwa katika taarifa ya usanifu, Wizara yangu ilimwelekeza Mtaalam Mshauri huyo kupitia upya makadirio ya mradi kwa lengo la kupunguza gharama ili iwiane na bajeti iliyopo. Mtaalam Mshauri aliwasilisha rasimu ya pili ya makabrasha ya zabuni mwezi Januari, 2015 ambayo yalitumika kutangaza zabuni ya ujenzi. Zabuni zilipokelewa tarehe 6/5/2015 na uchambuzi unaendelea. Mradi utatekelezwa katika mwaka wa fedha 2015/2016. Aidha, Wizara yangu inamtafuta Mtaalam Mshauri kwa ajili ya kufanya usanifu wa mabomba ya usambazaji maji kwenye maeneo mengine ya Jiji ambayo hayana mfumo wa kusambaza maji kwa sasa. Majadiliano ya kimkataba yanaendelea, matarajio ni kuanza kazi ya usanifu mwezi Julai, 2015.

**187. Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa Jiji la Dar es Salaam, Wizara yangu kupitia *DAWASA* iliingia makubaliano (*MoU*) na Kampuni ya *Power China Kunming* kwa madhumuni ya kutafuta fedha kutoka Benki ya *Exim* ya nchini China. Fedha hizo ni kwa ajili ya kutekeleza mradi wa kulaza mabomba ya kusambaza maji katika Jiji la Dar es Salaam. Kampuni ya *Power China Kunming* ilianza kazi ya upembuzi yakinifu ya mradi huo; na hadi mwezi Aprili 2015, Kampuni hiyo imewasilisha rasimu ya pili ya upembuzi yakinifu na mradi huo unatarajiwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2015/2016 kwa gharama ya **shilingi bilioni 316**.

#### **(f) Kuboresha Mfumo wa Uondoaji Majitaka**

**188. Mheshimiwa Spika**, Serikali inatekeleza mradi wa uondoaji wa majitaka katika Jiji la Dar es salaam ili kuongeza upatikanaji wa huduma hiyo kutoka **asilimia 10** ya wakazi kwa sasa kufikia **asilimia 30** ifikapo mwaka 2017. Utaratibu wa kupata Mtaalam Mshauri atakayesanifu mradi huo umekamilika na mkataba utasainiwa mwezi Juni, 2015. Kwa sasa Serikali inaendelea na majadiliano na Washirika wa Maendeleo walioonesha nia ya kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo. Vilevile, Serikali ilisaini Makubaliano ya Kisera (*Policy Dialogue*) na Serikali ya Korea Kusini tarehe 05/03/2015 ambapo Serikali ya Korea Kusini imekubali kutoa **Dola za Marekani milioni 89**, sawa na **shilingi bilioni 160.2** kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa mradi huo. Makubaliano ya awali ya mpango wa utekelezaji wa Mkataba wa Kifedha (*Financial Agreement*) yalisainiwa tarehe 25/03/2015.

Aidha, Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Korea Kusini pamoja na Benki ya Dunia itatekeleza mradi wa uondoshaji majitaka pamoja na ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya uondoaji wa maji ya mvua katika Jiji la Dar es salaam. Hatua za majadiliano zinaendelea kati ya Serikali na taasisi nyingine zinazohusika na ujenzi wa miundombinu ya barabara pamoja na Manispaa zote za Jiji la Dar es Salaam. Vikao vya majadiliano vinaendelea baina ya wataalam kutoka taasisi husika ikiwa ni pamoja

na Wizara ya Maji, OWM-TAMISEMI, DAWASA, DAWASCO, Mradi wa *DART*, TANROADS na Manispaa zote za Mkoa wa Dar es Salaam. Lengo la vikao hivyo ni kupitia na kuoanisha michoro ya ujenzi wa miundombinu ya majitaka na uondoaji maji ya mvua katika Jiji la Dar es Salaam.

**189. Mheshimiwa Spika**, mradi unatarajiwa kuanza kutekelezwa mwaka 2016, na kazi zitakazofanyika ni pamoja na upanuzi wa mfumo wa majitaka katika maeneo ya katikati ya Jiji; na ujenzi wa mifumo mipyä ya majitaka maeneo ya Ilala, Magomeni hadi Ubungo, Sinza, Kinondoni, Mwananyamala, Oysterbay, Masaki, Msasani, Kawe, *Mbezi Beach*, Kurasini, Keko, Chang'ombe na Temeke. Vilevile, mradi huo utahusu ujenzi wa mitambo **mitatu** ya kisasa ya kusafisha majitaka katika maeneo ya Jangwani, Kurasini na *Mbezi Beach*.

#### **(g) Miradi Mingine ya Maji Jijini Dar es Salaam**

**190. Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam, Wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ubelgiji (*BTC*) na Umoja wa Nchi za Ulaya imekamilisha miradi **sita** iliyobaki kati ya miradi **15** iliyopangwa kutekelezwa ya kujenga mifumo ya usambazaji maji katika maeneo hayo. Kazi zilizotekelzwa ni uchimbaji wa visima, ujenzi wa matanki na vituo vyaya kuchotea maji katika maeneo ya Tabata Darajani, Minazi Mirefu, Kinyerezi, Mwanamtoti, Yombo Dovya-Msakala na Tandale. **Majedwali Na. 9a, 9b na 9c** yanaonesha utekelezaji wa miradi **15** katika maeneo mbalimbali katika Wilaya za Jiji la Dar es Salaam.

**191. Mheshimiwa Spika**, vilevile katika kupunguza kero ya maji kwa wakazi wa Jiji la Dar es Salaam na vitongoji vyake, hadi mwezi Aprili 2015, DAWASA imechimba visima **49** katika maeneo mbalimbali ya Jiji. Kati ya visima hivyo, visima **23** vimekamilika na kuanza kutumika. Visima vilivyokamilika ni pamoja na visima **saba** vilivyopo Kimara katika maeneo ya Mavurunza A, Kilungule A, Kilungule B, King'ongo I, King'ongo III, Saranga I na Saranga II; visima **vitano** vipo Keko/Chang'ombe katika maeneo ya Keko-Magurumbasi, Keko-Mwanga, Chang'ombe A, Unubini na Chang'ombe-Toroli; visima **vitatu** vipo Sandali katika maeneo ya Sandali, Mpogo na Mwembeladu; visima **vitatu** vipo Mburahati maeneo ya *National Housing*, Shebe na Shule ya Msingi Muungano; visima **viwili** katika maeneo ya Mwaninga-Kigamboni na Kisarawe II; na visima **vitatu** katika maeneo ya Kipunguni, *FFU* na Mongo la Ndege yaliyoko Ukonga. Vilevile, ukamilishaji wa ujenzi wa visima **tisa** unaendelea katika maeneo ya Kisarawe visima **vinne**, Segerea visima **vitatu**, Chanika kisima **kimoja** na Mbagala Mwembe Pacha kisima **kimoja**. Visima vilivyobaki vimebainika kuwa na maji kidogo na vingine kuwa na kiwango kikubwa cha chumvi.

#### **(h) Mradi wa Maji wa Mloganzila-Chuo Kikuu cha Afya Muhimbili**

**192. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu imekamilisha ujenzi wa mradi wa maji ya bomba kwenda eneo la hospitali mipyä ya Chuo Kikuu cha Afya Muhimbili inayojengwa Mloganzila. Wizara imenunua na kufunga *booster pump*,

kulaza bomba kutoka Kibamba mpaka Mloganzila urefu wa **kilomita 3.5**, kukarabati *sump well* ya ujazo wa **lita 20,000**, kujenga mnara wa tanki la **lita 10,000** na kuweka transfoma mpya. Mradi huo umefanyiwa majoribio na maji yameweza kufika kwenye tanki lililopo eneo la Chuo Kikuu cha Muhimbili-Mloganzila. Kwa sasa mradi unafanya kazi.

### **3.3.6 Huduma ya Maji katika Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa**

#### **(a) Miji ya Kilosa, Turiani, Mahenge, Mvomero na Gairo**

**193. Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Aprili 2015, utekelezaji wa miradi ya maji katika Miji ya Kilosa imefikia **asilimia 80**, Turiani (77), Mahenge (77), Mvomero (81) na Gairo (86). Miradi hiyo ilisimama kutekelezwa kutokana na kuchelewa kwa upatikanaji wa fedha za kulipa madeni ya Wakandarasi na hivyo kusababisha waondoke kwenye maeneo ya miradi. Wizara yangu imefanya majadiliano na Wakandarasi ili warudi katika maeneo ya kazi. Majadiliano hayo yamefanikiwa na Wakandarasi hao wamekubali kuendelea na kazi. Katika mwaka 2015/2016, Wizara yangu itakamilisha ujenzi wa miradi katika miji hiyo.

#### **(b) Mji wa Bunda**

**194. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu iliendelea kutekeleza mradi wa maji katika Mji wa Bunda. Mradi huo uliwekewa jiwe la msingi na **Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda**, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 20/03/2015 wakati wa Maadhisho ya Wiki ya Maji Mkoani Mara. Kazi zinazoendelea kwa sasa ni kukamilisha ulazaji wa bomba umbali wa **kilomita 25.4** ambapo kwa sasa umefikia **asilimia 98**; ujenzi wa kichoteo ambao umefikia **asilimia 65**; bomba la maji kutoka Ziwani ambalo limejengwa kwa **asilimia 60**; pamoja na ujenzi wa vituo **10** vya kuchotea maji uliofikia **asilimia 45**. Vilevile, kazi ya kulaza mabomba ya kusambaza maji Mjini Bunda imeanza kwa uchimbaji wa mtaro wa umbali wa **kilomita 2** pamoja na ununuzi wa mabomba. Kazi hizo zitakamilika mwezi Juni, 2015.

#### **(c) Mji wa Orkesumet**

**195. Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na kero ya uhaba wa maji katika Mji wa Orkesumet, Serikali kwa kushirikiana na *BADEA* na *OFID* itajenga mradi wa majisafi utakaohudumia wakazi wa Mji huo. Mradi huo utagharimu **Dola za Marekani milioni 18.4**, kati ya fedha hizo *BADEA* imetoa **Dola za Marekani milioni 8**, *OFID Dola za Marekani milioni 8* na Serikali itatoa **Dola za Marekani milioni 2.4**. Kazi zitakazotekelawa ni pamoja na ulazaji wa bomba kuu umbali wa **kilomita 44**; mabomba ya usambazaji maji **kilomita 52**; ujenzi wa matanki **manne** yenye uwezo wa **lita milioni 1.6, lita 150,000, lita 225,000** na **lita 50,000**; ujenzi wa magati **10** na vituo **vinane** vya kuchotea maji. Hadi mwezi Aprili, 2015 Mtaalam Mshauri amekamilisha mapitio na kuwasilisha rasimu ya makabrasha ya zabuni kwa ajili ya kumwajiri Mkandarasi wa ujenzi. Wizara imeomba kibali *BADEA* na *OFID* kwa ajili ya kumpata Mkandarasi. Ujenzi utaanza katika mwaka wa fedha 2015/2016 na jumla ya **shilingi**

**bilioni 1.8** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo. Kati ya fedha hizo, **shilingi milioni 800** ni fedha za ndani.

**(d) Mji wa Muheza**

**196. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeandaa mradi wa kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Muheza. Mradi huo utatoa maji kutoka Mto Zigi kwenye milima ya Amani hadi Muheza umbali wa **kilomita 22.7**. Kazi za usanifu wa kina na tathmini ya athari za kimazingira na kijamii (*ESIA*) zimekamilika mwezi Machi, 2015. Aidha, Wizara yangu imejadiliana na Kampuni ya *EUROFINSA* ya Hispania kwa ajili ya kutekeleza mradi huo. Kampuni hiyo imewasilisha andiko la mradi kwa kutumia taratibu za *Engineering Procurement and Construction (EPC)*. Wizara imeridhika na andiko hilo na kuliwasilisha Ofisi ya Rais-Tume ya Mipango kwa ajili ya kuridhiwa na hatimaye kuwasilishwa Wizara ya Fedha. Mradi unatarajiwaa kuanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2015/2016 kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 26.63**. Mradi utakapokamilika utakuwa ndio ufumbuzi wa kudumu wa kero ya maji safi na salama kwa wakazi wapatao **30,384** wa Mji wa Muheza.

**(e) Mji wa Karatu**

**197. Mheshimiwa Spika**, mradi wa maji Mjini Karatu ulizinduliwa rasmi tarehe 22/04/2014 na **Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mradi huo umeongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 1.2** kwa siku hadi **lita milioni 1.92** kwa siku, sawa na **asilimia 41** ya mahitaji ya maji ya **lita milioni 4.7** kwa siku. Katika mwaka 2015/2016, Wizara yangu itaendelea kutekeleza kazi zilizobaki ambazo ni kukamilisha ujenzi wa visima **viwili** katika maeneo ya Bwawani na Kwa-Tom; ujenzi wa tanki **moja** lenye ujazo wa lita **225,000**; ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji umbali wa **kilomita 3.8**; ujenzi wa vioski **13**; ulazaji wa bomba kuu umbali wa **kilomita 5**; na kusambaza mabomba ya maji umbali wa **kilomita 8** katika eneo la G – Lambo.

**(f) Miradi ya Maji ya Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo**

**198. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu imetuma kiasi cha **shilingi bilioni 4.26** kwa ajili ya kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo. Miji hiyo ni pamoja na Ifakara, Ludewa, Mkuranga, Kondoa, Gairo, Namanyere, Chamwino, Dakawa, Vwawa, Mpwapwa, Mwanga, Mlowo, Igunga, Lamadi, Misungwi, Magu, Ilula, Chunya, Bunda, Tinde na Mutukula. Fedha hizo zimeziwezesha Mamlaka za Maji katika miji hiyo kuongeza wastani wa upatikanaji wa huduma ya maji kutoka **asilimia 57** mwaka 2013/2014 hadi kufikia **asilimia 60** mwaka 2014/2015. Katika mwaka 2015/2016, Serikali imetenga **shilingi bilioni 20** kwa ajili ya kuendelea na kazi za kukarabati na kupanua miundombinu ya maji katika miji hiyo. **Jedwali Na. 10** linaonesha mchanganuo wa fedha zitakazotumwa kwenye Mamlaka za Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo kwa mwaka 2015/2016. Utekelezaji wa miradi hiyo kwa mwaka 2014/2015 ni kama ifuatavyo:-

**(i) Mji wa Namanyere**

**199. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara ilituma **Shilingi milioni 650** kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Namanyere. Kazi zinazoendelea kutekelezwa ni ukarabati na upanuzi wa bwawa la maji la Mfili, ununuzi wa pampu na kuzifunga katika visima **vinne** vilivyochimbwa, ununuzi wa madawa ya kutibu maji na kukamilisha ulazaji wa bomba la usambazaji maji umbali wa **kilomita 2.7** kutoka Bwawa la Mfili hadi kwenye matanki ya maji.

**(ii) Mji Mdogo wa Lamadi**

**200. Mheshimiwa Spika**, kwa Mji Mdogo wa Lamadi, Wizara imetuma **shilingi milioni 195.8** kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji katika mji huo. Kazi zinazoendelea kutekelezwa ni ulazaji wa bomba kuu kutoka Ziwa Victoria lenye urefu wa mita **156**, ujenzi wa nyumba ya mtambo wa kusukuma maji na *sump tank*, ulazaji wa bomba la usambazaji maji umbali wa kilomita **14**, ujenzi wa vioski **17** na ununuzi wa matanki **manane** yenye ujazo wa **lita 10,000** kila moja. Kukamilika kwa kazi hizo kutaongeza upatikanaji wa huduma ya maji safi katika mji huo na kuwanufaisha wakazi wapatao **15,000**. Hadi mwezi Aprili 2015, utekelezaji wa mradi umefikia **asilimia 70** na utakamilika mwezi Juni, 2015.

**(iii) Mji wa Kilwa Masoko**

**201. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Mji wa Kilwa Masoko ulipatiwa **shilingi milioni 100** kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji. Kazi zinazoendelea kutekelezwa ni ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji umbali wa kilomita **3.18**, ukarabati wa tanki la maji la ujazo wa **lita 250,000** katika cha kitongoji cha Mpara pamoja na ulazaji wa bomba kuu umbali wa **kilomita 2.8** ili kuwezesha maji kufika katika tanki lililoko Mji wa Kilwa Masoko. Kukamilika kwa kazi hizo, wananchi zaidi ya **5,000** wa vitongoji vya Mpara, Mkwanyule, Kisangi, na Miina watapata huduma ya maji ya uhakika na endelevu.

**(iv) Mji Mdogo wa Ilula**

**202. Mheshimiwa Spika**, katika Mji mdogo wa Ilula, kwa kipindi cha mwaka 2013/2014 na 2014/2015, Serikali imetuma **shilingi milioni 616** kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo; kukarabati eneo la kuchotea maji (*intake*) katika mto Idemule chenye uwezo wa kuzalisha **lita 940,000** kwa siku; ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji umbali wa **kilomita 21.3**, kubadilisha mabomba ya zamani kwa umbali wa **kilomita 6.21** na kukarabati tanki la Mazombe la ujazo wa **lita 45,000**. Kazi hizo zimekamilika na kuongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita 600,000** kwa siku hadi **lita 940,000** kwa siku. Aidha, Wizara yangu inaendelea na mazungumzo na Kampuni ya Ostap ya nchini Austria ambayo imeonesha nia ya kutekeleza mradi wa kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Ilula. Kampuni hiyo imeelekezwa kuwasilisha Andiko la Mradi (*Project*

*Proposal*) pamoja na mpangokazi (*workplan*) kwa ajili ya kupitiwa na kuwasilishwa Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango kwa hatua zaidi.

#### **(v) Mji Mdogo wa Tinde**

**203. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara ilituma shilingi **milioni 100**, kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji katika Mji Mdogo wa Tinde. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni uchimbaji wa kisima kirefu, ujenzi wa magati, nyumba ya mtambo wa kusukuma maji na ununuzi wa tanki la plastiki. Hadi mwezi Aprili 2015, kazi ya uchimbaji wa kisima imekamilika na kazi zinazoendelea ni ujenzi wa magati **matatu**, nyumba ya mtambo kusukuma maji, usanifu wa mtandao wa kusambaza maji na ununuzi wa mabomba na tanki la maji. Kazi hizo zitakamilika mwezi Julai, 2015 na kukamilika kwake kutawanufaisha wakazi **6,316** wa mji huo.

#### **(vi) Mji ya Mugumu, Tarime na Sirari**

##### ***Mji ya Mugumu na Tarime***

**204. Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha huduma ya maji katika Mji ya Mugumu na Tarime, Wizara ilituma jumla ya **shilingi milioni 900** kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo ya maji. Kwa upande wa Mji wa Mugumu, kiasi cha **shilingi milioni 350** kilitumwa kwa ajili ya ujenzi wa mtambo wa kusafisha maji na ujenzi wa mradi huo umefikia **asilimia 40**. Aidha, katika Mji wa Tarime, **shilingi milioni 550** zilitumwa kwa ajili ya kutekeleza kazi za ujenzi wa nyumba **tatu** za mitambo ya kusukuma maji, ujenzi wa tanki la ujazo wa **lita 100,000**, ulazaji wa bomba kuu kwa umbali wa **kilomita 2.91** na ujenzi wa vituo **vinne** vya kuchotea maji. Mradi huo umefikia **asilimia 75** na wananchi wameanza kupata huduma ya maji kuititia vituo vitatu. Kazi zinazoendelea ni ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji. Miradi katika miji hiyo, itakamilika katika mwaka 2015/2016.

##### ***Mji wa Sirari***

**205. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na AfDB chini ya LV-WATSAN inatekeleza mradi wa kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Sirari. Kazi zitakazohusika ni pamoja na kulaza bomba kuu umbali wa **kilomita 4.5** kutoka Isibania, Kenya hadi Sirari; ujenzi wa *intake* kutoka Mto Hibwa; na tanki la ujazo wa **lita 250,000** litakalojengwa Sirari. Mradi unatarajiwu kugharimu **shilingi milioni 340**. Utekelezaji wa mradi umeanza kwa upande wa Kenya na kwa Tanzania, Mkandarasi ameajiriwa na ataanza kazi mara baada ya Halmashauri ya Tarime kukamilisha ulipaji wa fidia kwenye eneo la kujenga tanki. Kwa upande wa Tanzania, ujenzi huo utasimamiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Musoma. Kukamilika kwa mradi huo kutawanufaisha wakazi **16,000** wa Mji wa Sirari.

#### **(vii) Mji wa Chamwino**

**206. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu imetuma jumla ya **shilingi milioni 250** kwa ajili ya kutekeleza kazi za ukarabati wa mabomba kutoka

Chamwino Ikulu hadi Bwigiri umbali wa **kilomita 6**; ukarabati wa mabomba kutoka Chamwino hadi Msanga umbali wa **kilomita 6**; ununuzi wa dira za maji **770** pamoja na viungio vyake; kuunganisha wateja **300** kwenye mfumo mpya wa mabomba baada ya kuwaondoa kwenye mabomba yaliyochakaa. Hadi mwezi Aprili 2015, kwa ujumla kazi hizo zimetekelawa kwa wastani wa **asilimia 40** na zinatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2015 ambapo jumla ya wananchi **8,518** Mji wa Chamwino watanufaika na huduma ya majisafi. Mipango ya baadaye ni kutekeleza mipango ya muda wa kati na muda mrefu. Katika mipango ya muda wa kati, Wizara imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:- ukarabati wa tanki la maji la Bwigiri la ujazo wa **lita 400,000** pamoja na kufufua visima **viwili** nya maji vilivyopo Chamwino. Kwa upande wa mipango ya muda mrefu, Mtaalam Mshauri kupitia Awamu ya pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji atafanya upembuzi yakinifu na usanifu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji katika Miji ya Chamwino na Bahi. Katika mwaka 2015/2016, taratibu za kumwajiri Mtaalam Mshauri zitaendelea.

#### (viii) Mji ya Gairo, Dakawa na Ifakara

**207. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara ilituma kiasi cha **shilingi milioni 880** katika Mji ya Gairo (**milioni 500**), Dakawa (**milioni 300**) na Ifakara (**milioni 80**) kwa ajili ya kutekeleza kazi mbalimbali za kuboresha hali ya huduma ya maji katika miji hiyo. Kwa mji wa Gairo kazi zilizotekelawa ni ulazaji wa bomba kuu na bomba la usambazaji yenye urefu wa **kilomita 8.46**, uchimbaji wa visima **vitatu** na ujenzi wa vituo **vinane** nya kuchotea maji na utekelezaji wa kazi hizo kwa sasa umefikia **asilimia 60**. Kwa upande wa Mji wa Dakawa, kazi zilizotekelawa ni ulazaji wa bomba kuu na bomba la usambazaji lenye urefu wa **kilomita 8.15**, ujenzi wa vituo **vitatu** nya kuchotea maji na ununuzi wa dira za maji. Utekelezaji wa kazi hizo umefikia **asilimia 85**. Vilevile, katika Mji wa Ifakara kazi za ulazaji wa bomba kuu na bomba la kusambaza maji lenye urefu wa **kilomita 2.4** zimekamilika na ujenzi wa nyumba ya mtambo wa kusukuma maji unaendelea.

#### (ix) Mji wa Mkuranga

**208. Mheshimiwa Spika**, ili kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Mkuranga, Wizara ilituma kiasi cha **shilingi millioni 100**. Kazi zilizotekelawa ni pamoja na uchimbaji wa kisima, ulazaji wa bomba kuu **kilomita 2** kutoka katika visima hadi kwenye matanki, mabomba ya kusambaza maji yenye urefu wa kilomita **7.2**, kununua pamoja na kufunga pampu **mbili**. Kazi hizo zinatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2015.

#### (x) Mji wa Longido

**209. Mheshimiwa Spika**, katika kutatua tatizo la maji kwenye Mji wa Longido, Wizara yangu imefanya utafiti wa kina na kubaini kuwa chanzo pekee ambacho kitatosheleza mahitaji ya maji ni Mto Simba Kilichopo Mlima Kilimanjaro, Wilaya ya Siha Mkoani Kilimanjaro. Mradi huo utahudumia wakazi wa Mji wa Longido na Vijiji nya Oltepesh, Orbomba na Engikaret. Hadi mwezi Aprili 2015, usanifu wa kina na utayarishaji wa makabrasha ya zabuni umekamilika. Katika mwaka 2015/2016, ujenzi wa mradi

unatarajiwa kuanza baada ya kuajiri Mkandarasi na Wizara imetenga **shilingi bilioni 2** kwa ajili ya kutekeleza mradi huo.

### 3.3.7 Miradi ya Maji ya Kitaifa

**210. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika miji na vijiji vinavyohudumiwa na Miradi ya Kitaifa. Katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu ilituma fedha kwenye miradi hiyo kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji na utekelezaji wa miradi hiyo kwa mwaka huo na kazi zinazoendelea ni kama ifuatavyo:-

#### (i) Mradi wa Maji Chalinze

**211. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Serikali kwa kushirikiana na *BADEA*, Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China na Mfuko wa Pamoja wa Sekta ya Maji (*Basket Fund*), iliendelea kutekeleza Awamu ya Pili ya mradi wa maji Chalinze. Kazi zilizotekelawa ni pamoja na ujenzi wa matanki **40**; ujenzi wa vituo **372** vya kuchotea maji; ulazaji wa bomba kuu lenye umbali wa **kilomita 335** na mabomba ya kusambaza maji (**kilomita 127**) katika vijiji 47 pamoja na Kambi **3** za Jeshi. Awamu hiyo imegawanya katika vipande **tisa** ambavyo ni: **Lot 1, Lot 2, Lot 3, Lot 4, Lot 5, Lot 6, Package F, Package H** na **Package J**.

**212. Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Aprili 2015, miradi katika **Lot 1, Lot 2, Lot 4, Lot 5, Lot 6** na **Package J** imekamilika na wananchi katika vijiji **32** na Kambi **3** za Jeshi wanapata maji. Vijiji vilivyonufaika ni pamoja na Mkange, Mihuga, Mandamazingara, Masimbani, Kweikonje, Masuguru, Madesa, Pongwe-Msungura, Kiwangwa, Fukayosi, Kidomole, Makurunge, Mkenge, Msinune, Vigwaza, Buyuni, Visezi, Chamakweza, Chahua, Gwata, Gumba, Magindu, Lukenge, Kwaruhombo, Kifuleta, Pongwe-Kiona, Kwang'andu, Kidugalo, Ngerengere, Sinyaulime, Bwawani-Gwata, Kinonko, pamoja na Kambi za Jeshi za Sangasanga, Kizuka na Kinonko. Aidha, kwa upande wa **Lot 3**, mradi umelenga kuboresha huduma ya maji katika vijiji **7** ambapo utekelezaji wa mradi huo umekamilika katika vijiji **6** na wananchi wa vijiji hivyo wanapata maji. Vijiji vilivyonufaika ni Kinzaguzi, Makombe, Talwanda, Msigi, Kisanga na Mindukeni. Kazi ya ulazaji bomba katika kijiji cha Malivundo inaendelea na itakamilika mwezi Julai, 2015.

**213. Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa mradi wa **Package H**, unaohusisha vijiji **8** unaendelea na kwa sasa vijiji **vitatu** vya Msolwa, Mdaula na Matuli vinapata maji. Vijiji **vitano** vilivybaki vya Mwidu, Visakazi, Tukamisasa, Kaloleni na Ubenazomozi utekelezaji wake umefikia **asilimia 95** na ujenzi utakamilika mwezi Juni, 2015. Kwa upande wa **Package F**, ujenzi unaendelea na hadi mwezi Aprili 2015, kazi zilizokamilika ni kufunga pampu **2** Mbewe na Mkandarasi anaendelea na ujenzi wa vituo vya kusukuma maji; kufanya majoribio ya pampu **4** za Ubenazomozi na kufunga mtambo kwenye chujio la Wami. Kazi hizo zitakamilika mwezi Julai, 2015. Mradi utakapokamilika, utawanufaisha wakazi **197,684** wa Wilaya tatu za Bagamoyo, Kibaha na Morogoro Vijijini. **Jedwali Na. 11** linaonesha vijiji vilivyonufaika kwa kila kipande cha mradi.

**214. Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Aprili 2015, Mkandarasi wa utekelezaji wa Awamu ya Tatu ya mradi wa maji wa Chalinze amepatikana na gharama ya mradi ni **Dola za Marekani milioni 60**. Kazi zitakazotekelawa ni pamoja na kukarabati wa chanzo; kujenga tanki kubwa la kuhifadhi maji lenye uwezo wa **lita milioni 2** katika Mlima Mazizi; kujenga matanki **18** ya kuhifadhi maji yenye jumla ya **lita milioni 2.75**; kupanua mitandao ya kusambaza maji; kufunga pampu za kusukuma maji kutoka Wami hadi kwenye tanki la Mlima Mazizi; kufunga pampu kwenye kituo cha Mbwewe ili kusukuma maji kwenda katika kijiji cha Manga Wilayani Handeni; pamoja na kujenga vituo **210** vya kuchotea maji katika maeneo ambayo hayakufikiwa na ujenzi wa Awamu ya Kwanza na ya Pili. Mradi huo unatarajiwa kuanza mwezi Juni, 2015 na utachukuwa muda wa miezi 15 hadi kukamilika. Mradi ukikamilika utaongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 7.2** za sasa hadi **lita milioni 11** kwa siku. Katika mwaka 2015/2016, Serikali imetenga **shilingi bilioni 3** kwa kuanza utekelezaji wa mradi wa Awamu ya Tatu.

#### (ii) Mradi wa Mugango-Kiabakari

**215. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Serikali ilituma **shilingi milioni 100** kwa ajili ya ukarabati wa bomba kuu la maji kutoka kwenye chanzo hadi Kiabakari na kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Butiama. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (*BADEA*) na Mfuko wa Maendeleo wa Saudia (*Saudi Fund for Development-SFD*) imeanza mpango wa kutekeleza mradi wa maji wa Mugango–Kiabakari. Mradi huo unakadirwa kugharimu **Dola za Marekani milioni 30.69**. Kazi zitakazotekelawa ni ujenzi wa chanzo; ujenzi wa mtambo wa kusafisha na kusukuma maji; kujenga matanki **matatu**; kulaza mabomba kutoka eneo la Mugango kuititia Kiabakari hadi Butiama umbali wa **kilomita 32**; kukarabati mitambo ya kusukuma maji ya Kiabakari; na kulaza mabomba ya mtandao wa usambazaji maji kutoka Butiama hadi Bisalye.

**216. Mheshimiwa Spika**, kukamilika kwa mradi huo kutawanufaisha wakazi wapatao **80,000** waliopo eneo la mradi pamoja na vijiji vilivypo umbali wa kilomita 12 pembezoni mwa bomba kuu. Wizara imeomba kibali (*No Objection*) *BADEA* na *Saudi Fund* kwa ajili ya kumpata Mtaalam Mshauri wa kufanya mapitio ya usanifu na usanifu wa mradi wa miundombinu ya maji na mkataba umesainiwa tarehe 11/05/2015 na kazi ya mapitio itaanza mwezi Juni, 2015. Katika mwaka 2015/2016, Serikali imetenga **shilingi milioni 300**, fedha za ndani kwa ajili ya kuboresha huduma ya upatikanaji wa maji katika eneo la mradi wakati matayarisho ya ujenzi wa mradi mpya yanaendelea.

#### (iii) Mradi wa Makonde

**217. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Serikali ilituma **shilingi milioni 226** kwa ajili ya kuboresha hali ya upatikanaji wa maji katika vijiji na miji katika Mradi wa Kitaifa wa Makonde. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Uingereza kuititia Idara yake ya Maendeleo ya Kimataifa (*DFID*) itakarabati visima virefu **sita** katika chanzo cha Mitema. Kazi hiyo inatarajiwa kuanza mwezi Juni, 2015 na kukamilika

mwezi Septemba, 2015. Mahitaji ya maji kwa sasa ni **lita milioni 14.2** kwa siku ambapo, kukamilika kwa kazi hiyo kutaongeza uzalishaji wa maji kutoka **lita milioni 7.4** za sasa hadi **lita milioni 14.8** kwa siku na kuweza kuboresha huduma ya upatikanaji wa maji katika maeneo yanayohudumiwa na mradi huo. Katika mwaka 2015/2016, jumla ya **shilingi bilioni 1.8** zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo. Aidha, Wizara yangu inaendelea na majadiliano na Kampuni ya *Ostap* ya nchini Austria ambayo imeonesha nia ya kutekeleza kazi za kuboresha huduma ya maji katika Mradi wa Kitaifa wa Makonde. Hadi sasa Kampuni hiyo imeelekezwa kuwasilisha Andiko la Mradi (*Project Proposal*) pamoja na mpangokazi kwa ajili ya kupitiwa na kuwasilishwa Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango kwa hatua zaidi.

**(iv) Mradi wa Handeni Trunk Main (HTM)**

**218. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu ilituma **shilingi milioni 150** kwa ajili ya kuboresha hali ya upatikanaji wa maji katika miji na vijiji vinavyohudumiwa na mradi wa Kitaifa wa *HTM*. Aidha, Wizara yangu inaendelea na majadiliano na Kampuni ya *BAM International* ya nchini Uhlanzi pamoja na *AfDB* kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji katika maeneo yanayohudumiwa na mradi wa kitaifa wa *HTM*. Katika mwaka 2015/2016, Serikali imetenga fedha za ndani **shilingi bilioni 1** kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji katika eneo la mradi wakati matayarisho ya mradi mpya yanaendelea.

**(v) Mradi wa Wanging'ombe**

**219. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Serikali yangu ilituma **shilingi milioni 180** kwa ajili ya kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika miji na vijiji vinavyohudumiwa na Mradi wa Kitaifa wa Wanging'ombe. Aidha, Wizara yangu imejadiliana na Kampuni ya *EUROFINSA* ya Hispania kwa ajili ya kutekeleza mradi huo. Kampuni hiyo imewasilisha andiko la mradi kwa kutumia taratibu za *Engineering Procurement and Construction (EPC)*. Wizara imeridhika na andiko hilo na kuliwasilisha Ofisi ya Rais-Tume ya Mipango kwa ajili ya kuridhiwa na hatimaye kuwasilishwa Wizara ya Fedha. Mradi unatarajiwa kuanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2015/2016 kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 64.69**. Vilevile, Serikali imetenga **shilingi milioni 800** fedha za ndani kwa ajili ya kuboresha huduma ya upatikanaji wa maji kabla ya kuanza kutekeleza mradi mpya.

**(vi) Mradi wa Masasi-Nachingwea**

**220. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu ilituma **shilingi milioni 84** kwa Mamlaka ya Maji Mtwara ambayo ilikuwa ni msimamizi wa ujenzi wa mradi wa maji wa Masasi-Nachingwea kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi walioipisha ulazaji wa bomba kuu la maji katika vijiji vya Chinongwe na Likwachu Wilayani Ruangwa; na vijiji vya Chiumbati na Tunduru-ya-Leo katika Wilaya ya Nachingwea. Katika mwaka 2015/2016, Serikali imetenga fedha za ndani **shilingi bilioni 1** kwa ajili ya kuimarisha huduma ya maji kwenye maeneo ya Mradi wa Kitaifa wa Maji wa Masasi-Nachingwea.

## (vii) Mradi wa Maswa

**221. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu ilituma **shilingi milioni 50** kwa Mamlaka ya Mradi wa Kitaifa Maswa, kwa ajili ya kulipia sehemu ya gharama za umeme wa mitambo ya kusukuma maji. Katika mwaka 2015/2016, Serikali imetenga **shilingi bilioni 1.5** kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji katika maeneo yanayohudumiwa na mradi huo.

### 3.3.9 Kuzijengea Uwezo Mamlaka za Maji Mijini

#### (a) Ujenzi wa Ofisi za Mamlaka

**222. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuzijengea uwezo Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira Mijini kwa kujenga na kukarabati ofisi za mamlaka. Hadi mwezi Aprili 2015, ujenzi wa ofisi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Babati umefikia **asilimia 92**. Katika Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Tunduma, ujenzi wa ofisi umefikia **asilimia 70**. Aidha, Wizara yangu imezielekeza Mamlaka za Maji za Miji ya Geita na Mpanda kuwasilisha michoro ya ofisi na makadirio ya gharama za ujenzi kwa ajili ya kuhakikiwa ili ujenzi uanze. Katika mwaka 2015/2016, Wizara yangu itakamilisha ujenzi wa ofisi za Mamlaka za Maji za Babati na Tunduma, na kuanza ujenzi wa ofisi za Mamlaka za Geita na Mpanda. Vilevile, ukarabati wa ofisi za mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira katika Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa utafanyika.

#### (b) Mafunzo kwa Watumishi

**223. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Serikali ikishirikiana na Shirika la Maendeleo la Ujerumanu (GIZ) imeendelea kuzijengea uwezo Mamlaka za Miji ya Wilaya na Miji Midogo pamoja na Miradi ya Kitaifa kwa kutoa mafunzo. Mafunzo yaliyotolewa yalihusu nyanja za kiufundi; uongozi na utawala; biashara; na usimamizi wa fedha. Faida zilizopatikana kwa watumishi wa Mamlaka hizo ni kuongezeka kwa ufanisi wa utendaji kazi za kila siku na kuendelea kuwapatia huduma bora wananchi. Katika mwaka 2015/2016, Wizara kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji itaendelea kuisimamia miradi inayotekelawa kwenye mamlaka za maji mijini ili iweze kukamilika na kuweza kutoa matokeo yaliyotarajiwa. Vilevile, Wizara yangu itaziimarisha Mamlaka za Maji Mijini kwa kuzipatia ofisi vitendea kazi, mafunzo na watumishi wa kutosha ili ziongeze ufanisi katika utoaji wa huduma ya maji kwenye maeneo yao.

#### (c) Malipo ya Umeme

**224. Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imeendelea kuchangia gharama ya sehemu ya ankara za umeme kwa Mamlaka za Maji Mijini za Daraja C pamoja na Miradi ya Kitaifa. Katika mwaka 2014/2015, jumla ya **shilingi milioni 506** zimetumwa kwenye Mamlaka za Miradi ya Maji ya Kitaifa kwa ajili ya kulipia sehemu ya ankara za umeme wa mitambo ya kuzalisha maji. Katika mwaka 2015/2016, Wizara yangu itaendelea

kuziimarisha Mamlaka hizo ili hatimaye ziweze kuijendesha kibiashara na hivyo, kuipunguzia Serikali mzigo.

### 3.4 TAASISI ZA WIZARA YA MAJI

#### 3.4.1 Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (*EWURA*)

**225. Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea kuisimamia Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (*EWURA*) ili iweze kutekeleza majukumu yake ya kutoa leseni, kusimamia utekelezaji wa masharti ya leseni, kudhibiti ubora na ufanisi wa utoaji huduma, kutathmini na kuitisha bei za huduma na kutatua migogoro baina ya watoa huduma na wateja wao. *EWURA* inatekeleza majukumu hayo kulingana na Kifungu **Na. 414** cha Sheria **Na.11** ya *EWURA* ya mwaka 2001; ambapo Sheria hiyo inaitaka *EWURA* kudhibiti utoaji wa huduma kwenye Sekta za umeme, mafuta ya petroli, gesi asilia, majisafi na usafi wa mazingira nchini. Katika mwaka 2014/2015, kwa upande wa Sekta ya Maji, *EWURA* imeendelea na udhibiti wa huduma za upatikanaji wa maji na uondoaji majitaka katika Mamlaka **146** za majisafi na usafi wa mazingira nchini. Kati ya hizo, Mamlaka **23** ni za Miji Mikuu ya Mikoa; Mamlaka **113** za Miji Mikuu ya Wilaya na Miji midogo; *DAWASA*; *DAWASCO*; na Mamlaka za Miradi **nane** ya maji ya Kitaifa.

**226. Mheshimiwa Spika**, *EWURA* ilipokea maombi ya kubadilisha bei za majisafi na majitaka kutoka Mamlaka **13** za majisafi na usafi wa mazingira na ilitathmini na kuidhinisha bei za Mamlaka **saba** za Mtwara, Tanga, Tabora, Dodoma, Singida, Kahama na Korogwe. Aidha, *EWURA* inaendelea kutathmini bei za maji za Mamlaka **sita** za Shinyanga, Ngudu, Moshi, Kiomboi, *KASHWASA* na *DAWASA*. Sababu za maombi ya mabadiliko ya bei ni kutohana na kuongezeka kwa gharama za uendeshaji na kuziwezesha Mamlaka kutekeleza mipango yao ya kibiashara. Vilevile, *EWURA* ilitoa maoni katika Mipango ya Kibiashara (*Business Plans*) ya miaka mitatu kutoka Mamlaka za Maji za Arusha, Babati, Dodoma, Geita, Iringa, Moshi, Mtwara, Mwanza, Shinyanga, Singida, Tanga, Tabora, Njombe, Mbanga, *KASHWASA*, *MANAWASA* na Ngudu. Mamlaka zilizobaki zinaendelea kutekeleza mipango yao ya kibiashara.

**227. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, *EWURA* ilikagua miundombinu inayotoa huduma ya majisafi na majitaka katika Mamlaka mbalimbali za maji mijini ili kuhakiki viwango vya huduma vinavyotolewa na Mamlaka hizo, kupima ubora wa maji, kufuatilia utekelezaji wa mipango ya kibiashara na utekelezaji wa maagizo ya *EWURA*. Mamlaka **61** zilikaguliwa ambazo ni:- Arusha, Babati, Bariadi, Bukoba, *DAWASCO/DAWASA*, Dodoma, Geita, Iringa, Kigoma, Lindi, Mbeya, Morogoro, Moshi, Mpanda, Mtwara, Musoma, Mwanza, Njombe, Shinyanga, Singida, Songea, Sumbawanga, Tabora, Tanga, Bunda, Chunya, Gairo, Igunga, Ilula, Itumba-Isongole, Kahama, Kondoa, Karagwe, Katesh, Kilwa-Masoko, Korogwe, Ludewa, Mafinga, Makete, Mbalizi, Mbulu, Mkuranga, Mpwapwa, Monduli, Nzega, Ngudu, Pangani, Orkesumet, Rujewa, Songe, Tukuyu, Tunduma, Tunduru, Utete, Vwawa, Chalinze, *HTM*, *KASHWASA*, Makonde, Wanging'ombe na *MANAWASA*. Ukaruzi na uhakiki huo unatumika kutoa maelekezo maalum kwa Mamlaka ili kuboresha kasoro zilizobainika na kuandaa taarifa ya utendaji wa Mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira mijini kila mwaka.

**228. Mheshimiwa Spika**, taarifa ya utendaji wa Mamlaka kwa kipindi cha mwaka 2013/2014 iliyotayarishwa na *EWURA*, inaonesha kuwa Mamlaka za maji zimepiga hatua katika ufungaji wa dira za maji, kuongezeka kwa idadi ya wateja wa majisafi na majitaka, kuongezeka kwa wastani wa saa za upatikanaji wa huduma ya maji na ukusanyaji wa maduhuli. Vilevile, *EWURA* ilipokea jumla ya malalamiko **saba** yaliyohusu ankara za majisafi na majitaka zilizokosewa, ukosefu wa maji, kukatiwa huduma ya maji kimakosa na huduma hafifu kwa wateja. Kati ya malalamiko hayo, **sita** yamepatiwa ufumbuzi na **moja** lililobaki liko katika hatua ya utatuvi.

**229. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Sekta Ndogo za Umeme, Petroli na Gesi Asilia, *EWURA* imeendelea kusimamia Sekta ndogo hizo ili kuhakikisha uwepo, ubora na usalama wa huduma hizo kwa kuandaa kanuni na taratibu zinazovutia uwekezaji. *EWURA* imetoa leseni **mbili** kwa wawekezaji wa miradi midogo ya umeme isiyozidi Megawati **10** (makampuni ya Mapembasi ya Njombe na Bwelui ya Mbeya); leseni mpya **125** za Petroli na kati ya hizo, leseni **saba** ni kwa ajili ya wauzaji wa jumla wa mafuta ya petroli, leseni **110** kwa ajili ya vituo vya mafuta, leseni **moja** kwa ajili ya uagizaji wa jumla wa vilainishi, leseni **tatu** za uagizaji wa jumla wa gesi ya kupikia inayotokana na mafuta ya petroli, leseni **moja** kwa ajili ya kuuza mafuta kwenye meli (*bunkering*), na leseni **tatu** kwa viwanda vyenye miundombinu ya mafuta kwa ajili ya matumizi binafsi (*Consumer Installation Licence*). Vilevile, *EWURA* imeendelea kupanga bei kikomo za mafuta ya petroli yanayouzwa kwenye vituo vya mafuta na kusimamia kuhakikisha mlaji hauziwi zaidi ya bei kikomo. Aidha, *EWURA* imeidhinisha ombi la *TPDC* la tozo la kuchakata na kusafirisha gesi asilia na imeendelea kukagua miundombinu ya kuchakata, kusafirisha na kusambaza gesi asilia na kubainika kuwa ni salama kwa matumizi na mazingira.

**230. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/2016, *EWURA* imelenga kuzingatia vipaumbele vifuatavyo katika kuimarisha udhibiti wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira nchini.

- (i) Uandaaji wa miongozo ya uwekezaji na ya utoaji wa huduma ya maji kwa kuishirikisha Sekta Binafsi katika utoaji wa huduma za majisafi na majitaka;
- (ii) Kufuatilia utendaji wa mamlaka za maji mijini kwa kuchambua na kuhakiki taarifa za utendaji kazi wa Mamlaka za maji nchini kwa kukagua miundombinu na utendaji wa mamlaka za maji;
- (iii) Ufuatiliaji wa utekelezaji wa miongozo ya viwango vya ubora wa huduma zinazotolewa na mamlaka za maji;
- (iv) Kuendelea kufuatilia utekelezaji wa mipango ya kibiashara (*Business Plans*) ya mamlaka kwa kuzingatia mwongozo uliotolewa na *EWURA*; na
- (v) Kuhakikisha kuwa viwango vya ubora wa huduma na viashiria vya utendaji vilivyoainishwa kwenye Mkataba wa Utendaji Kazi (*Performance Agreement*) vinazingatiwa na mamlaka.

**231. Mheshimiwa Spika**, *EWURA* ni mamlaka ya udhibiti wa Sekta kuu mbili za Nishati na Maji. Ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi, nimeagiza *EWURA* iendeleze ushirikiano wa karibu na kupokea na kutekeleza miongozo inayotolewa na Wizara zinazosimamia Sekta hizo kulingana na sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

### 3.4.2 Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji

**232. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Chuo kilidahili wanafunzi **383** wa stashahada (*Water Technicians*) na wanafunzi **119** wa shahada ya kwanza ya uhandisi wa rasilimali za maji na umwagiliaji (*Bachelor of Engineering in Water Resources and Irrigation*). Kwa sasa Chuo kina jumla ya wanafunzi **1,117**. Katika jitihada za kuongeza idadi ya wanafunzi wa kike katika masomo ya sayansi, Mamlaka ya Elimu Tanzania (*TEA*) ilifadhilli wanafunzi wa kike **41** katika kozi ya kuwawezesha kujiunga na masomo ya stashahada (*Access Course*). Ufadhilli huo umeongeza udahili wa wanafunzi wa kike kutoka **138** mwaka 2013/2014 hadi **224** katika mwaka 2014/2015. Vilevile, jumla ya wanafunzi **217** walihitimu mafunzo yao mwezi Novemba 2014 katika fani mbalimbali zinazohusu Sekta ya Maji. Katika kutekeleza jukumu la utoaji wa ushauri katika masuala ya maji, Chuo kilifanya utafiti wa maji chini ya ardhi katika Halmashauri za Songea Vijijini, Mwanga, Korogwe, Mvomero na Iringa Mjini.

**233. Mheshimiwa Spika**, Wizara iliendelea na mpango wa kukijengea uwezo Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji ambapo jumla ya watumishi **13** waligharamiwa mafunzo ya muda mrefu, watumishi **watano** mafunzo ya muda mfupi na watumishi wapya **17** walajiriwa. Aidha, maabara ya kupima mwenendo wa maji (*Hydraulics Laboratory*) ilikarabatiwa na imeanza kutumika. Maabara nyingine za kufundishia ziliboreshwu kwa kuwekewa vifaa mbalimbali vikiwemo vifaa vyaa uchunguzi wa ubora wa maji, hali ya hewa, haidrolojia, usambazaji maji na upimaji ardhi pamoja na ununuzi na ufungaji wa viti **800** katika madarasa. Aidha, Wizara ilikamilisha ukarabati wa majengo ya chuo mwezi Desemba, 2014; na kuajiri Mtaalam Mshauri kwa ajili ya kufanya usanifu wa jengo la ghorofa sita lenye madarasa, maabara, kumbi za mikutano na maktaba.

**234. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Serikali ilitenga jumla ya **shilingi milioni 300** kwa ajili ya Mfuko wa Mafundi Sanifu (*Water Technician Fund*) ambapo jumla ya wanafunzi **212** wamenufaika kwa kupata mkopo kutoka kwenye mfuko huo. Wizara yangu itaendelea kuchangia katika mfuko huo kiasi cha **shilingi milioni 300** kila mwaka ili wanafunzi wengi zaidi waweze kunufaika na mkopo huo. Katika mwaka 2015/2016, Chuo kitaongeza idadi ya wanafunzi wa mwaka wa kwanza wanaodahiliwa kwa mwaka kutoka **502** ya sasa na kufikia **920**. Vilevile, Wizara itagharamia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa watumishi **20** katika fani mbalimbali, na kuanza ujenzi wa jengo la ghorofa **sita** pamoja na kukarabati madarasa, mabweni pamoja na nyumba za walimu. Aidha, Chuo kimepanga kufanya tafiti mbalimbali ikiwemo uwepo wa maji chini ya ardhi kwenye maeneo **100**, uendelezaji wa miradi ya maji vijijini ikiwemo Mfumo wa *Water Point Mapping* na teknolojia ya uvunaji wa maji ya mvua; pamoja na mbinu za kupunguza upotevu wa maji mijini.

### 3.4.3 Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa (DDCA)

235. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu kuptitia Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa (DDCA) iliendelea na jukumu lake la kuongeza vyanzo vya maji kwa kuchimba visima maeneo mbalimbali nchini. Hadi mwezi Aprili 2015, DDCA imefanya uchunguzi wa maji chini ya ardhi kwenye maeneo **154** kwa ajili ya uchimbaji wa visima virefu na ifikapo mwezi Juni 2015, maeneo **214** yatakuwa yamechunguzwa. Vilevile, Wakala ulichimba visima virefu **233** na ifikapo mwezi Juni, 2015 kulingana na malengo, visima **300** vitakuwa vimechimbwa. **Jedwali Na. 12** linaonesha orodha ya visima vilivyochimbwa hadi mwezi Aprili, 2015.

236. **Mheshimiwa Spika**, Wakala umekamilisha miradi ya ujenzi wa miundombinu ya usambazaji maji katika jengo la Benki Kuu ya Tanzania na eneo la Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) Kibada-Kigamboni. Aidha, upembusi yakinifu wa miradi ya mabwawa katika maeneo ya Msomela na Mtunduzi yaliyopo Handeni ulikamilika. Hadi mwezi Aprili 2015, ujenzi wa mabwawa ya Aviv katika Halmashauri ya Songea na Tilia (Mbinga) pamoja na ukarabati wa mabwawa ya Olypasei katika Halmashauri ya Kiteto, Mbangala (Chunya), Kwamaligwa (Kilindi), Habiya (Itilima), Matwiga (Chunya) na Sekeididi (Kishapu) unaendelea na utakamilika katika mwaka 2015/2016.

237. **Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea kujenga uwezo wa Wakala kwa kununua mitambo kwa ajili ya uchimbaji visima, ujenzi wa mabwawa na vifaa vya uchunguzi wa maji chini ya ardhi. Vilevile, ukarabati wa karakana, mitambo na majengo unaendelea. Katika mwaka 2014/2015, Wizara imenunua mtambo kwa ajili ya uchimbaji visima yenye thamani ya **Dola za Marekani milioni 6.8** ikijumuisha seti **8** za mitambo ya kuchimbia visima (*drill rigs*); mitambo **7** ya kufua upemo (*compressors*); mitambo **mitano** ya kupimia wingi wa maji (*pumping test units*); karakana **moja** inayohamishika (*mobile workshop*); kamera **moja** ya kisima (*borehole camera*); na nyenzo za kazi. Jitihada hizo, zitauwezesha Wakala kuchimba visima virefu **450**, kufanya utafiti kwenye maeneo **300**, kujenga mabwawa makubwa **mawili**, ya ukubwa wa kati **manne** na mabwawa madogo **10** kwa mwaka. Vilevile, uchunguzi wa ubora wa udongo kwa ajili ya mahitaji mbalimbali ya kimaendeleo pamoja na usanifu wa maeneo **16** ya ujenzi wa mabwawa utafanyika.

### 3.4.4 Bohari Kuu ya Maji

238. **Mheshimiwa Spika**, Bohari Kuu ya Maji imeendelea kuhakikisha kuwa vifaa na nyenzo zenye ubora unaotakiwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji nchini vinawafikia watekelezaji wa miradi hiyo kulingana na mahitaji na kwa wakati. Hadi mwezi Aprili 2015, Wizara kuptitia Bohari Kuu ya Maji, imesambaza mabomba yenye vipenyo mbalimbali na urefu wa **kilomita 80,000**; viungio vyake (*fittings*); na dira za maji **10,000**. Vifaa hivyo vilipelekwa kwenye miradi ya maji inayotekelzwa katika Mamlaka za Maji za Singida, Babati, Wanging'ombe, Chalinze, Chamwino, Tanga, Mtwara, Dodoma, Kondoa, Namanyere, Makonde, Igunga, Kigoma, **KASHWASA** na kwenye Halmashauri za Wilaya mbalimbali nchini.

**239. Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia maagizo niliyotoa katika hotuba yangu ya mwaka jana, Bohari Kuu ya Maji imeanza kushirikiana na wadau mbalimbali kutoka Sekta Binafsi katika kutekeleza Sera ya Ubria baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (*Public Private Partnership-PPP*). Katika mwaka 2015/2016, Wizara yangu itaendelea kusambaza vifaa na nyenzo mbalimbali kwa ajili ya kuhakikisha miradi ya maji inatekelezwa kwa ufanisi. Vilevile, Bohari hiyo itaendelea kuwashawishi wawekezaji zaidi ili kuingia nao ubia, kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma na hivyo kupunguza utegemezi kwa Serikali Kuu.

### **3.5 MASUALA MTAMBUKA**

#### **3.5.1 Sheria**

**240. Mheshimiwa Spika**, ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa Sheria za maji, Wizara yangu imeendelea kutoa elimu kuhusu Sheria **Na.11** ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji na Sheria **Na. 12** ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira za mwaka 2009, kwa Halmashauri, Bodi za Maji za Mabonde, Mamlaka za maji na wadau wengine wa Sekta ya Maji pamoja na jamii kwa ujumla. Elimu hiyo hutolewa kuitia warsha, mikutano, semina na makongamano. Vilevile, Wizara inaendelea kutoa ushauri wa kisheria kuhusu utekelezaji wa Sheria hizo na kwa mwaka 2014/2015, jumla ya nakala **5,200** za Sheria za Maji na Kanuni zake zimesambazwa kwa wadau.

**241. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara imekamilisha kuandaa Matamko **matatu** ya kutambua maeneo ya mabonde madogo ya maji katika vyanzo na kuyatangaza kwenye Gazeti la Serikali la tarehe 19/09/2014. Vyanzo vya maji ambavyo mabonde madogo yametangazwa ni chanzo cha maji cha Kikuletwa/Ruvu [*The Water Resources Management (Designation and Declaration of Kikuletwa/Ruvu Water Catchment Area) Order 2014*]; chanzo cha maji cha Umba/Zigi [*Water Resources Management (Designation and Declaration of Umba/Zigi Water Catchment Area) Order, 2014*]; na chanzo cha maji cha Mto Ruaha Mkuu [*The Water Resources Management (Designation and Declaration of Great Ruaha Water Catchment Area) Order, 2014*].

**242. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, maoni, ushauri na mapendekezo ya wadau kuhusu Kanuni **nne** yamekusanywa, kufanyiwa kazi na kanuni hizo zipo kwenye utaratibu wa kutangazwa katika Gazeti la Serikali. Kanuni hizo ni *The Water Resources Management (Transfer of water use, discharge and groundwater permits) Regulations 2015; The Water Resources Management (Control and Management of Storm Water) Regulations 2015; The Water Supply and Sanitation (Provision and Management of Sewage and Waste Water Services) Regulations 2015; na The Water Supply and Sanitation (Delegation of Powers by the Minister to Local Government Authorities) Notice 2015*.

**243. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu imeendelea na mchakato wa kurekebisha Sheria **Na.11** ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji na Sheria **Na. 12** ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira za mwaka 2009 pamoja na Sheria **Na. 273** ya DAWASA ya mwaka 2001. Maoni, ushauri na mapendekezo ya wadau yaliyotolewa kwenye mkutano wa mapitio ya sheria hizo uliofanyika mwezi Februari, 2015 yanaendelea kufanyiwa kazi. Vilevile, Wizara imekamilisha rasimu ya **Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Maji** na kuijadili rasimu hiyo na wadau kwenye vikao vilivyofanyika mwezi Novemba, 2014 na Machi, 2015. Maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na wadau yamefanyiwa kazi na kwa sasa Wizara inaendelea na taratibu za kuwasilisha mapendekezo ya kutunga sheria hiyo kwenye Baraza la Mawaziri.

**244. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/2016, Wizara yangu itaendelea kukamilisha utayarishaji wa Kanuni za Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji na Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira kutegemeana na uhitaji, upatikanaji

wa rasilimali fedha pamoja na ukamilishaji wa tafiti. Vilevile, kukamilisha marekebisho ya Sheria za Maji, utayarishaji wa rasimu ya **Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Maji** na kuendelea kutoa ushauri kuhusu Sheria za maji kwa wadau wote wa Sekta.

### 3.5.2 Habari, Elimu na Mawasiliano

**245. Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imeendelea kutoa elimu na taarifa mbalimbali zinazohusu Sekta ya Maji, hii inatokana na umuhimu wake kwa jamii kama njia mojawapo ya kuelezea masuala ya usimamizi wa rasilimali za maji na uendelezaji wa miradi ya maji nchini. Mnamo mwezi Juni 2014, Wizara yangu ilishiriki kikamilifu katika maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika kitaifa Mkoani Dar es Salaam. Katika maonesho hayo, Wizara ilishika nafasi ya kwanza kwa ubunifu kwenye utendaji kazi wake kupitia teknolojia ya kuondoa madini ya *fluoride* kwenye maji kwa kutumia chengachenga za mifupa ya ng'ombe.

**246. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara iliendelea kutoa elimu kwa wananchi kupitia maonesho, warsha, tovuti na vyombo mbalimbali vya habari. Maadhisho ya Wiki ya Maji yaliyofanyika kitaifa mkoani Mara mwezi Machi 2015. Wakati wa maadhisho hayo, miradi ya maji ilizinduliwa na kuwekwa mawe ya msingi katika maeneo mbalimbali nchini. Mkoani Mara **Mhe. Dkt. Mohamed Gharib Bilal**, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliweka jiwe la msingi kwenye mradi wa maji wa Musoma na **Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda**, Waziri Mkuu aliweka jiwe la msingi kwenye mradi wa maji Bunda. Vilevile, Wizara yangu ilishiriki maonesho ya Kilimo ya Nanenane yaliyofanyika mwezi Agosti, 2014 katika viwanja vya Ngongo Mjini Lindi. Aidha, jumla ya machapisho **3,000** yalisambazwa kwa wadau; na vipindi **vitano** vya luninga na vipindi **vitatu** vya redio vilirushwa hewani katika kipindi cha maadhisho hayo. Pamoja na vipindi hivyo; Idara, vitengo, taasisi za Wizara na wadau mbalimbali wa sekta hutumia maadhisho hayo kuelimisha umma kuhusu kazi mbalimbali zinazotekelozwa katika Sekta ya Maji.

**247. Mheshimiwa Spika**, vilevile, katika mwaka 2014/ 2015, Wizara yangu ilitoa vipindi maalum katika redio na luninga, pamoja na makala kwenye magazeti yaliyolenga kufafanua na kuelimisha jamii kuhusu masuala mbalimbali ya Sekta ya Maji. Aidha, Wizara imefanikisha kuboresha tovuti na hivyo kuifanya kuwa rafiki zaidi kwa watumiaji. Katika mwaka 2015/2016, Wizara yangu itaendelea kuelimisha wananchi na kutoa taarifa mbalimbali zinazohusu Sekta ya Maji pamoja na kuandaa na kutangaza vipindi kwenye luninga na redio.

### 3.5.3 Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

**248. Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imeendelea na juhudzi za Serikali za utekelezaji wa mpango wa Serikali Mtandao ili kuboresha utoaji wa huduma zinazohusiana na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA). Katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu imeboresha mfumo wa kielektroniki wa takwimu na taarifa ([www.mowimis.go.tz](http://www.mowimis.go.tz)) ili kusaidia masuala ya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji. Vilevile, mafunzo kuhusu matumizi ya

mfumo wa kielektroniki wa takwimu na taarifa yametolewa kwa watumishi **30** wa Makao Makuu ya Wizara. Aidha, Wizara imepanga kuwapatia mafunzo hayo watumishi wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira, Bodi za Maji za Mabonde, Mikoa mipyä na Halmashauri za Wilaya ifikapo mwezi Julai 2015.

**249. Mheshimiwa Spika**, vilevile, Wizara imeendelea kutekeleza Mpango wa Uendeshaji wa Serikali kwa Uwazi (*Open Government Partnership*) kwa kuboresha tovuti yake ([www.maji.go.tz](http://www.maji.go.tz)) na kushiriki katika matumizi ya Tovuti ya Takwimu Huria ([www.opendata.go.tz](http://www.opendata.go.tz)). Lengo ni kurahisisha upatikanaji wa taarifa mbalimbali za Sekta ya Maji kwa uwazi ndani na nje ya nchi. Aidha, Wizara imeanza kutumia mfumo wa Barua Pepe ya Serikali (*Government Mailing System*) katika mawasiliano ya kiserikali badala ya kutumia anuani za barua pepe binafsi kama vile *yahoomain*, *gmail*, n.k; na pia, Wizara imeunganishwa kwenye Mkonga wa Taifa ili kuboresha urahisi wa mawasiliano kwa njia ya TEHAMA.

**250. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2015/2016, Wizara yangu itatekeleza kazi zifuatazo: kuandaa mpango mkakati wa TEHAMA wa Sekta ya Maji (*Water Sector ICT Strategy*) na miongozo ya matumizi ya TEHAMA; kuimarisha zaidi mfumo wa kielektroniki katika ukusanyaji wa takwimu, uchambuzi, na utayarishaji wa ramani za vituo vya kuchotea maji vijijini (*Water Point Mapping System*); kupanua mfumo wa kielektroniki wa Menejimenti ya Takwimu na Taarifa (*Management Information System*) na kuoanisha na mifumo mingine iliyopo; kutekeleza mpango wa ‘*Open Data*’; na kujenga uwezo wa Wizara na Taasisi zake katika matumizi ya TEHAMA kwa kununua vifaa vya kisasa na kutoa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu kwa wataalam.

### 3.5.4 Jinsia

**251. Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imeendelea kuhamasisha uwepo wa uwiano wa kijinsia baina ya wanawake na wanaume kama inavyoelekezwa katika Sera ya Maji (2002) pamoja na Sheria za Maji za mwaka 2009. Uwiano huo unazingatiwa kwenye maeneo ya vyombo vya maamuzi makubwa katika usimamizi, uendeshaji na matumizi kwenye utekelezaji wa miradi ya maji. Katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu ilishiriki katika Kongamano la Siku ya Wanawake Duniani lililofanyika kitaifa tarehe 06-08/03/2015 mkoani Morogoro. Vilevile, Wizara inazingatia suala la kurithishana madaraka (*succession plan*) kwa kuangalia sifa za miundo na kuweka kipaumbele hasa kwa wanawake wenye sifa; na imeendelea kuhamasisha wanawake kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali za uongozi.

**252. Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ujerumanî (GIZ) imeendelea kuandaa Mkakati na Mwongozo wa masuala ya jinsia. Nyaraka hizo zitatumika katika kupanga mipango madhubuti na kubaini changamoto zinazohusu jinsia mahala pa kazi na kuzipatia ufumbuzi. Katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea na mpango wa kuwa na uwiano/usawa katika uongozi kwa kuzingatia sifa, taaluma na uadilifu. Vilevile, Wizara itakamilisha maandalizi ya benki ya takwimu ya masuala ya jinsia kwa lengo la kuwa na takwimu sahihi za ushiriki unaozingatia jinsia katika mipango, ufuutiliaji na usimamizi wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji.

### **3.5.5 UKIMWI**

**253. Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imeendelea kutoa elimu kuhusu UKIMWI kwa watumishi wake, na tarehe 16/12/2014, Wizara kwa kushirikiana na G/Z iliadhimisha siku ya UKIMWI duniani kwa watumishi wote kwa kuendesha kongamano katika viwanja vya Makao Makuu ya Wizara. Katika kongamano hilo watumishi wapatao **600** walishiriki na kati ya hao, watumishi **141** walipata ushauri nasaha na kukubali kupima VVU kwa hiari yao. Matokeo ya upimaji huo yalibaini watumishi **watatu** kuwa na maambukizi ya VVU. Vilevile, Dawati la UKIMWI la Wizara lilishiriki katika maonesho ya Wiki ya Maji yaliyofanyika kitaifa Mkoani Mara tarehe 16-22/3/2015 kwa kutoa elimu, ushauri nasaha pamoja na upimaji wa hiari kwa jamii na washiriki walionesha mwitikio mkubwa.

**254. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu imeendelea kutoa posho maalum ya chakula na dawa kwa watumishi wake **10** waliojiweka wazi kuwa wanaishi na VVU ili kupata lishe bora. Vilevile, Kamati ya UKIMWI ya Wizara imeundwa na Mpango wa UKIMWI Mahali pa Kazi umeandaliwa tayari kwa utekelezaji. Aidha, Wizara itaendelea kutenga bajeti ya masuala ya UKIMWI; kuandaa mpango wa mafunzo utakaoonesha aina ya mafunzo yatakayotolewa; na kuzingatia mahitaji halisi ya watumishi wanaoishi na VVU kama yalivyoainishwa katika Sheria ya Kazi na Mwongozo wa Utumishi wa Umma.

### **3.5.6 Maendeleo ya Rasilimali Watu**

**255. Mheshimiwa Spika**, katika hotuba yangu ya mwaka jana nililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara inahitaji wataalam **8,749** kwa kipindi chote cha utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (2007-2025), ili kutekeleza majukumu kwa ufanisi na kufikia malengo yaliyokusudiwa. Katika kutekeleza suala hilo Wizara ilivasiliana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na kufanikiwa kupata kibali cha kuajiri wataalam **475**. Kibali hicho kilielekeza waajiriwe Wahandisi **125**, Mafundi Sanifu **150** wa Daraja la II na Mafundi Sanifu Wasaidizi **200**. Hadi mwezi Aprili, 2015 jumla ya wataalam **318** kati ya wataalam **475** wameajiriwa na kupangiwa vituo vya kazi.

**256. Mheshimiwa Spika**, ajira ya wataalam hao kutoka Sekretarieti ya Ajira ilifanyika kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza walajiriwa wataalam **41** kati ya hao **29** ni Wahandisi na **12** ni Mafundi Sanifu. Wataalam walioajiriwa katika awamu ya kwanza walipangiwa vituo vya kazi kwenye Idara za Wizara ili kupunguza uhaba wa watalaam. Katika awamu ya pili, Wizara ilipokea wataalam **277** ambao kati ya hao Wahandisi ni **67**, Mafundi Sanifu **210**. Watumishi hao wote walipangwa kwenye Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri za Wilaya. Hadi sasa Sekta ya Maji ina jumla ya wataalam **1,856** wanaosimamia na kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji.

**257. Mheshimiwa Spika**, Wizara imekamilisha mpango wa mafunzo kwa watumishi wa kuwajengea uwezo watumishi ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Aidha, viongozi **saba** wamehudhuria mafunzo ya usimamizi wa fedha (*Financial Management and Disbursement Course*); viongozi **34** wamehudhuria mafunzo ya kuboresha utendaji (*Strengthening Leadership Performance*); viongozi **wanane** wamehudhuria mafunzo ya utatuzi wa migogoro, usimamizi wa mikataba na utawala bora; na watumishi **15** wamehudhuria mafunzo ya *PPP*. Vilevile, watumishi **210** wa Sekta ya Maji wamehudhuria mafunzo ya kutumia mifumo ya kielektroniki ya *Management Information System (MIS)* na *Water Point Mapping (WPM)*; watumishi **20** wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi; na watumishi **85** wa fani ya haidrolojia kutoka Makao Makuu na Ofisi zote za Bodi za Maji za Mabonde wamepata mafunzo ya namna bora ya kukusanya takwimu kutoka kwenye vituo vyaa maji kwa kufuata taratibu za kimataifa za *World Metrological Organization*.

### **3.5.7 Mapambano Dhidi ya Rushwa**

**258. Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu katika mwaka 2014/2015, imeendelea na harakati za kupambana na vitendo vya rushwa kwenye maeneo yote ya kazi. Katika kutekeleza harakati hizo, Dawati la Malalamiko limeendelea kusimamia kwa karibu ambapo jumla ya malalamiko **matano** yalipokelewa na kupatiwa ufumbuzi. Aidha, baada ya kupokea mrejesho wa wadau kuhusu Mkataba wa Huduma kwa Mteja, Wizara itaufanya mapitio Mkataba huo ili ulingane na hali halisi ya mahitaji ya sasa katika kutoa huduma na kupunguza mianya ya rushwa.

### **3.5.8 Uratibu wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji**

**259. Mheshimiwa Spika**, Serikali katika azma yake ya kuendeleza Sekta ya Maji nchini, imeweka mfumo endelevu wa kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji. Kupitia mfumo huo, Serikali imeandaa na kutekeleza Sera ya Maji ya Mwaka 2002, Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Maji (2006-2015) na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (2006-2025). Vilevile, Mfumo huo unaandaa na kutekeleza taratibu za kisheria na kuweka muundo wa kitaasisi wenyewe uwezo wa kutekeleza Sera ya Maji. Muundo huo unahuisha ushirikishwaji wa Wadau wa Sekta ya Maji katika hatua mbalimbali za utekelezaji kuanzia uibuaji, usanifu, upangaji, ujenzi, usimamizi, uendeshaji hadi matengenezo ya miradi ya maji pamoja na kuchangia gharama za huduma ya maji.

**260. Mheshimiwa Spika**, Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (*Water Sector Development Programme – WSDP*) ya mwaka 2007 – 2025 inaendelea kutekelezwa nchini kote. Utekelezaji wa Progamu hiyo upo katika Awamu ya Pili baada ya Awamu ya kwanza kukamilika mwezi Juni, 2014. Programu hiyo inatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo. Kulingana na Hati ya Makubaliano kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo, Wizara yangu inaratibu programu hiyo kwa kushirikiana na OWM-TAMISEMI, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundji na Wizara ya Fedha. Lengo ni kuhakikisha kuwa viwango na kasi ya utekelezaji wa programu vinazingatia thamani ya fedha iliyowekezwa (*value for money*). Hadi mwezi Aprili 2015, vikao vya pamoja vya mashauriano kutoka ngazi ya wataalam hadi ngazi ya makatibu wakuu vilifanyika, na mukutano wa mwaka wa wadau wa Sekta ya Maji (*Joint Water Sector Review Meeting*) uliandaliwa na kufanyika kwa mafanikio tarehe 15 – 16 Novemba 2014 ambapo maamuzi kuhusu utekelezaji wa programu yalitolewa. Vilevile, ziara za ukaguzi (*Joint Supervision Missions*) zimefanyika pamoja na utayarishaji wa taarifa mbalimbali za utekelezaji. Uratibu huo unafanyika kulingana na matakwa ya Hati ya Makubaliano ya programu. Katika mwaka 2015/2016, Wizara yangu itaendelea kuratibu programu hiyo ikiwa ni pamoja na kuhakikisha majadiliano baina ya wadau wa sekta yanafanikiwa na kutoa taarifa mbalimbali za utekelezaji wa programu.

#### ***Awamu ya Pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji***

**261. Mheshimiwa Spika**, katika kikao kilichopita cha Bunge la bajeti, nililitaarifu Bunge lako Tukufu juu ya maandalizi ya Awamu ya Pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji yaliyohusisha tathmini ya utekelezaji wa awamu ya kwanza ya programu iliyofanyika mwezi Februari hadi Mei, 2013. Tathmini hiyo ilipitia maeneo yote yanayohitaji maboresho kwa ajili ya Awamu ya Pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (2014/2015 – 2018/2019). Maeneo hayo ni pamoja na utekelezaji wa Mipango Shirikishi ya Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji; mipango ya ujenzi wa miradi ya maji vijiji inayohusisha ukarabati, upanuzi, ujenzi wa miradi mipyaa na uendeshaji na matengenezo ya miradi katika Halmashauri; mipango ya ujenzi wa miradi ya maji katika Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo, kuboresha huduma za maji katika Miji Mikuu ya Mikoa likiwemo Jiji la Dar es Salaam; na mipango ya kuzijengea uwezo taasisi zinazotekeleza Programu ikiwa ni pamoja na kuongeza wigo wa Kampeni ya Kitaifa ya Usafi wa Mazingira. Hivi sasa, Wizara inaendelea na utekelezaji wa kipindi cha mpito kwa kukamilisha kazi za Awamu ya Kwanza ya programu.

**262. Mheshimiwa Spika**, Awamu ya Pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji itakuwa haina tofauti kubwa kimuundo na awamu iliyopita, na inakadirwa kuwa na bajeti ya **Dola za Marekani bilioni 3.3**. Awamu hiyo itatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano hadi mwaka 2018/2019. Katika awamu hiyo, Sekta ya Maji itatekeleza mpango wa kuboresha huduma za maji vijiji na mijini pamoja na usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji. Mpango huo unalenga kujenga, kukarabati na kupanua jumla ya vituo **76,334** vya kuchotea maji vyenye uwezo wa kuhudumia watu **19,080,000** vijiji na kufikisha vituo **155,934** vitakavyohudumia jumla ya watu **38,475,697** sawa na **asilimia 80** ifikapo mwaka 2020.

**263. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa huduma ya maji mijini, miradi mikubwa inayoendelea kutekelezwa katika Jiji la Dar es Salaam, inalenga maunganisho ya maji **500,000** majumbani, viwandani, Taasisi za Umma na shughuli za biashara ili kuongeza wastani wa upatikanaji wa huduma ya maji kutoka **asilimia 68** za sasa hadi **asilimia 95** ifikapo mwaka 2020. Vilevile, utekelezaji wa miradi ya ukarabati wa miundombinu ikiwa ni pamoja na udhibiti wa wizi wa maji utapunguza upotevu wa maji kutoka **asilimia 57** za sasa hadi **asilimia 25** ifikapo mwaka 2020.

**264. Mheshimiwa Spika**, kwa Miji Mikuu 23 ya Mikoa; mpango unalenga maunganisho ya maji **200,000** ya majumbani yatakayohudumia watu **2,000,000** ifikapo mwaka 2020; kupunguza upotevu wa maji kutoka **asilimia 35** za sasa hadi **asilimia 25** kwa kipindi hicho; na hivyo, kuongeza wastani wa upatikanaji wa huduma ya maji kutoka **asilimia 86** za sasa hadi **asilimia 98** ifikapo mwaka 2020. Aidha, katika Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na maeneo yanayohudumiwa na Miradi ya Kitaifa; miradi iliyopangwa kutekelezwa inalenga maunganisho ya maji **110,000** ya majumbani yatakayohudumia jumla ya watu **1,100,000**; hivyo kuongeza wastani wa upatikanaji wa huduma ya maji kutoka **asilimia 60** za sasa hadi **asilimia 65** ifikapo mwaka 2020.

**265. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa rasilimali za maji, hatua zitakazochukuliwa na Ofisi za Bodi za Maji za Mabonde nchini ni pamoja na kuyatambua, kuyatenga na kuyatangaza maeneo yote ya vyanzo vya maji kuwa hifadhi kisheria; kujenga mabwawa

na visima virefu hasa kwenye maeneo kame; kuboresha utendaji wa maabara za maji ili kudhibiti viwango vya majisafi na majitaka; kuboresha mfumo wa utoaji wa vibali vya kutumia maji kwa shughuli za kijamii na kiuchumi kwenye mabonde yote; na kuboresha menejimenti ya takwimu za wingi na ubora wa maji kwenye mabonde yote.

### **3.6 CHANGAMOTO NA HATUA ZINAZOCHUKULIWA**

**266. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2014/2015, Sekta ya Maji imekuwa na mafanikio hasa kwa upande wa utekelezaji wa miradi ya maji vijijini kupitia mpango wa *BRN*. Pamoja na mafanikio hayo, Sekta imeendelea kukabiliana na changamoto mbalimbali. Maelezo kuhusu changamoto hizo pamoja na hatua zinazochukuliwa ni kama ifuatavyo:-

#### **3.6.1 Uwekezaji mdogo kwenye miundombinu ya maji ikilinganishwa na mahitaji ya kijamii na kiuchumi**

**267. Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Maji inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa huduma ya maji unaosababishwa na uwekezaji mdogo kwenye miundombinu ya maji ikilinganishwa na mahitaji ya kijamii na kiuchumi katika maeneo ya vijijini na mijini. Miji inakua kwa kasi kutokana na ongezeko la idadi ya watu, na kasi kubwa ya uwekezaji katika viwanda, biashara na ujenzi wa makazi. Vilevile, maeneo mengi ya miji mikuu ya wilaya, miji midogo na vijijini yanakua kwa kasi na idadi ya watu kuongezeka wakati huduma ya maji haitoshelezi. Ongezeko la watu mijini kitaifa ni wastani wa **asilimia 4.5** kwa mwaka tofauti na maeneo ya vijijini ambapo wastani wa ongezeko la watu ni **asilimia 2.3** kwa mwaka. Kwa Jiji la Dar es Salaam, ambalo linakabiliwa na uhaba mkubwa wa maji lina ongezeko kubwa la watu la **asilimia 6** kwa mwaka. Kasi kubwa ya ongezeko la idadi ya watu mijini na vijijini isiyowiana na uwekezaji kwenye miundombinu ya maji kumesababisha kuongezeka kwa mahitaji makubwa ya huduma ya maji nchini. Sababu zinazochangia changamoto ya uwekezaji mdogo usiolingana na mahitaji pamoja na hatua zinazochukuliwa zimefafanuliwa katika aya zifuatazo:-

##### **(a) Upatikanaji Mdogo wa Fedha kulinganisha na Bajeti**

**268. Mheshimiwa Spika**, bajeti inayokasimiwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji haikidhi mahitaji halisi ya utekelezaji wa miradi. Vilevile, kiasi cha fedha kinachotolewa ni chini ya kiwango kilichokasimiwa. Kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo, fedha za maendeleo za ndani zilizotolewa zilikuwa ni kidogo ikilinganishwa na fedha zilizokasimiwa. Katika mwaka 2012/2013, jumla ya **shilingi 140,015,967,000** zilikasimiwa ambapo fedha zilizotolewa zilikuwa ni **shilingi 104,000,000,000** sawa na upungufu wa **asilimia 25.7**; kwa mwaka 2013/2014, kiasi cha **shilingi 312,066,164,000** zilikasimiwa na kiasi kilichotolewa ni **shilingi 166,000,000,000** sawa na upungufu wa **asilimia 53.2**. Katika mwaka 2014/2015, fedha zilizokasimiwa ni **shilingi 312,066,164,000** na hadi mwezi Aprili, 2015 kiasi cha **shilingi 82,390,507,067** zimetolewa sawa na **asilimia 26.4**.

**269. Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na changamoto ya upatikanaji mdogo wa fedha, Wizara yangu imeendelea kuwahamasisha Washirika wa Maendeleo wanaochangia Mfuko wa Pamoja wa Sekta ya Maji kuongeza michango yao. Vilevile, Wizara inaendelea kuwashawishi washirika wengine wa maendeleo kuchangia katika Sekta ya Maji ili kuongeza fedha kwenye bajeti ndogo inayoelekezwa kwa Sekta. Washirika hao ni pamoja na Serikali ya Watu wa China, Serikali ya India, na Mifuko ya

Kimataifa ya Maendeleo kama *Saudi Fund for Development* na *OFID*, ambao wamechangia katika ujenzi wa Bwawa la Kidunda na mradi wa maji wa Same-Mwanga-Korogwe. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa kama *KfW* na *DFID* inakamilisha taratibu za kuanza kupata fedha za kukamilisha miradi kuititia Mipango ya *Output-Based Arrangement Funding* kwa Mamlaka za Maji Mijini na *Payments by Results Program* kutekeleza miradi ya maji vijijini. Aidha, Serikali ipo katika hatua za mwisho za maandalizi ya Sheria ya Mfuko wa Maji itakayotumika kusimamia mfuko huo ambao ulianza kutekelezwa mwaka 2013/2014 lakini kukosa chombo cha usimamizi wake.

#### **(b) Ushiriki Hafifu wa Sekta Binafsi katika Sekta ya Maji**

**270. Mheshimiwa Spika**, ushiriki wa Sekta Binafsi umejikita zaidi katika ujenzi wa miundombinu ya maji na suala la uendeshaji na usimamizi wa miradi umebakari kwenye Mamlaka za Maji, Halmashauri na Vyombo vya Watumiaji Maji. Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuiwezesha Sekta Binafsi kuongeza ushiriki wake katika uendeshaji wa miradi ya maji vijijini na mijini kuititia Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (*Public Private Partnership –PPP*). Hatua hizo ni pamoja na kutunga Sera ya Taifa ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ya mwaka 2009, Sheria ya Ubia ya mwaka 2010 na Kanuni zake. Pamoja na jitihada za Serikali kuweka misingi hiyo, Sekta Binafsi bado haijahamasika vya kutosha katika kushiriki kwenye kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwemo miradi ya maji.

**271. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeamua kuchukua juhudzi za makusudi za kuhakikisha Sekta Binafsi inashiriki kikamilifu katika kubuni, kujenga, kusimamia na kuendesha miradi ya maji. Ili kutimiza azma hiyo, Mamlaka za Maji zitajengewa uwezo wa kuandaa miradi ya maji itakayoendeshwa na Sekta Binafsi. Vilevile, Wizara itawajengea uwezo wataalam wake kwa kuwapatia mafunzo yanayohusu Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi na uwekezaji. Katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea kushirikiana na Washirika wa Maendeleo, Taasisi na Asasi mbalimbali ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya maji na usafi wa mazingira kuititia *PPP*.

#### **3.6.2 Kupungua kwa Rasilimali za Maji**

**272. Mheshimiwa Spika**, pamoja na nchi yetu kuwa na rasilimali za maji katika maeneo mengi, rasilimali hiyo imeendelea kupungua siku hadi siku na kusababisha uhaba wa maji kwa matumizi salama ya majumbani pamoja na shughuli za maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Upungufu huo unasababishwa na uchafuzi wa vyanzo vya maji, uvamizi katika vyanzo vya maji kwa ajili ya shughuli za kibinadamu, matumizi holela ya maji na mabadiliko ya tabianchi. Uchafuzi wa vyanzo vya maji umekithiri hasa kutokana na utiririshaji majitaka kutoka viwandani, shughuli za uchimbaji madini na kilimo cha umwagiliaji.

**273. Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na changamoto ya kupungua kwa rasilimali za maji, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wengine hususan *NEMC* imekuwa ikifanya ukaguzi wa mara kwa mara katika maeneo ya viwanda, migodi na

mabwawa ya kutibu majitaka ili kuhakikisha utupaji majitaka unafanyika kulingana na sheria, kanuni na taratibu za utunzaji mazingira ili kuvinusuru vyanzo vyetu visiendelee kuathiriwa. Vilevile, Wizara imeanza kutekeleza mpango wa kutunza na kuhifadhi vyanzo vya maji, kwa kubainisha na kuainisha vyanzo vilivyo katika hatari ya kuharibiwa ili maeneo hayo yawekewe mipaka na hatimaye kutangazwa kuwa maeneo tengefu. Hadi sasa jumla ya maeneo **tisa** yametangazwa kuwa maeneo tengefu na maeneo **31** yapo katika hatua za kutangazwa.

**274. Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imeendelea kutoa elimu kwa watumiaji maji kuhusu Sheria ya Rasilimali za Maji na Kanuni zake zinazosimamia matumizi ya maji kwa lengo la kudhibiti matumizi holela. Kanuni hizo ni *Regulations Regarding Water Abstraction, Use and Discharge Permits; na Ground Water (Exploration and Drilling) Licensing Regulations*. Aidha, vyombo vya usimamizi wa rasilimali za maji vilivyosajiliwa kisheria vimeendelea kuimarishwa ili kuhakikisha rasilimali za maji zinagawanya na kutumiwa kwa mujibu wa Sheria.

**275. Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali zikiwemo kujenga mabwawa madogo na makubwa kwa ajili ya kuhifadhi maji kwa matumizi mbalimbali; kuimarisha ukusanyaji wa takwimu zinazohusu rasilimali za maji na mabadiliko ya tabianchi; kutoa mafunzo kwa wataalam na kuelimisha umma ili kuongeza weledi kuhusu mabadiliko ya tabianchi; kutumia utaalam asilia (*Indigenous knowledge*) katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; na kushirikiana na taasisi za kiserikali na zisizo za kiserikali zinazofanya utafiti kuhusu mabadiliko ya tabianchi kwa lengo la kufanya utafiti wa pamoja na kutathmini matokeo ya tafiti hizo. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo inaandaa mipango itakayozingatia masuala ya athari za mabadiliko ya tabianchi ambayo ni pamoja na;

- (i) Mipango Shirikishi ya Uendelezaji na Usimamizi wa Rasilimali za Maji (*IWRM&DPs*); na
- (ii) Jukwaa la Majadiliano ya Athari za Mabadiliko ya Tabianchi katika Sekta ya Maji (*Water Sector Climate Change Coordination Mechanism Dialogue Forum*).

### 3.6.3 Uendelevu wa Miradi ya Maji Vijijini

**276. Mheshimiwa Spika**, tathmini ya jumla ya miradi ya maji vijijini iliyofanyika mwaka 2013 kupitia mpango wa *BRN*, ilibaini kuwa vituo **14,800** vya kuchotea maji sawa na **asilimia 40** ya vituo **37,000** vilivyojengwa zaidi ya miaka 20 iliopita, vilikuwa havifanyi kazi. Vituo hivyo vilikuwa vihudumie jumla ya watu **milioni 5.3** ya wakazi waishio vijijini. Sababu za vituo hivyo kutofanya kazi ni pamoja na:-

- (i) Kukosekana kwa mipango ya uendeshaji na matengenezo wakati wa kuandaa miradi ya maji vijijini;
- (ii) Uteuzi wa aina ya teknolojia sahihi kuendeleza chanzo cha maji;

- (iii) Kutokupatikana kwa wakati kwa vipuri vya miradi ya maji;
- (iv) Kiwango cha chini cha ufuatiliaji wa masuala ya kiufundi; na
- (v) Usimamizi hafifu wa makusanyo ya fedha za miradi.

Kutokana na upungufu huo, Wizara yangu imeandaa Mkakati wa Uendelevu wa miradi ya maji vijijini (*National Rural Water Supply Sustainability Strategy*) ambao utekelezaji wake utaanza katika mwaka wa fedha 2015/2016. Mkakati huo unasisitiza yafuatayo:-

- (i) Kuunda Vyombo vya Watumiaji Maji (COWSOs) na kuhimiza wasajili kuongeza kasi ya usajili wa miradi iliyopo na mingine itakayojengwa;
- (ii) Kuimarisha ukusanyaji wa takwimu sahihi za vituo vinavyotoa maji na visivyotoa maji kuitia mfumo wa kompyuta (*Water Point Mapping System-WPMS*);
- (iii) Kusaidia matengenezo makubwa ambayo yapo nje ya uwezo wa Vyombo vya Watumiaji Maji (COWSOs); na
- (iv) Kuwezesha kuwepo kwa maghala ya kuhifadhi vifaa na vipuri vya maji katika maeneo mbalimbali nchini pamoja na kuhakikisha uwepo wa wataalam na ushauri wa kitaalam katika maeneo ya vijijini.

### **3.6.4 Upotevu wa Maji**

**277. Mheshimiwa Spika**, uendeshaji wa miradi ya maji umeendelea kuathirika kutokana na upotevu mkubwa wa maji ambao hadi sasa ni wastani wa **asilimia 35** ya maji yanayozalishwa kwa Miji Mikuu ya Mikoa **23** na kwa upande wa Dar es Salaam upotevu huo ni **asilimia 57**. Kiwango cha upotevu wa maji kinachokubalika kimataifa ni **asilimia 20**. Upotevu huo husababishwa na hujuma kwenye miundombinu ya maji, wizi wa maji na miundombinu chakavu. Hali hiyo imesababisha Mamlaka hizo 23 za Maji Mijini kupoteza kila mwezi jumla ya **shilingi bilioni 1.83** za mauzo ya maji na kwa Jiji la Dar es Salaam, jumla ya **shilingi bilioni 2.64** hypotea kila mwezi. Upotevu huo wa mapato umesababisha Mamlaka za Maji Mijini kushindwa kulipia ghamama za uendeshaji na matengenezo ya miundombinu na hivyo, Serikali kulazimika kubeba mzigo huo ili kuondoa kero ya uhaba wa maji kwenye maeneo mbalimbali nchini.

**278. Mheshimiwa Spika**, hatua zinazochukuliwa za udhibiti wa maji yanayopotea bila kulipiwa ni kwa Mamlaka za Maji Mijini kufunga dira za maji kwa wateja wote waliouanganishiwa huduma ili kubaini matumizi yao halisi. Upotevu wa maji ni kiashiria kimojawapo kwenye Mkataba wa Makubaliano uliosainiwa tarehe 02/02/2015 kati yangu na Wenyeviti wa Bodi za Mamlaka za Maji Mijini katika kutekeleza mpango wa *BRN* kwa maji mijini. Vilevile, Wizara imekamilisha rasimu ya mapitio ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji **Na. 11** na Sheria ya Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira **Na. 12** ili kuzipa nguvu zaidi za kukabiliana na watakaobainika kuhusika na wizi wa

maji, vifaa na uharibifu wa miundombinu ya maji. Uboreshaji wa sheria hizo uko kwenye hatua za mwisho na utakapokamilika, miswada ya sheria hizo itawasilishwa kwenye Bunge lako Tukufu.

**279. Mheshimiwa Spika**, kwa Jiji la Dar es Salaam, Kikosi Maalum cha Wataalam wa Wizara na vyombo mbalimbali nya Dola, kiliundwa ili kubaini wezi wa maji na kuwafikisha kwenye vyombo nya sheria. Hadi mwezi Aprili 2015, kuna jumla ya kesi **163** zilizopo mahakamani na watuhumiwa **23** wa kesi hizo wamepewa adhabu mbalimbali zikiwemo kutumikia kifungo au kulipa faini na kesi zilizobaki zinaendelea.

#### **4.0 SHUKRANI**

**280. Mheshimiwa Spika**, napenda sasa kuchukua fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia kuiwezesha Wizara yangu kufanikisha majukumu yake. Nakiri kwamba mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2014/2015 ni kutokana na jitihada za pamoja, ushirikiano na misaada ya kifedha na kitaalam kutoka kwa Wadau mbalimbali. Wadau hao ni pamoja na nchi wahisani, mashirika ya maendeleo ya kimataifa, taasisi zisizo za kiserikali, mashirika ya kidini, na taasisi za kifedha. Napenda kuzishukuru nchi rafiki zikiwemo Serikali za Ujeruman, Uholanzi, Uingereza, Marekani, Japan, Hispania, Ufaransa, China, Uswisi, Ubeligiji, Ireland, Korea Kusini, Sweden, Denmark, Norway, India, Misri, Saudi Arabia na Kuwait.

**281. Mheshimiwa Spika**, vilevile, natoa shukrani kwa taasisi za fedha za kimataifa na mashirika ya kimaendeleo kwa misaada ya fedha na ushirikiano wa kitaalam katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu na malengo ya Wizara yangu. Taasisi hizo ni pamoja na:- Benki ya Dunia (*WB*), Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*), Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (*KfW*), Benki ya Maendeleo ya Ufaransa (*AFD*), Benki ya Uwekezaji ya Umoja wa Ulaya (*EIB*), Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika (*BADEA*), Mfuko wa Maendeleo wa Nchi Zinazozalisha Mafuta (*OPEC Fund for International Development-OFID*), Mfuko wa Maendeleo wa Saudia (*SFD*), Umoja wa Ulaya (*EU*), Shirika la Marekani la Changamoto za Milenia (*MCC*), Shirika la Misaada ya Maendeleo la Norway (*NORAD*), Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (*DFID*), Shirika la Maendeleo la Ujerumani (*GIZ*), Mpango wa Umoja wa Mataifa wa Maendeleo (*UNDP*), Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan (*JICA*), Mpango wa Umoja wa Mataifa wa Makazi Duniani (*UN HABITAT*), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (*UNICEF*), Shirika la Misaada ya Maendeleo la Sweden (*SIDA*), Shirika la Misaada ya Maendeleo la Canada (*CIDA*), Shirika la Misaada ya Maendeleo la Denmark (*DANIDA*) na Shirika la Misaada la Marekani (*USAID*).

**282. Mheshimiwa Spika**, aidha, michango ya mashirika ya kidini imeongeza hamasa katika kuyafikia malengo tuliojiwekea. Hivyo, napenda kuyashukuru mashirika hayo ya kidini ya *World Islamic League*, Shirika la *Ahmadiya Muslim Jamaat Tanzania*, *Islamic Foundation*, Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania, Kanisa la Kilutheri la Ujeruman, Baraza Kuu la Waislam Tanzania, Kanisa Katoliki Tanzania, Kanisa la Kianglikana Tanzania, *Catholic Agency for Overseas Aid and Development (CARITAS)*, *Adventist Development Relief Agency (ADRA)*, *Norwegian Church Aid* na *Livingwater International*. Pia, nazishukuru taasisi zisizo za kiserikali za *Tanzania Water and Sanitation Network (TAWASANET)*; Wahamasishaji wa Maji, Maendeleo na Afya (*WAMMA*); *Southern Highlands Participatory Organizasition (SHIPO)*; *WaterAid*; *World Vision*; *Plan International*; *Concern Worldwide*; *Netherlands Volunteers Services (SNV)*; Shirika la Kimataifa la Kuhifadhi Uasili na Mali Asili (*IUCN*); *World Wide Fund for Nature (WWF)*; *African Medical Research Foundation (AMREF)*; *Clinton HIV Aids Initiative (CHAI)*; *Bill and Melinda Gates Foundation*; na wale wote ambao wameendelea kuisaidia Wizara ya Maji kufanikisha malengo yake.

**283. Mheshimiwa Spika**, pia, naomba nimshukuru **Bw. Phillippe Dongier**, Mkurugenzi Mkazi wa Benki ya Dunia kwa nchi za Burundi, Uganda na Tanzania anayemaliza muda wake. Kuwepo kwake nchini tangu mwaka 2012 hadi atakapomaliza rasmi muda wake tarehe 30/06/2015 kumewezesha Sekta ya Maji kupata mafanikio makubwa katika kuwapatia wananchi huduma ya maji vijijini na mijini. Napenda kumtakia heri na fanaka katika kituo chake kipyra cha kazi. Aidha, nachukua fursa hii kumkaribisha Mkurugenzi Mkazi mpya, **Bi. Bella Bird** atakayeanza rasmi kazi tarehe 01/07/2015. Tunamuahidi kumpatia ushirikiano wa kutosha utakaozidi kuongeza chachu kwenye harakati za maendeleo ya nchi yetu.

**284. Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya kipekee kabisa naomba nitumie fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa **Mhe. Amos Gabriel Makalla (Mb)**, Naibu Waziri wa Maji; **Mhandisi Mbogo Futakamba**, Katibu Mkuu; Wakurugenzi wote, Wakuu wa Vitengo, Wataalam na Watumishi wote wa Wizara; na Maafisa Watendaji Wakuu wa Mashirika, Wakala na Taasisi zilizo chini ya Wizara yangu kwa ushirikiano wanaonipatia pamoja na kujituma kwao kwa kusimamia utekelezaji wa majukumu yao kwenye Sekta ya Maji kwa kiwango cha hali ya juu. Napenda pia, nimshukuru aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, **Mhandisi Bashir Juma Mrindoko** ambaye amestaafu kwa heshima. Ni matumaini yangu kuwa huko aliko kwa sasa anaendelea kuwa balozi mzuri wa Sekta ya Maji.

**285. Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya kipekee nachukua fursa hii kuishukuru sana familia yangu, akiwemo mke wangu mpenzi **Kudra Maghembe** na watoto wetu **Dkt. Ngwaru Maghembe**, **Dkt. Mwanamkuu Maghembe**, **Namcheja** na **Namvumo Maghembe** kwa upendo, ushirikiano pamoja na msaada wao katika kipindi chote na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi uliohitajika. Familia yangu inaendelea kuwa nguzo muhimu katika maisha yangu.

**286. Mheshimiwa Spika**, vilevile, ninayo furaha kubwa kuendelea kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Mwanga amba wamekuwa nami bega kwa bega katika kipindi chote cha miaka mitano iliyopita. Natumaini tutaendelea kushirikiana katika kipindi kijacho ili kuiletea maendeleo Wilaya yetu na Taifa kwa ujumla. Napenda kuwashakikishia kuwa nitaongeza nguvu zaidi ili Wilaya yetu ya Mwanga iwe moja ya Wilaya bora nchini.

## **5.0 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2015/2016**

**287. Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **shilingi 458,900,981,000** kwa ajili ya matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka 2015/2016, ili Wizara iweze kutekeleza majukumu na malengo yaliyoelezwa katika hotuba hii. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida ni **shilingi 31,643,077,000** ambapo **shilingi 13,682,361,000** sawa na **asilimia 43.3** ni kwa ajili ya kugharamia Matumizi Mengineyo (**OC**) na **shilingi 17,960,716,000** sawa na **asilimia 56.7** ni kwa ajili ya kulipa mishahara (**PE**) ya watumishi wa Wizara na Chuo cha Maji. Jumla ya bajeti ya maendeleo ni **shilingi 427,257,904,000** ambapo kati ya

fedha hizo **shilingi 315,000,000,000** sawa na **asilimia 74** ni fedha za ndani na **shilingi 112,257,904,000** sawa na **asilimia 26** ni fedha za nje.

**288. Mheshimiwa Spika**, naomba tena nitoe shukrani zangu kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara kwa anwani: [www.maji.go.tz](http://www.maji.go.tz).

**289. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.